# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Arobaini na Nne - Tarehe 6 Juni, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2013/2014.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. DAVID E. SILINDE (MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na swali la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na atakayeuliza swali letu la kwanza ni Mheshimiwa Omar Rashid Nundu.

Na. 351

**Wananchi Kuuawa kwa Tuhuma za Wizi Mdogo Mdogo**

**MHE. OMAR R. NUNDU** aliuliza:-

Kumezuka hulka mbaya kwa baadhi ya watu kuchukua sheria mkononi mwao kwa kuwaua wenzao kutokana na tuhuma za wizi mdogo mdogo kama wa simu za mkononi na kadhalika:-

(a) Je, ni Wananchi wangapi wameuawa katika mazingira haya?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha vitendo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2012 hadi Aprili, 2013 jumla ya watu 1,666 waliuawa kwa kupigwa na Wananchi waliojichukulia Sheria mkononi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikichukua hatua za kisheria, ikiwa ni pamoja na kuwakamata watuhumiwa wote wanaohusika na matukio ya aina hiyo na kuwafikisha Mahakamani. Aidha, Jeshi la Polisi chini ya dhana ya utii wa sheria bila shuruti, hutoa mafunzo kupitia vyombo vya habari ili kuwaelimisha Wananchi umuhimu wa kufuata Sheria, pia kuwashirikisha Viongozi wa Dini kuwataka waumini wao kuacha ukatili. Serikali inalaani vikali tabia ya Wananchi kujichukulia sheria mkononi na inawataka Wananchi kufuata sheria za nchi.

**MHE. OMAR R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya ufasaha lakini ya kusitusha kutokana na idadi kubwa ya watu ambao wameuwa kwa kipindi kifupi na ukichukulia kuwa uhai wa binadamu ni tuzo nadhimu ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia:-

(i) Je, ni kesi ngapi za mauaji ya aina hii zimekwishatolewa hukumu na hukumu hizo ni za aina gani?

(ii) Kwa kuwa Vituo vya Polisi vikiwa karibu na sehemu ambazo zimejificha husaidia kujua uhalifu unaotokea; na kwa kuwa kuna vitu vingi ambavyo vimejengwa kwa muda mrefu ambavyo mpaka leo havina Polisi kama kile ambacho kipo kwa Munduwangu, Kijiji cha Mwambani kule Tanga kilichojengwa takribani miaka mitano iliyopita na kinaota nyasi tu lakini hakuna polisi. Sasa ni hatua gani Serikali inachukua kuhakikisha kuwa Polisi wako karibu na sehemu ambayo matukio kama haya yanaweza kutokea ili kuyazuia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu kesi ngapi. Kesi nyingi ambazo zimetokea katika suala hili bado ziko kwenye upelelezi, kwa sababu hii ni *mob justice* na siyo rahisi kupata msaada wa Wananchi katika kuwaonesha wahusika.

Pamoja na hivyo, bado upelelezi unaendelea kwenye kesi nyingi za namna hii na nyingine zimefikia hatua karibu kuzipeleka mahakamani.

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu vituo vya polisi; naomba niseme kwamba, Vituo vya Polisi kuwa kwenye maeneo mengi ni faida, lakini siyo Vituo vya Polisi ambavyo vitatufanya tusiuane kiholela. Hili ni suala la elimu, kuthamini maisha na kutaka kila mtu, kila raia, akubali kutii sheria bila shuruti, lakini pia kwa yule ambaye anamwona mwenzake bado analegalega, amsaidie kumuweka sawa.

Mheshimiwa Spika, suala muhimu pamoja na Wananchi wenyewe kukataa kuuana, kuna doria ambazo tunazifanya katika maeneo mengi; hizi ndizo ambazo zinaweza zikasaidia kuliko kusema kila litakapotokea tukio pawe na kituo. Pamoja na hayo, vituo ambavyo vimeshajengwa na bado havijawekewa askari, hili tunalifanyia kazi lakini mara nyingi kuna *standards* au mambo ambayo yanakuwa hayajatimia, ndiyo maana inakuwa tabu kupeleka askari. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama ana *specific issue* au kituo, tutalizungumza na tutalifanyia kazi kama tutakavyokubaliana.

**SPIKA:** Ahsante. Sikuona wengine walioomba, tunaenda swali linalofuata; Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa!

Na. 352

**Raia wa Kigeni Kuhesabiwa na Kujipatia Vitambulisho vya Taifa**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Zoezi la uandikishaji wa Vitambulisho vya Taifa linaendelea katika nchi yetu ambayo inazungukwa na nchi nyingine zenye migogoro:-

(a) Je, raia wa nchi nyingine hawawezi kujipatia vitambulisho hivyo?

(b) Je, zoezi la kuhesabu watu (sensa) halikuwagusa raia wa nchi nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa nchi yetu imezungukwa na nchi zenye migogoro; hivyo, kutoa viashirio vya kuweza kuandikisha watu wasiostahili. Kwa kulitambua hilo, *NIDA* inaendesha zoezi hili kwa umakini na kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali kama vile TAMISEMI*, RITA* na Uhamiaji ili kuthibitisha makazi ya mwombaji, kutambua umri wa mwombaji na kupata uthibitisho wa uraia wa mwombaji kabla ya kutoa kitambulisho.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa hatuandikishi watu wasiohusika, Serikali imepeleka Madaftari ya Wakazi yanayoratibiwa na Serikali za Mitaa, ambayo lengo lake kubwa ni kuandikisha wakazi wote wa kila kaya zilizo katika kijiji au shehia na kuzihifadhi taarifa hizo. Taarifa zilizoko kwenye Madaftari ya Wakazi ndizo zitakazotumika kumwandikisha mwombaji wa kitambulisho cha Taifa kama kigezo kikuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujaza fomu ya maombi, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kijiji au Shehia, ikijumuisha Wajumbe wa Vitongoji, itachambua maombi hayo na kubainisha watu ambao siyo Raia wa Tanzania. Hatua hii itazuia raia wa nchi nyingine kuweza kujipatia Vitambulisho vya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuhesabu watu lina lengo la kujua idadi ya watu waliopo nchini. Katika kutekeleza zoezi hilo, kila mtu anayehesabiwa hutakiwa kutoa taarifa

ya uraia wake. Lengo la kufanya hivyo ni kuiwezesha Serikali kutambua nani ni raia na nani siyo raia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa swali la nyongeza, naomba kidogo msimame ninyi mlioomba.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya kumwuliza kama ifuatavyo:-

(i) Sote tunaelewa kuwa zoezi la sensa lililopita, lilikumbwa na matatizo kiasi kwamba wako baadhi ya Watanzania wenzetu hawakutaka kujiandikisha au hawakuandikishwa na wao pia wanayo haki ya kupata vitambulisho. Katika mazingira hayo ambayo mtu hakuandikishwa kwenye sensa, lakini anataka kitambulisho cha Utanzania na anayo haki ya kupata; inakuwaje katika suala hilo?

(ii) Kielelezo cha msingi cha mtu kuandikishwa kuwa raia au kupata haki za uraia ni cheti chenyewe cha kuzaliwa na tunaielewa nchi yetu kwa sasa kuwa mara nyingi fedha zinakufanya upate kitu hata kama siyo haki yako. Inapotokea watu wamepewa vyeti vya kuzaliwa kwa kununua halafu wakapewa Vitambulisho vya Taifa ambavyo vitawafanya wawe Watanzania wa kudumu. Katika mazingira hayo Serikali inatoa tamko gani na hivi vitu siyo vigeni kwa sababu kuna watu hivi sasa tunaelewa wapo Tanzania Bara lakini wanakuja Zanzibar wanapiga kura, wako watu wa nchi nyingine wanapiga kura hapa na tunajua hilo. Je, unatoa kauli gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khalifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kulitokea matatizo katika uandikishaji wa watu kwenye sensa iliyopita, lakini naomba niseme kwamba, utaratibu wa kuandikisha

na kutoa vitambulisho hauendani moja kwa moja na sensa iliyopita. Vina uhusiano, lakini usajili wa watu unafanywa kivyake na hilo ndiyo muhimu kwamba, madaftari tumeyatoa na watu wanafuatwa kwenye kaya zao kuandikishwa. Hapo ndipo ambapo mtu ambaye hakuandikisha anaweza akapata tatizo, lakini siyo lazima mtu aliyeandikishwa sensa ndiyo apate kitambulisho; hilo haliko sawa kwa sababu siku ya sensa wengine hawakulala nchini. Kwa hiyo, wote hao watapata vitambulisho ikiwa mchakato huu wa vitambulisho utafuatwa na kukamilika ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyeti vya kuzaliwa na uraia na Vitambulisho vya Kitaifa. Kama nilivyosema awali ni kwamba, nguvu kubwa ya kuamua na kuhakiki nani ni Mtanzania wa kuzaliwa ni kijijini alikotoka. Sasa nguvu tunaziweka huko ili ile Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kijiji ndiyo ambayo inajua nani kamzaa nani na nani mjukuu wa nani. Kwa hiyo, kwa kutumia daftari ambalo tumelipeleka, tuna hakika kwamba, mtu ambaye amefoji cheti kama sote tutakuwa wawazi na kutaka kuilinda hii nchi, hakuna raia wa nje mwenye cheti atakayepata Kitambulisho cha Taifa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa zoezi la uandikishaji wa vitambulisho vipya limekuwa likiendelea lakini mpaka hivi sasa ni Viongozi pekee ndiyo ambao wamekuwa wakipata. Sasa ningependa tupate kauli ya Serikali kwa sababu tunatarajia vitambulisho hivi vinaweza vikaenda mpaka kupigia kura katika uchaguzi ujao. Je, ni lini sasa Serikali itamaliza zoezi hili la kuandikisha Wananchi wote na kupata vitambulisho hivi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Silinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, *speed* ambayo inakwenda zoezi hili siyo tuliyoitegemea. Mpaka sasa walioandikishwa zaidi ni Wafanyakazi wa Serikali wa Bara

na Zanzibar, wameandikishwa pia watu wa Kilombero kwa sababu kulikuwa na majaribio na watu wengine wa kawaida Dar es Salaam. Jumla ya watu kama 2,700,000 wameshaandikishwa. Hata hivyo, lengo hasa la zoezi hili na lini limalizike, tulikuwa tumepanga limalizike mwaka unaokuja. Mwaka 2014 tuwe tumelimaliza na vitambulisho hivi viwe ni sehemu katika mchakato wetu wa kupiga kura na kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, kweli kuna tatizo na tatizo hasa lipo kwenye bajeti. Mahitaji ya *NIDA* kwa ajili ya shughuli hii hayafikiwi kwenye bajeti na tunaishukuru Serikali, mwaka huu imepiga hatua kuliko ilivyofanya mwaka jana, lakini tuna *gap* ya hatua na fedha hasa kwenye vifaa vya kuchukulia alama za vidole pamoja na picha za waandikishwaji. Tunategemea kwamba, pengine mwaka huu tunaweza tukaongezewa fedha kwa utetezi wetu sisi lakini pia na Waheshimiwa Wabunge. Pia mwakani tukifanikiwa kuiziba hiyo *gap, speed* itaongezeka na tunaweza tukakamilisha kwa wakati unaotakiwa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa zoezi hili la uandikishaji kupata Vitambulisho vya Taifa ni muhimu hasa kwenye suala la kuhamasisha Watanzania kuweza kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa na ni mradi mkubwa; na kwa kuwa kuna *Project* ya *Big Results Now*; Serikali haioni kuna umuhimu wa kuwekeza kwenye mradi huu kwa haraka ili ukamilike kwa wakati ambayo itasaidia pia kwenye kura ya maoni, kwenye Katiba na Uchaguzi Mkuu ujao, badala ya kusuasua ambayo inaweza ikasababisha vurugu katika chaguzi na mambo ya kuongeza Pato la Taifa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Unajua maswali mengine yana-*repeat themselves*, lakini naomba ujibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbatia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo ya Serikali ni lipi liingie kwenye *labs* vitambulisho havikuingia. Vitambulisho vilichukuliwa kama ni kipaumbele cha Taifa na Serikali inatambua umuhimu wa vitambulisho. Lazima tushukuru kwamba tulivyotoka mwaka jana ambapo tulipata bilioni kumi kwa ajili ya shughuli hii na mwaka huu kupata 251, ni hatua tayari ya Serikali. Pamoja na hivyo, nafikiri nipo *optimistic* kwamba, mwakani tutamaliza zoezi hili na Serikali ipo *conscious* kwenye hilo na umuhimu wake.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vitambulisho hivi mchakato wake umeanza muda mrefu sana huko nyuma na ulisuasua kutokana na sababu mbalimbali na leo tunapewa sababu kwamba, kuna upungufu wa fedha na hatujajua kama fedha hizi zitatengwa au zitapatikana mwakani. Je, Serikali sasa pamoja na sisi Wabunge tunajiandaaje ili hizi fedha zipatikane kwa wakati mwafaka na vipande hivi vipatikane kabla ya uchaguzi wa mwaka 2015?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, suala la kutenga fedha kwa ajili ya kumaliza utayarishaji wa Vitambulisho vya Taifa litakamilika. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi, mpango wa fedha umekamilika na tuna uhakika tutamaliza.

**SPIKA:** Maswali ya nyongeza saba haiwezekani, isipokuwa Wabunge mkafanye uhamasisho kwa watu wajitokeze kupata vitambulisho. Nadhani ndiyo kubwa la kufanya. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Martha Mlata, atauliza swali hilo.

Na. 353

**Ruzuku ya Mbolea na Pembejeo za Kilimo**

**MHE. MARTHA M. MLATA** aliuliza:-

Serikali imeendelea kutoa ruzuku ya mbolea na pembejeo za kilimo kwa ajili ya mazao ya chakula na

biashara kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao, kuongeza Pato la Taifa na la mkulima:-

Je, Serikali inatambua kwamba kuna baadhi ya mazao ambayo ni chakula na pia yanatumika kama zao la biashara hivyo ione jinsi ya kuyapa kipaumbele zaidi kwa ruzuku hizo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, baadhi ya mazao ambayo ni ya chakula pia yanatumika kama mazao ya biashara katika sehemu mbalimbali hapa nchini. Mfano, mazao ya mahindi na mpunga, ambayo Serikali imekuwa ikiyapa ruzuku ya mbolea pamoja na mbegu bora kwa miaka mitano mfululizo.

Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Serikali ilitoa ruzuku ya tani 126,117 za mbolea ambapo kaya 940,783 zilinufaika na tani 8,278 za mbegu bora za mahindi na tani 1,694 za mbegu bora za mpunga ili kuboresha uzalishaji wa mazao hayo na kuhakikisha wakulima wanapata chakula cha kutosha na kuwaongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2013/2014 hadi 2015/2016, Wizara kupitia Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*), imejiwekea malengo ya kuongeza uzalishaji kwa kiasi cha mahidi tani 100,000 na mchele tani 290,000 katika mashamba mapya ya wakulima wakubwa na wadogo. Kwa wakulima wadogo, katika mwaka wa 2013/2014, Serikali itatumia shilingi bilioni 91.5 kugharimia ruzuku ya pembejeo za mazao zikiwemo mbolea, mbegu, miche na viatilifu. Aidha, lengo la Wizara yangu ni kuwawezesha wakulima kuzalisha chakula kwa wingi na kuwaruhusu kuuza ziada ya mazao ndani na nje ya nchi bila vikwazo vyovyote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mlata, swali la nyongeza. Naomba msimame kidogo; Mheshimiwa Mlata endelea, lakini ninyi wengine simameni kidogo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ambayo amenipatia Mheshimiwa Waziri.

(i) Ni kweli katika tani alizozitaja, tani kumi za mtama ndizo zilizokuja kwenye Mkoa wa Singida, lakini alizeti zilikuwa tani nane tu na mbolea ya Minjingu ilikuwa tani 63. Hatukuweza kupata ruzuku kwenye mazao ya mahindi, ambayo mahindi ni zao la biashara la pili katika Mkoa wa Singida na Zao la Mpunga ambalo linalimwa kwa wingi sana kule Mgungira. Sasa napenda kujua kama Serikali inatambua kwamba, kuna kituo ambacho kinazalisha mbegu bora ambacho kipo Mpambaa Mtinko ili waweze kukiingiza katika utaratibu wa kutoa ruzuku na Mkoa wa Singida uweze kupata ruzuku ya mahindi?

(ii) Kwa nini Serikali inakataza mazao mengine yasilimwe katika Mkoa wa Singida na hali mazao mengine yakiwa yanalimwa; kwa mfano mahindi; kwa nini isiache mahindi pia yakalimwa kama zao la biashara? Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mlata, kama, ifuatavyo:-

Kwanza, kama nilivyosema, mazao yote haya, mahindi na mpunga, yanaweza yakawa ya chakula na wakati huo huo yakawa ya biashara mradi tu uzalishe ziada na yauzwe nje. Sasa kuhusu kwa nini mazao fulani hayaruhusiwi na mengine yanaruhusiwa. Katika nchi hii tunakwenda na *agro-ecological zones*. Mikoa ya Kati, mvua zake siyo nzuri, lakini hata hivyo, katika Mikoa hii na hususan Mikoa wa Singida, yapo maeneo mengine yanayopakana na Mkoa wa Singida, ambayo mvua zake niyo nzuri. Sisi tunachokifanya ni kuangalia pale ambapo mvua siyo nzuri, basi tunasema walime mazao ambayo

yanaweza kustahimili ukame. Ninakubaliana na Mheshimiwa Mlata kwamba, yapo maeneo katika Mkoa wa Singida, ambayo mvua zake ni nzuri na kwa kweli hatuna sababu ya kusema kama mvua ni nzuri katika maeneo fulani basi tuwazuie kabisa. Kuhusu hicho kituo, nitatuma wataalamu watakwenda pale watakitazama, kwa sababu vituo vyote viko chini.

Mheshimiwa Spika, labda nimalizie tu kwa kusema kwamba, Mkoa wa Singida ni mmoja wa mikoa ambayo haikupatwa na kashfa yoyote ile katika ubadhirifu wa pembejeo. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Mlata, kwa kufuatilia suala hili.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kayombo!

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa takwimu zinaonesha kwamba, mara Serikali ilipoanza kutoa ruzuku kwenye mazao haya, uzalishaji katika mazao haya umeongezeka sana na kwa hiyo, wakulima hasa wa Mkoa wa Ruvuma kwenye Zao la Mahindi wanapata matatizo ya soko.

Je, Serikali haioni kwamba wakati sasa umefika wa kufikiria kutoa ruzuku kwa ajili ya kununua mashine za kukoboa na kusaga haya mahindi ili wale wakulima waweze kuuza unga badala ya kuuza mahindi?

**SPIKA:** Hakulielewa swali naomba urudie!

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Kwa kuwa huu mfumo wa ruzuku umeonesha matokeo mazuri kwa maana ya ongezeko la mazao hasa ya mahindi:-

Je, Serikali haioni kwamba, wakati umefika sasa wa kutoa ruzuku ya fedha kwa wakulima hawa hasa wa kule Mbinga, Songea na Namtumbo, kwa ajili ya kununua mashine za kukoboa na kusaga hayo mahindi ili waweze kuuza unga badala ya kuuza mahindi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kayombo, kama ifuatavyo:-

Kwa sasa tunatoa ruzuku kwa ajili ya pembejeo, hata ruzuku yenyewe ya pembejeo haijawatosha wakulima ambao tunawalenga. Sasa tukiingia kwenye kutoa ruzuku ya fedha kununulia mashine, bado muda huo utakuwa haujafika. Ninachoweza kusema tu ni kwamba, tuna utaratibu mzuri tu wa kuwasaidia wakulima ili kujipatia mashine kama hizi anazozisema Mheshimiwa Kayombo. Tunao Mfuko wa Pembejeo ambao unakopesha wakulima fedha kwa riba nafuu, kiasi cha asilimia saba kwa mwaka, unaweza kujipatia fedha hizo ukanunua mashine za kukoboa mahindi au kukamua mafuta ya alizeti. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Kayombo na Wabunge wote, tutumie fursa hii, uko Mfuko huu, iko pia Benki ya *TIB,* zote zinatoa fursa hizi za kukopesha wakulima kujipatia fedha kwa ajili ya usindikaji wa mazao.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Mwaka wa Fedha wa 2013/14, Serikali imekuja na utaratibu mpya wa kukopesha pembejeo kwenye vikundi hususan kwa vijana; na kwa kuwa tunajua hali ya hewa wakati mwingine inaweza ikawa mbaya, vijana wakalima lakini hawapati mafanikio. Wakati huo huo wanakuwa wanadaiwa ule mkopo. Sasa; je, Serikali ina mkakati gani au imeandaa utaratibu gani kama vile kuwa na bima kwa vijana hawa wanaokopa mkopo kupita *CRDB* ili wasije wakapata matatizo badala ya kuinuliwa kiuchumi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchuchuli, kama ifuatavyo:-

Kwanza, utaratibu huu mpya wa mikopo, tumesema nao bado haujawa sahihi kabisa, kwa sababu vikundi vyenyewe havijulikani kwa uhakika katika nchi nzima. Katika maeneo vipo, kwa hiyo, tumesema tuaanza na maeneo yale tu ambayo vikundi vinajulikana kwa uhakika na

vinakopesheka. Sasa kuhusu kinga kwamba, imetokea dharura kama hiyo; nadhani hilo ni suala zuri na ndiyo maana hata kwa upande wa mazao tumesema tutakuja na utaratibu wa *price stabilisation fund* yanapotokea matatizo kama hayo. Jambo hili nadhani ni zuri, mimi nalichukua, tunatakiwa kulijadili pamoja na vyombo vinavyohusika, kuweka kinga kama hizo, bima ya mazao. Nadhani ndungu zangu linajadilika hili, ni wazo zuri.

**MH. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Katika msimu wa kilimo uliopita Wananchi wa Mkoa wa Manyara walilazimishwa kusainishwa vocha ya mbolea, ukiachilia mbali ya mbegu. Wao walihitaji Mbegu lakini mawakala wakawalazimisha wasaini ya mbolea ambayo hawahitaji. Walitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya na hakuna hatua zilizochukuliwa. Naomba nifahamu kutoka kwa Waziri; je, ni azma ya Serikali kushirikiana na mawakala kuwaibia Wananchi hawa?

**SPIKA:** Wewe Gekul kwani waliwaibia? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri majibu!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gekul, kama ifuatavyo:-

Ni kweli zoezi la kutoa pembejeo kupitia vocha limekuwa na changamoto nyingi. Wapo wajanja wengi, wala siyo mawakala tu, hata baadhi ya watendaji ambao walishiriki katika mazoezi hayo. Ninachoweza kusema ni kwamba, hao ni wezi na ni waharifu kama waharifu wengine na Serikali haijashirikiana nao. Sasa niseme nimelichukua hilo. Sisi tunafanya zoezi la kuwabaini watu wote hawa tuwafikishe mahakamani. Kwa hiyo, hata huko kwako Mheshimiwa nitakuja, nitawatuma na watakapobainika watakamtwa tu wafikishwe Mahakamani.

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata,

Mheshimiwa Suleiman Nchambi Suleiman, alitakiwa kuuliza lakini kwa niaba yake Mheshimiwa Mansoor!

Na. 354

**Uchimbaji wa Mabwawa kwa Ajili ya Kilimo Kishapu**

**MHE. MANSOOR S. HIRAN (K.n.y. MHE. SULEIMAN N. SULEIMAN)** aliuliza:-

Jimbo la Kishapu lina ukosefu wa mvua kwa kiwango kikubwa hivyo kusababisha kilimo Jimboni humo kuwa duni:-

Je, ni lini Serikali itachimba mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa kuwa tunayo mito mikubwa?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman N. Suleiman, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua changamoto inayowakabili Wananchi wa Jimbo la Kishapu, ukizingatia kwamba Kishapu ni moja ya maeneo ambayo yanaathiriwa na ukame wa mara kwa mara unaosababisha uhaba wa chakula na hivyo, Serikali kulazimika kuwapelekea chakula cha msaada. Kwa upande mwingine, Wilaya ya Kishapu inazo fursa za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji hususan kwa kuvuna maji ya mvua katika mabonde yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Kishapu, Mheshimiwa Suleiman Nchambi, amekuwa akifuatilia uanzishaji wa Miradi ya Umwagiliaji yeye mwenyewe binafsi. Nampongeza sana kwa jitihada hiyo. Kinachotakiwa sasa ni kuibua miradi ya ujenzi wa mabwawa na miundombinu mingine ya umwagiliaji na kuiweka katika mipango ya maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ya Kishapu ili iweze kujadiliwa, kupitishwa na kuombewa fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, tayari hatua zimeanza kuchukuliwa, ambapo wataalam wa umwagiliaji kutoka Ofisi ya Kanda ya Ziwa kwa kushirikiana na Wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, wamekamilisha usanifu wa mabanio mawili ya Ngeme na Nyenze hekta 267, kwa ajili ya utekelezaji kupitia Mradi wa *DASIP* (Mradi wa Nyenze). Aidha, natumia fursa hii kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wataalam wa Umwagiliaji wataendelea kufanya uchunguzi wa maeneo yote yanayofaa kwa kujenga mabwawa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu na kufanya usanifu wa miradi hiyo ili itafutiwe fedha za utekelezaji kutoka Serikali na katika vyanzo vingine vya fedha.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Wilaya ya Kwimba ni jirani na Wilaya ya Kishapu. Kwenye Wilaya ya Kwimba tuna Mradi wa Umwagiliaji wa Mahiga ambao uko chini ya Serikali Kuu. Leo una miaka mitatu, huo Mradi unasuasua haueleweki unaisha lini. Naomba Waziri au Serikali itoe tamko kwamba huo Mradi utaisha lini, nauliza swali hilo kwa sababu hata Halmashauri ya Wilaya haifahamu Mradi utaisha lini? Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mansoor, kama ifuatavyo:-

Naomba nimfahamishe kwamba, nimepata taarifa ya huu Mradi wa Mahiga na kwamba unasuasua. Sasa ninamuahidi kwamba, nitaufuatilia kuanzia leo hii. Nitatuma wataalam wafuatilie ni nini kinausibu Mradi huu maana ni wa siku nyingi, ulishapata fedha tangu miaka ya nyuma. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba, Mradi huu unakarabatiwa. Ninamhakikishia kwamba, nitafuatilia.

**SPIKA**: Shida yangu mmesimama wengi, wote watasema miradi ya kwao itawezekana kweli? Mheshimiwa Chibulunje na Mheshimiwa Lembeli mtauliza maswali hayo. Kwanza, Mheshimiwa Chibulunje!

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa yapo mabwawa ya zamani yaliyochimbwa katika baadhi ya maeneo kame hapa nchini na sasa hivi yanahitaji ukarabati. Nataka Mheshimiwa Waziri anifahamishe wana mpango gani wa kuyakarabati mabwawa haya ya zamani ili yaweze kuwa na uwezo wa umwagiliji, yakiwemo Mabwawa ya Ikowa na Dabalo katika Jimbo langu la Chilonwa?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Ukanda huu, *Central Plateau*, Mikoa ya Kati ambayo mvua zake ni za shida shida, lengo letu ni kuhakikisha kwamba, tunajikita kwenye uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga mabwawa. Bwawa la Ikowa ni mojawapo ya Mabwawa ambayo yamekuwa yanafanya kazi vizuri, lakini yanahitaji kukarabatiwa na hasa yanahitaji kuongezewa tuta. Wengi wanadhani suala ni kwenda kuchimbua udongo ulioko mle ndani. Kitaalam, kuondoa udongo katika bwawa lililojaa mara nyingi ni gharama kuliko kutafuta eneo lingine. Kuna uwezekano pia wa kuongeza tuta ili tuweze kulikarabati.

Mheshimiwa Naibu Waziri ametembelea bwawa hili wiki iliyopita nadhani na ameliona. Kwa hiyo, nakuahidi Mheshimiwa Chibulunje kwamba, Wizara yangu itafuatilia mabwawa yote haya, tuangalie uwezekano wa kuyakarabati.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hali ya hewa ya Wilaya ya Kishapu inafanana kabisa katika maeneo mengi ya Kanda ya Ziwa, yakiwemo ya Wilaya ya Kahama; na kwa kuwa tayari eneo la Kata ya Nyandekwa katika Jimbo la Kahama, lilishaanishwa kwamba linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji lakini Serikali bado haijaanza utekelezaji katika hilo:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza hilo ili kuweza kuwasaidia Wananchi katika eneo hilo? Ahsante.

**SPIKA**: Naona mtaenda kwenu kila mtu, lakini Mheshimiwa Waziri hakujiandaa huko; Mheshimiwa Waziri lakini unajua yote, haya!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda nitoe siri tu kwamba, Mheshimiwa Lembeli tumekubaliana kabisa na amenikaribisha Kahama. Sasa labda kwa faida ya watu wake ni kwamba, tutakwenda kutembelea Kahama kuangalia mabwawa na siyo bwawa tu, tunakwenda pia kuangalia tatizo la tumbaku kule Kahama. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lembeli ahadi yangu bado iko pale pale.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, Tanzania kwa mujibu wa *Economist Report* ya mwaka 2011.

**SPIKA:** Usije ukatuhutubia, kwanza haiendi hivyo, endelea! Tunasema usituhutubie!

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni swali tu. Kwa mujibu wa Ripoti ya *Economist* ya mwaka 2011, Tanzania ni nchi ya 11 kwa mito mingi Duniani; na kwa taarifa ya hali ya maji Duniani, Tanzania ina maji yanayofaa kwa umwagiliaji kwa maana ya *fresh water*, zaidi ya asilimia 17 ya maji yote yanayopatikana Duniani. Hata hivyo, Tanzania ina eneo la takribani hekta milioni 29,400,000 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hizi zote ni *potentials* ambazo zinalifanya Taifa hili liwe mzalishaji mkubwa wa kuuza nje. Ni bahati mbaya kwamba mpaka sasa Tanzania inaagiza mchele kutoka nje. Naomba kuiuliza Serikali; inaona aibu kiasi gani kuwa Taifa la uagizaji chakula nje wakati ina fursa zote hizi?

**SPIKA**: Yale yale, Mheshimiwa Waziri majibu! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, akihutubia na mimi inabidi nimhutubie.

**SPIKA:** Mimi nitakuzuia!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Kafulila kwamba, kwanza, naomba nimsaidie kwamba, sisi wenyewe wala siyo taarifa za *economist*, tumefanya utafiti wenyewe; eneo linalofaa kumwagilia katika nchi hii ni hizo 29.3 *million* hekta, hizo ni jumla. Katika hizo, hekta milioni 2.3 zinafaa sana kuliko maeneo mengine. Hekta milioni 4.8 zinafaa kwa kiwango cha kati na zilizobaki 22.3 zinabaki kwa kiwango cha chini. Sasa kinachotusibu hapa siyo suala la kuona aibu, ni kwamba, kujenga miradi ya umwagiliaji kunahitaji fedha, miradi midogo inahitaji kwa wastani kitu kama dola 2000 kwa hekta. mikubwa zaidi inakwenda mpaka 10,000 kwa hekta. Kwa hiyo, suala hilo ndiyo linalotuletea shida.

Tukija kwenye suala la uagizaji wa mchele, sisi hatujaagiza chakula kwa muda mrefu. Mwaka huu ndiyo tumeagiza mahindi Zambia na mchele. Hata hivyo, tumeagiza baada ya kuona hali ya hewa ilikuwa mbaya, tukawa na wasiwasi tusije tukajikuta Wananchi wanapata tabu kwa ajili ya mfumko wa bei. Kwa hiyo, tumefanya hivyo tu kwa ajili ya kujikita kupambana na mfumko wa bei unaoweza kujitokeza. Kwa miaka mitatu, mine, mfululizo, Tanzania ilikuwa haiagizi kabisa chakula.

**SPIKA:** Swali la mwisho, Mheshimiwa Cheyo!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa tuna mabwawa mbalimbali; kwa mfano, Nkoma tuna Bwawa na tuna Ziwa Victoria ambalo linatumika sana Misri na ndugu yangu kule naye anajenga Bwawa la Kasori; ni lini tutapelekewa Wataalam wa kuweza kupima Miradi ya Umwagiliaji kwa kutumia maji ya mabwawa na Ziwa Victoria?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cheyo, kama ifuatavyo:-

Wataalam katika Kanda ya Ziwa; tumegawanya nchi hii katika Kanda za Umwagiliaji, Kanda ya Ziwa inahudumiwa na Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda ya Ziwa, ambayo Makao Makuu yako pale Mwanza na wanaendelea kufanya upembuzi na utafiti kuangalia mabwawa na mito iko wapi, lakini kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya.

Miradi lazima iibuliwe na Halmashauri, lakini nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wataalam hao wataendelea kufanya zoezi hili na hivi sasa wako katika utaratibu wa kuangalia namna bora ya kutumia maji ya Ziwa kwa kutumia nishati mbadala, kwa sababu yale unaweza ukayachukua kwa kutumia *solar energy, wind energy*, halafu ukamwagilia maeneo ambayo yako pembeni mwa Ziwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, hili tunaendelea kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Tuendelee na swali la mwisho.

Na. 355

**Uzalishaji Duni Katika Kilimo**

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH (K.n.y. MHE. RUKIA KASSIM AHMED)** aliuliza:-

Licha ya kuwa na ardhi kubwa na yenye rutuba nchini, wakulima wengi huzalisha magunia manane kwa ekari moja, wakati kihalisia ekari moja huzalisha magunia 80:-

Je, Serikali inafanya maandalizi gani kwa wakulima ili waweze kuzalisha kwa tija na hivyo kuondokana na umaskini uliokithiri?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, leo umepatikana. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, naomba nisahihishe kidogo, kwa faida yake tu kwamba, *figures* zile alizoweka za magunia 80 kwa ekari, mimi pamoja na utaalam wangu, kwa miaka yangu yote, nikipiga hesabu inakuja kwenye uzalishaji wa tani 17 mpaka 20 kwa hekta, sidhani kama ziko mahala popote.

Baada ya kusema hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza wakulima kwa jitihada kubwa wanayofanya, kuzalisha chakula tunachokula katika nchi hii. Ni kweli kwamba, bado kuna haja ya kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo ili kufikia Mapinduzi ya Kijani. Ili kufikia lengo hilo, kazi zinazotekelezwa ni pamoja na kupanua kilimo cha umwagiliaji, kuhamasisha matumizi ya pembejeo bora, kuongeza uzalishaji wa mbegu bora, kuimarisha utafiti na huduma za ugani, ukaguzi wa madawa ya kilimo na mbegu, kutoa mafunzo kwa wakulima, kuhamasisha matumizi ya zana za kilimo na kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mimea.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Serikali wa kutoa pembejeo zenye ruzuku umeanza kuonesha mafanikio mazuri, ambapo uzalishaji wa mazao umeanza kuongezeka. Kwa mfano, uzalishaji wa mahindi kwa miaka mitatu iliyopita umeongezeka kutoka wastani wa tani 1.2 kwa hekta hadi tani 4.5 kwa hekta, wakati mpunga umechupa kutoka wastani wa tani 1.8 kwa hekta hadi zaidi ya tani 4.5 kwa hekta.

Pamoja na mafanikio hayo, Serikali inafanya juhudi

kuhakikisha kwamba, matumizi ya pembejeo hususan mbolea, yanaongezeka kwa sababu takwimu tulizonazo zinaonesha kwamba, matumizi yetu ya mbolea bado yako chini; ni takribani kilo kumi tu kwa hekta, ikilinganishwa na kilo 21 kwa hekta katika nchi ya Malawi, kilo 51 kwa hekta katika nchi ya Afrika Kusini na nchi nyingine kama Holland imefikia mpaka zaidi ya kilo 500 kwa hekta. Jitihada zinazofanywa ni pamoja na kuhamasisha sekta binafsi kuzalisha na kuingiza mbolea nchini pamoja na kuanzisha viwanda vya kuzalisha mbolea.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Wakulima wanalalamika sana kwamba, pembejeo hazifiki kwa wakati na hili ndilo linalofanya kupungua kwa uzalishaji. Je, Serikali iko tayari kutoa kauli sasa kuhakikisha kwamba mbolea zinafika kwa wakati kwa wakulima?

(ii) Kwa mujibu wa takwimu alizotupa ni kwamba Tanzania sasa inatumia kilo kumi kwa hekta na hii inapunguza sana uzalishaji, wakati nchi za wenzetu zimezidi zaidi ya kilo 50 kwa hekta. Mheshimwia Waziri haoni kwamba kufanya hivyo ni kudhoofisha ile dhana nzima ya KILIMO KWANZA?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu suala la pembejeo kutofika kwa wakati, tumekuwa tunajibu hatua tunazozichukua ili kuhakikisha pembejeo zinafika. Moja ya changamoto tulizokuwa tunazipata huko nyuma, ni utaratibu wa Bajeti ya Serikali *(Budget Cycle)*. Tulikuwa tunamaliza msimu au bajeti mwezi wa nane, ndipo fedha zianze kutoka. Kwa hiyo, tatizo la uchapishaji wa vocha, uagizaji wa mbolea,

lilikuwa pia linatuathiri katika mfumo mzima wa mtiririko wa pembejeo. Sasa huu utaratibu wa *budget cycle* tuliouanza, tunamaliza *June, come July,* tunaamini kwamba, sasa tutakuwa tunapata fedha mapema; na imani yangu ni kwamba, kutakuwa na mabadiliko katika ufikishwaji wa pembejeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi madogo ya virutubisho, kilo kumi kwa hekta; ni kweli nimeziweka hizi *figures* makusudi kwa sababu huko nyuma tulikuwa tunatumia kilo nane tu. Sasa baada ya kuweka taratibu hizi za ruzuku ndiyo tumepanda mpaka kumi na ndiyo maana tumeweka utaratibu huu sasa wa kwamba, tuhakikishe tunazalisha mbolea kwa wingi, tutumie rasilimali zetu, *Minjingu Rock Phosphate*, Gesi iliyopo, viwanda vihamasishwe vijengwe, tupate mbolea nyingi ili tuwafikie hao wenzetu na kwa kweli wamefikia kwenye *green revolution* kwa matumizi makubwa ya mbolea. Kwa hiyo, lengo siyo kudhoofisha, lengo ni kwenda huko ambako wenzetu wamefika.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilitangaza kuwa msimu huu itabadilisha mfumo wa kutoa pembejeo na baadaye wakasema kwamba, haitabadilisha mfumo utabaki uleule wa mwaka jana; na kwa kuwa Wananchi wameanza kulalamika, hawaelewi sasa ni mfumo gani utatumika kwa mwaka huu wa kilimo, yaani wa 2013/14; je, ni kupitia mawakala ama kupitia vikundi:-

Sasa Serikali inatoa tamko gani kwa wakulima ili waweze kujiandaa vizuri kama ni kwa vikundi wajiweke kwenye vikundi, kama ni kwa mawakala wawatafute mawakala ambao ni waaminifu ili tusijichanganye msimu wa kilimo utakapofika? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Tarehe 28 na 29, tulikuwa na Semina hapa Dodoma, ambayo ilikuwa inajadili mfumo wa usambazaji wa ruzuku ya pembejeo, walihudhuria Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Tulichokubaliana ni kwamba, tukisema mfumo wa kutumia vikundi ndiyo tu utumike, bado kuna wengine wataathirika, kwa sababu kuna mahali pengine vikundi hivyo havipo. Kuna mahali pengine ukisema vikundi, ndiyo vinaibuka siku hiyo hiyo na mfumo wa vikundi pia unahitaji mabenki nayo yavitambue, mabenki yanataka vikundi vyenye taratibu vinavyoweza kulipa vyenye *bank statements.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichokubaliana kwa kifupi ni kwamba, mifumo yote itatumika, yale maeneo ambayo utaratibu wa vocha uligubikwa na changamoto nyingi za wizi na nini, hao tutawaangalia kivyao. Wale ambao walifanya vizuri zaidi nao tutawaangalia kivyao.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi tu ni kwamba, wiki hii tutatoa maelezo kwamba, ni Mikoa ipi itatumia utaratibu wa vocha, kulingana na mfumo uliotumika mwaka jana. Pia tuna sababu ya kurejea utaratibu wa vocha kwa sababu tunazo fedha za *World Bank*, takribani shilingi bilioni 19, fedha hizi zinatakiwa zitumike kwa utaratibu wa vocha maana ndiyo masharti yao. Kwa hiyo, kwa maeneo ambayo yalifanya vizuri, tutatumia utaratibu wa vocha.

Wale ambao vikundi vipo imara, kama kule kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, ninaamini tutakwenda na utaratibu wa mikopo kwa vikundi. Kwa hiyo, mifumo yote itakwenda sambamba. *(Makofi)*

**MHE. DUNSTAN L. KTANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa furasa hii. Kwa kuwa matumizi bora ya rasilimali ardhi ni msingi muhimu katika mapinduzi ya kilimo; na kwa kuwa Sekta ya Ufugaji wa Samaki imeonekana ndiyo sekta inayokua zaidi kuliko sekta yoyote ya uzalishaji wa chakula. Je, Wizara ya Kilimo ipo tayari sasa kutoa agizo kwamba pale tutakapoanzisha skimu yoyote ya umwagiliaji iende sambamba na ufugaji wa samaki? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, swali zuri hilo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali zuri sana hilo kwamba, kwa kweli hiyo sasa ndiyo *integrated development* katika kilimo na wala siyo jambo geni. Mahala pengine ukienda Mikoa kama ya Kilimanjaro ambako nimefanya kazi sana, tulikwishaanza kufanya utaratibu huo, ambapo Miradi yote ya Umwagiliaji, inawekewa pia mabwawa ya samaki pembeni na siyo samaki tu, samaki na juu wanaweka chanja za kufugia mifugo mingine kama bata. Kwa hiyo, inawiana; bata wanatoa kinyesi kinasaidia samaki wanakula, maji ya umwagiliaji yanakwenda kwenye samaki, kwa hiyo, inakuwa mlishano.

Mimi nakubaliana naye, ni suala ambalo tunatakiwa kulifanyia kazi kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Halmashauri za Wilaya, tunapoibua Miradi yote hii; na kwa njia nyingine itatupunguzia gharama kwamba kila mradi utenge fedha zake, maana mvuvi atenge fedha za uvuvi, kumbe maji ya umwagiliaji yako hapo hapo. Mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, hili ni wazo zuri sana.

**SPIKA:** Mheshimwa Leticia Nyerere, swali la mwisho.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ukosefu wa chakula nchini husababishwa ama kwa sababu ya ukosefu wa mvua, yaani ukame au kwa sababu ya ongezeko kubwa la mvua za kupindukia kama iliovyotokea kule Wilayani kwetu Kwimba. Je, Serikali inatoa elimu kwa kiwango gani kuhusu tabia nchi, yaani *climate change* ili tuweze kuepukana na njaa za mara kwa mara nchini?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Nyerere, kama ifuatavyo:-

Elimu kwa wakulima kuhusu tabia nchi ni sehemu mojawapo ambayo tumeijenga katika Miradi yetu. Sasa hivi kila Mradi unaoanzishwa, una kipengele cha mambo ya mazingira na hilo ni suala mojawapo na hakuna hata mradi mkubwa sasa hivi unaoweza ukauanzisha bila kwanza kupitia masuala mtambuka haya ya mazingira. Kwa sababu hiyo, ndani ya Serikali, katika Ofisi ya Makamu wa Rais, chini ya Mheshimiwa Huvisa, kipo Kitengo Maalum cha Masuala ya Mazingira na mojawapo ni kutoa elimu ya masuala kama hayo. Ndani ya Wizara yangu pia kuna Kitengo cha Mazingira, kwa hiyo, labda tu tuseme tuache suala hili liendelee kupata hamasa kubwa ili Wananchi wapate uelewa huu.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimimiwa uhuru mlionao huu siyo wa kawaida, kwa hiyo, kinachotakiwa ni kuuliza maswali mafupi na wanaojibu wajibu kwa kifupi, kusudi tuwe na wachangiaji wengi, lakini hatuwezi kuendelea tu. *(Makofi)*

Nina matangazo mawili tu. Kwanza kabisa, Katibu wa Wabuge wa CHADEMA, Mheshimiwa David Ernest Silinde, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kuwa, leo baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba, watakuwa na kikao chao katika Ofisi ya Kiongozi wa Upinzani. Hii ni baada ya kuahirisha kikao humu ndani, saa saba.

Ofisi pia inawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwenye Viwanja vya Maonesho vya Bunge, kuna Maonesho ya Meza za Maabara ya Shule, yaani *Science Kit and Mobile Laboratory Science Table,* yanaoneshwa na Kampuni ya *Worldwide Education Care.* Maonesho haya yataanza leo tarehe sita na hivyo Wabunge wapite na kuona ili wapate fursa ya kuzisaidia shule zao kwa kupata ushauri juu ya matumizi ya vifaa hivyo muhimu. Mpite tu mkaangalie hayo mambo ya kisayansi yako pale.

Baada ya kusema hayo, Waheshimwia Wabunge, tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014
### Wizara ya Fedha

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea, nina tangazo; wengine wanaleta vikaratasi bila kuchapwa ndiyo maana Spika anasahau. Nimeombwa na Katibu wa Wabunge wa CCM kwamba, niwatangazie Waheshimwa Wabunge wa CCM leo saa saba mchana kutafanyika Kikao cha Chama katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa mtoa hoja!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwako pamoja na Naibu Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mbunge wa Kongwa), Waheshimiwa Wenyeviti; Jenista Joakim Mhagama (Mbunge wa Peramiho), Mussa Azzan Zungu (Mbunge wa Ilala) na Muhammed Seif Khatib (Mbunge wa Uzini), kwa kuongoza vyema majadiliano ya Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuishukuru kwa namna ya pekee, Kamati ya Kudumu ya Uchumi, Viwanda na Biashara chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa (Mbunge wa Mufindi Kaskazini) na Makamu wake, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula (Mbunge wa Mkinga), kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyoyatoa kwa Wizara wakati wa kuchambua mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Fedha. Aidha, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa

Kamati ya Kudumu ya Bajeti, Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Mashariki, pamoja na Kamati nzima kwa ushauri wao makini. Katika uandaaji wa Hotuba hii, Wizara imezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati hizo pamoja na ushauri na maoni ya hoja mbalimbali zilizotolewa wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuwashukuru Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (Mb) na Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene (Mb). Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wakuu wa Idara na Vitengo, Wafanyakazi wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Ramadhan M. Khijjah na Naibu Makatibu Wakuu; Dkt. Servacius B. Likwelile, Ndugu Elizabeth J. Nyambibo na aliyekuwa Katibu Mkuu Msaidizi, Ndugu Laston T. Msongole aliyestaafu hivi karibuni, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, napenda kuwashukuru Profesa Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Ndugu Harry Kitilya, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Dkt. Albina Chuwa, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na Wakuu wa Taasisi na Wakala wa Serikali chini ya Wizara kwa michango yao katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na malengo ya mwaka 2013/2014. Uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Mpango na Bajeti ya Wizara, unazingatia mambo yafuatayo: Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II); Vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa mwaka 2011/2012 - 2015/2016; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010; Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA); Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2013/2014 - 2015/2016; pamoja na

Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma - *Public Finance Management Reform Programme (PFMRP).*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara iliandaa mpango unaolenga kutekeleza yafuatayo: Kuongeza mapato ya ndani kufikia uwiano wa Pato la Taifa wa asilimia 18 kwa mwaka 2012/2013 ikilinganishwa na asilimia 16.9 kwa mwaka 2011/2012; kufanya mapitio ya Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania *(MPAMITA);* kuandaa Mwongozo wa Mpango na Bajeti; kufuatilia matumizi ya fedha za Serikali; kufanya uchambuzi wa mawasilisho ya Bajeti za Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi, Wakala, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kutoa Kitabu cha Bajeti Toleo la Wananchi - *Citizen's Budget;* kujenga uwezo wa uandaaji na usimamizi wa Bajeti ya Muda wa Kati pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati; kusimamia na kuimarisha uendeshaji na uunganishaji wa Mfumo wa Malipo wa Serikali - *Intergrated Financial Management System (IFMS);* kuimarisha usimamizi na utoaji wa taarifa mbalimbali za fedha; kuendelea na ukaguzi wa miradi ya maendeleo na kutoa ushauri wa kitaalam kwa watekelezaji wa miradi hiyo; na kuhakikisha sheria za ununuzi wa umma na fedha za umma zinazingatiwa katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Wizara pia ilipanga kuratibu utekelezaji wa MKUKUTA Awamu ya Pili; kuimarisha utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi - *Public Private Partinership (PPP)* ili kupanua fursa za kuchangia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; kuendelea kusimamia utendaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali; kuendeleza kada za Uhasibu, Ukaguzi wa Ndani, Ugavi, Uchumi, Uhakiki Mali, Watakwimu, Usimamizi wa Fedha na Wataalamu wa TEHAMA; kuendelea kuhuisha Daftari la Mali ya Serikali; kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha; na kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi chini ya Mpango wa *Millenium Challenge Account Tanzania (MCA-T)*. Pamoja na hayo, Wizara pia ilipanga kutathmini mzunguko wa Bajeti *(Budget Cycl*e) na kuwasilisha Serikalini mapendekezo yake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012, Pato la Taifa liliendelea kuimarika na kufikia ukuaji wa asilimia 6.9 ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2011, ikiwa ni zaidi ya lengo la asilimia 6.8 mwaka 2012. Sekta ya Fedha ambayo inasimamiwa na Wizara ya Fedha ilichangia katika shughuli za kiuchumi na kukuza Pato la Taifa. Katika mwaka 2012, Sekta hii ya Fedha ilichangia asilimia 1.8 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na asilimia 1.7 ya mwaka 2011. Ongezeko hili la ukuaji lilitokana na utekelezaji madhubuti wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho cha mapitio, Wizara pia ilitekeleza Sera ya Fedha na bajeti kwa lengo la kupunguza ukwasi na mfumuko wa bei ambapo Benki Kuu ya Tanzania iliongeza mauzo ya fedha za kigeni katika Soko la Fedha kama njia mojawapo ya kudhibiti mfumuko wa bei. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania ilipandisha kiwango cha chini cha akiba ya amana za Serikali katika mabenki kutoka asilimia 30 hadi asilimia 40 pamoja na kupunguza kiwango cha kuhodhi fedha za kigeni kulingana na mitaji yao kwa mabenki kutoka asilimia 10 hadi asilimia 7.5 kuanzia Desemba, 2012. Hatua hizo zilisaidia kupunguza kiwango cha mfumuko wa bei kutoka asilimia 18.7 mwezi Aprili, 2012 hadi asilimia 9.4 mwezi Aprili, 2013 pamoja na kusaidia kuimarika kwa kiwango cha ubadilishaji wa shilingi dhidi ya Dola ya Kimarekani. Aidha, katika kuimarisha usimamizi na maendeleo ya Sekta ya Fedha, Wizara imerekebisha muundo wake *(Organisational Structure),* kwa kuanzisha Idara ya Maendeleo ya Sekta ya Fedha – *Financial Sector Development Division* ambayo itasimamia Sera za Sekta ya Fedha na taasisi ndogo za fedha kama *SACCOS* na *VICCOBA*.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Wizara imeratibu maboresho ya uandaaji wa bajeti ya 2013/2014 kwa kuzingatia mzunguko mpya wa bajeti *(New Budget Cycle).* Aidha, Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, uliandaliwa kwa kushirikisha wadau

mbalimbali na kusambazwa kwa wakati. Vilevile, Wizara imeandaa na kusambaza nyaraka muhimu za bajeti ambazo ni pamoja na Vitabu vya Bajeti ya Serikali *(Volume I, II, III* na *IV* kwa mwaka 2012/2013) kama vilivyopitishwa na Bunge lako Tukufu na kitabu kinachotoa maelezo ya Bajeti ya Serikali katika kipindi cha muda wa kati kwa mwaka 2012/2013 - 2014/2015. Kitabu hiki kinasaidia kuwajulisha Wananchi na wadau wengine kuhusu matokeo ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita pamoja na mwelekeo wa bajeti ijayo kwa kipindi cha muda wa kati. Kadhalika, katika kuboresha uelewa wa Bajeti ya Serikali kwa Wananchi, Kitabu cha Bajeti Toleo la Wananchi kwa mwaka 2012/2013 kimeandaliwa na kusambazwa kwa wakati na kuwekwa kwenye tovuti ya Wizara. Kitabu hiki kimesaidia kueleza bajeti kwa Wananchi wa kawaida kwa lugha rahisi na hivyo kuongeza uwazi katika kutoa taarifa muhimu za kibajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kujenga uwezo wa kuandaa mipango na bajeti kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara ilitekeleza mambo yafuatayo: Kufanya tathmini ya mchakato wa bajeti ya 2012/2013 kuhusu namna bajeti ilivyoandaliwa, changamoto zinazojitokeza na jinsi ya kuzitatua; kuwajengea uwezo Maofisa wa Bajeti wa Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu kuandaa bajeti ya 2013/2014, maboresho yaliyofanywa kwenye Mfumo wa Kugawa Fedha za Bajeti - *Strategic Budget Allocation System* (*SBAS*) na kuandaa bajeti inayozingatia utendaji - *Performance Based Budgeting;* na kuhuisha Mwongozo wa kuandaa mipango na bajeti, ambao umezingatia mzunguko mpya wa bajeti. Wizara imeendelea kuandaa na kusimamia malipo ya mishahara ya kila mwezi kwa ajili ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kuendelea kusimamia na kufuatilia uandaaji na utekelezaji

wa Bajeti ya Serikali; kupitia mifumo na taratibu zinazotumika katika uandaaji wa mpango na bajeti pamoja na ufuatiliaji wa utendaji ili kuongeza ufanisi katika uandaaji na utekelezaji wa bajeti; na kuziwezesha Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa mipango na bajeti zake zinazoendana na miongozo ya mipango na bajeti ya taifa. Aidha, Wizara itaanza kutekeleza mkakati wa kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali kutoa taarifa za kila mwezi za malipo ya mishahara kwa Watumishi wa Serikali katika vituo vyao vya kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha usimamizi wa misaada na mikopo ili kupata matokeo tarajiwa. Mafunzo ya mfumo wa kutunza takwimu na kumbukumbu zingine za misaada na mikopo yalitolewa kwa Maafisa kutoka Wizara 21 na Washirika wa Maendeleo wapatao 20. Aidha, mapitio ya utekelezaji wa Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania *(MPAMITA)*, 2006 – 2011 wenye lengo la kuimarisha usimamizi wa misaada, yalifanyika.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa mikataba mbalimbali ya misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na mikopo ya kibiashara kutoka katika mabenki kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa vinu viwili vya kusafisha gesi asilia Mtwara na Songosongo; ujenzi wa bomba kubwa la gesi kutoka Mtwara kupitia Somanga - Fungu mpaka Dar es Salaam; upembuzi yakinifu kwa ajili ya ukarabati wa Reli ya Tanzania Zambia (*TAZARA*); na fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha usimamizi wa misaada na mikopo ya kibajeti, Wizara iliandaa mkutano wa Mwaka wa Mapitio ya Misaada na Mikopo ya Kibajeti - *General Budget Support Annual Review* uliofanyika mwezi Novemba, 2012. Matokeo yaliyotokana na Mkutano huo ni Washirika wa Maendeleo kuipatia Serikali misaada ya kibajeti yenye thamani ya shilingi bilioni 1,163.13, fedha ambayo imepangwa kutumika katika bajeti ya 2013/2014.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo *(Development Partners),* imeimarisha Mfumo wa Mapitio ya Matumizi ya Umma - *Public Expenditure Review (PER)* kwa kuanzisha sekretarieti ya pamoja yenye wajumbe wa upande wa Serikali na upande wa Washirika wa Maendeleo pamoja na kuandaa Mpango Kazi wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/ 2014, Wizara inatarajia kukamilisha Mfumo mpya wa Ushirikiano wa Kimaendeleo - *Development Cooperation Framework* kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Mfumo huu ndiyo utakaoongoza usimamizi wa Misaada na Mikopo ya Kibajeti katika kutekeleza mipango na programu za kitaifa za kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maendeleo. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya Mfumo wa Kutunza Kumbukumbu za Misaada na Mikopo *(Aid Management Platform)* kwa Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na Asasi za Kiraia. Vilevile, Wizara itaendelea na utaratibu wa kuandaa mkutano wa Mapitio ya mwaka ya Misaada na Mikopo ya Kibajeti pamoja na Mapitio ya Matumizi ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa linajumuisha mikopo ya nje na mikopo ya ndani. Wizara iliendelea kusimamia ulipaji wa deni la Taifa ambapo katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Aprili, 2013 malipo yalifikia shilingi bilioni 1,666.77. Kati ya hayo malipo ya deni la nje ni shilingi bilioni 213.57 na malipo ya deni la ndani ni shilingi bilioni 1,453.20. Aidha, katika kuboresha usimamizi wa Deni la Taifa, Wizara inakamilisha uanzishwaji wa Idara ya Usimamizi wa Madeni ambayo itaanza kazi mwaka ujao wa fedha, pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kujenga uwezo wa kufanya upembuzi yakinifu na kuhakikisha kuwa uwezo wa usimamizi madhubuti wa Deni la Taifa unajengwa na kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ilitekeleza yafuatayo: Kuboresha Mfumo wa Malipo Serikalini – *Integrated Financial Management System (IFMS)* kutoka mfumo wa toleo la *EPICOR 7.3.5*

kwenda toleo la *EPICOR 9.05* kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa fedha za umma; kukamilisha zoezi la kutoa mafunzo ya kufanya malipo moja kwa moja benki kwa njia ya kielektroniki - *Tanzania Inter-Bank Settlement System (TISS)* kwa Watumishi wa Hazina ndogo zote, Bunge, Mikoa, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Idara ya Ushirika, ikiwa ni maandalizi ya kuunganisha Taasisi hizo kwenye mtandao wa *TISS* ili kuboresha usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Wahasibu 200 kutoka mikoa 25 walipata mafunzo juu ya usimamizi wa fedha za umma; Wahasibu 425 kutoka Wizara mbalimbali na Sekretarieti za Mikoa walipata mafunzo juu ya Viwango vya Kimataifa vya kihasibu vya kuandaa Hesabu za Serikali – *International Public Sector Accounting Standards (IPSAS)* na watumishi 120 kutoka katika Wizara na Taasisi walipata mafunzo ya kusimamia Mabadiliko na Kuandaa Mipango Mkakati - *Change Management and Strategic Planning* kwa lengo la kujenga uwezo wa Idara za Bajeti na Mipango katika kutekeleza maboresho ya usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha usimamizi wa fedha za umma kwa kuendelea kutekeleza Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma – *Public Finance Management Reform Programme (PFMRP),* ambapo Awamu ya Nne ya Programu ilianza kutekelezwa Julai, 2012 na itakamilika Juni, 2017. Programu ya *PFMRP* pamoja na mambo mengine, imewezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanza kutumia akaunti sita za benki badala ya akaunti nyingi zilizokuwepo kwa lengo la kuendelea kuboresha usimamizi wa fedha za Umma. Aidha, Programu ilitoa fedha za kuwezesha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuandaa Mpango Mkakati wake wa Programu ya Usimamizi wa Fedha za Umma. Vilevile, matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa programu yalifanywa kama sehemu ya mapitio ya mwaka ya Misaada na Mikopo ya Kibajeti yaliyofanyika mwezi Novemba, 2012 yalionesha kuwa utekelezaji wa Programu ulikuwa wa kuridhisha na

ulizingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma katika kufanya ununuzi ulifikia asilimia 74.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza mpango kazi wa miaka mitano wa kuiwezesha Serikali Kuu kuandaa hesabu kwa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu – *International Public Sector Accounting Standards* (*IPSAS*) *accrual basis*. Kwa mara ya kwanza, hesabu za Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2013 zitaandaliwa kwa kutumia viwango hivyo vya Kimataifa. Aidha, Wizara imeandaa miongozo mbalimbali na kufanya mikutano elekezi ili kuwajengea uwezo na uelewa wahasibu na wadau mbalimbali. Katika kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali pamoja na utoaji wa taarifa zenye ubora na uwazi, Wizara imeendelea kusimamia na kuimarisha mtandao wa malipo ya Serikali katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Hazina Ndogo pamoja na Vikosi vya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti na kusimamia mapato na matumizi, Wizara ilitoa mafunzo ya matumizi bora ya mashine za kutolea *VISA* kwa Wahasibu waambata wa Balozi zetu zote 32. Aidha, mashine hizo zilifanyiwa matengenezo na mashine nyingine mpya ziliwekwa. Vilevile, watumishi 263 wa kada za Uhasibu, Ukaguzi wa Ndani, TEHAMA na Ugavi kutoka Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa walipata udhamini katika mafunzo ya shahada na stashahada katika vyuo mbalimbali vya hapa nchini ili kuendelea kujenga uwezo wao katika eneo la usimamizi wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara itaendelea kusimamia, kuimarisha na kudhibiti mapato na matumizi ya fedha za Serikali kwa kuboresha mtandao wa malipo wa Serikali. Aidha, Wizara itatoa ushauri wa kitaalamu na kuunganisha Hazina Ndogo na Sekretarieti za Mikoa ili kuziwezesha kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki kupitia Benki Kuu ya Tanzania *(TISS)*. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi

na mrefu kwa wahasibu wa Wizara, Mikoa na Idara za Serikali ya kuandaa hesabu katika viwango vya kimataifa – *IPSAS Accrual Basis* na kuongeza uelewa wa matumizi ya mtandao wa *EPICOR 9.05.*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Awamu ya Nne ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa kufanya yafuatayo: Kuandaa mkakati wa utekelezaji wa kubadilisha mfumo wa *IPSAS Cash* kwenda *IPSAS Accrual*; kuufanyia marekebisho mwongozo wa uandaaji wa Mipango na Bajeti za muda wa Kati; kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapa mafunzo katika kada za fedha, ununuzi, ukaguzi wa ndani na usimamizi wa mali ya Serikali katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia fedha na mali ya umma; kufanya mapitio ya mifumo ya fedha za Serikali kwa ajili ya kuhuisha na kuwianisha; kuandaa Mkakati wa Kudhibiti Uanzishwaji wa Mifumo ya Fedha inayojitegemea; kuandaa Sera ya Usimamizi wa Madeni; na kuandaa Mpango wa Mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma kwenye maeneo ya uandaaji wa mipango, utekelezaji pamoja na kumudu mabadiliko yanayojitokeza katika Usimamizi wa Fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Nne, itaendelea kusambaza mfumo wa kompyuta wa ukaguzi wa ndani kwa Wizara na Idara zinazojitegemea 15 pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa 15. Aidha, mkakati wa utekelezaji wa mapendekezo ya utafiti juu ya vyanzo vya mapato kwa ajili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa utaandaliwa pamoja na kuhuisha mfumo wa ugawaji wa fedha kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, Mpango Mkakati wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa upande wa Zanzibar utaandaliwa na kusambazwa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Sera ya Ununuzi

wa Umma, Wizara imetekeleza yafuatayo: Kukamilisha Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma; kukamilisha rasimu ya Kanuni za Ununuzi wa Umma; kuendelea kuhuisha taarifa za Maofisa Ununuzi na Ugavi katika daftari ambapo jumla ya Maofisa 989 wameingizwa katika daftari hilo. Aidha, Wizara imeendelea na taratibu za kuanzisha kada ya Ununuzi Serikalini pamoja na kusimamia na kuendeleza kada ya Ugavi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara imepanga kufanya yafuatayo: Kuanza utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma; kufuatilia na kufanya tathmini ya mfumo wa Ununuzi wa Umma; na kuendelea kuhakiki Daftari la Taifa la Taarifa za Maafisa Ununuzi na Ugavi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya kudhibiti shughuli za ununuzi nchini, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma - *PPRA* ilifanya yafuatayo: Kaguzi za ununuzi katika miradi 137 ya ujenzi inayotekelezwa na Halmashauri mbalimbali za Wilaya; kaguzi za ununuzi katika Taasisi za Umma 121; chunguzi sita za ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi zimefanyika na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa zimependekezwa; kuchapisha jarida la *Tanzania Procurement Journal* ili kutoa matangazo ya zabuni na taarifa nyingine zinazohusu ununuzi wa umma; na kusambaza Mfumo wa Upokeaji na Usimamizi wa Taarifa za Ununuzi nchini - *Procurement Management Information System (PMIS)* kwa Taasisi 299 na kutoa mafunzo juu ya mfumo huo. Aidha, *PPRA* ilitoa mafunzo ya ununuzi wa umma kwa watumishi 735 kutoka Taasisi za Umma 41. Vilevile, *PPRA* iliandaa Mkutano wa *Commonwealth Public Procurement Network (CPPN*), uliofanyika Dar es Salaam mwezi Oktoba, 2012 na washiriki wapatao 111 kutoka nchi mbalimbali Duniani walihudhuria ili kubadilishana uzoefu katika fani ya ununuzi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, *PPRA* imejiandaa kufanya ukaguzi katika Taasisi za Umma 115 pamoja na miradi ya ujenzi 200 kwa ununuzi

uliofanywa na taasisi hizo. Aidha, Ofisi za Kanda Dodoma na Mbeya zinatarajiwa kufunguliwa ili kusogeza karibu zaidi shughuli zake kwa Halmashauri na Manispaa na kuandaa Mpango Kazi wa utekelezaji wa kuanzisha Mfumo wa Ununuzi kwa njia ya Mtandao wa kielektroniki - *e-procurement system,* ambao pamoja na mambo mengine, unatarajia kupunguza upungufu wa ufanisi wa ununuzi unaotokana na kuweka taarifa kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni – *PPAA* imeendelea kushughulikia rufaa za zabuni za umma. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Aprili, 2013, Mamlaka ilipokea jumla ya mashauri 24 ambapo mashauri 21 yalifanyiwa mapitio na maamuzi kutolewa. Katika mapitio hayo, mashauri 15 walalamikaji walishinda na Taasisi za Ununuzi kuagizwa kufanya marekebisho kwa kuzingatia sheria. Mashauri mawili yalikataliwa baada ya kuletwa nje ya muda uliowekwa kisheria na pia Mamlaka kutokuwa na uwezo wa kuyajadili - *lack of powers of jurisdiction*. Aidha, mashauri matatu walalamikaji walishindwa na shauri moja lilifutwa na mlalamikaji mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Mamlaka itaendelea kusikiliza na kutolea maamuzi migogoro katika Ununuzi wa Umma na kuelimisha umma na wadau juu ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini – *Goverment Procurement Services Agency (GPSA)* imetekeleza yafuatayo: Ofisi za kutoa huduma ya uuzaji wa mafuta na vifaa kwenye Mikoa mipya ya Njombe, Katavi, Geita na Simiyu zimefunguliwa na zimeanza kufanya kazi; Mafunzo kuhusu mfumo wa vifaa na huduma mtambuka yalifanyika kwenye vituo vinane ambavyo ni Arusha, Morogoro, Mbeya, Dodoma, Dar es Salaam, Tanga, Kigoma na Mtwara ambapo jumla ya washiriki 498 walihudhuria ili kuwajengea uwezo wa huduma ya ununuzi Serikalini; na kuandaa utaratibu wa kununua kwa pamoja vifaa na

huduma mtambuka kwa kutangaza zabuni 31 ambapo waombaji 9,256 wamejitokeza. Aidha, ukarabati wa ofisi katika Mikoa ya Lindi, Tabora na Shinyanga umekamilika na ukarabati wa ofisi katika Mkoa wa Mtwara na ujenzi wa ofisi, ghala na kisima cha mafuta katika Mkoa wa Manyara unaendelea kwa lengo la kuimarisha huduma za ununuzi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara kupitia *GPSA* imepanga kutekeleza yafuatayo: Kukamilisha ujenzi wa ofisi, ghala na kisima cha mafuta katika Mkoa wa Manyara; kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa ghala na kisima cha mafuta katika Mikoa ya Njombe, Katavi, Geita na Simiyu; kufanya ukarabati wa majengo ya ofisi za Mikoa ya Dodoma, Manyara, Dar es Salaam, Mtwara, Kagera na Morogoro; kuongeza wigo wa vifaa *(stock range)* kutoka 86 iliyopo sasa hadi kufikia 100; na kuanza kutekeleza mkakati wa kununua vifaa vya kuuza kutoka kwa watengenezaji na mawakala wakubwa.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa magari ni moja ya eneo ambalo linatumia fedha nyingi za Umma na kutokana na hilo, Serikali imeona kuwa kuna umuhimu wa kuweka utaratibu bora utakaowezesha kupata thamani ya fedha katika ununuzi pamoja na matumizi ya magari yake. Ununuzi wa magari kwa sasa umekuwa ukifanywa na kila Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za Serikali, Halmashauri na Ofisi za Mikoa kwa kila moja kuandaa mchakato wa ununuzi wake. Utaratibu huu umesababisha kuwepo kwa ununuzi wa aina nyingi za magari na kwa bei zinazotofautiana baina ya Taasisi moja na nyingine. Wizara imeandaa rasimu ya utaratibu wa mfumo wa ununuzi wa magari kwa pamoja ambapo *GPSA* itahusika na jukumu hili. Utaratibu huu utaanza kutumika mara baada ya kupitishwa na Mamlaka zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara imeanza kuandaa Sera ya Taifa ya Mali ya Serikali. Wizara pia iliendelea kuhakiki Mali ya Serikali

iliyopo katika Wizara, Idara zinazojitegemea na kutoa ushauri wa kuhakikisha kuwa mali ya Serikali inatunzwa na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Wizara iliendelea na zoezi la kuondosha mali chakavu katika Wizara na Idara za Serikali, ambapo jumla ya shilingi milioni 401.14 zilipatikana kutokana na mauzo ya magari 98, mitambo 57 na vifaa vingine chakavu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara itaendelea na zoezi la kuthamini mali; kuhakiki na kuhuisha Daftari la Mali ya Serikali kwa ajili ya kufanya usuluhishi kwa njia ya mtandao, kufuta na kuondosha vifaa chakavu zikiwemo samani, magari, mitambo na madawa yaliyokwisha muda wake na vifaa vingine katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Wizara itaendelea na hatua mbalimbali zinazohusika katika kukamilisha Sera ya Taifa ya Mali za Serikali ili kuweza kuwa na usimamizi bora wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mpango wa *Millenium Challenge Account – Tanzania (MCA-T),* imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la *Millennium Challenge Corporation (MCC).* Utekelezaji wa miradi inayohusika umeendelea vizuri licha ya changamoto ambazo zimeathiri kasi ya utekelezaji kama vile mvua nyingi kwa Mikoa ya Ruvuma na Rukwa na matatizo ya kiufundi. Ujenzi wa Barabara ya Tanga - Horohoro ulikamilika kwa kiwango cha lami na kukabidhiwa kwa Serikali mwezi Oktoba, 2012; ujenzi wa barabara za Ukanda wa Mtwara, yaani Songea – Namtumbo na Peramiho – Mbinga na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kisiwa cha Mafia nao unaendelea vizuri. Aidha, kazi ya kuweka lami katika barabara tano za Pemba Kaskazini imeanza na ujenzi wa Barabara ya Tunduma – Sumbawanga ambao umegawanywa katika sehemu tatu; Tunduma – Ikana, Ikana – Laela na Laela – Sumbawanga unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya kupeleka umeme

Zanzibar kupitia chini ya bahari na ule wa ukarabati wa mtandao wa umeme kwa Mkoa wa Dodoma sasa umekamilika kupitia akaunti hii ya *Millenium Challenge.* Utekelezaji wa miradi mingine ya ukarabati wa vituo vya kupoozea umeme, ukarabati wa mtandao wa umeme kwa Mikoa ya Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Mwanza na Kigoma, ikiwa ni pamoja na Mradi wa Umeme wa Juakali pale Kigoma, inaendelea. Aidha, miradi ya upanuzi wa mtambo wa maji Ruvu chini na ukarabati wa mfumo wa maji kwa Manispaa ya Morogoro nayo pia inaendelea kwa kutumia Mfuko huu wa Msaada kutoka Marekani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji wa kuridhisha wa miradi, katika kikao cha Bodi ya MCC kilichofanyika mwezi Desemba, 2012, kiliamua kuikubalia Tanzania kuidhinisha maandalizi ya Mpango wa Pili wa Miradi ya *MCC (MCC Compact II).* Serikali imeshaanza maandalizi hayo baada ya kuunda Sekretarieti ya uratibu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara imeandaa na kutoa miongozo ya usimamizi wa vihatarishi katika Sekta ya Umma pamoja na Mwongozo wa Uhakiki wa Ubora wa Ukaguzi wa Ndani. Miongozo hii ilizinduliwa mwezi Machi, 2013. Aidha, Wizara imetayarisha Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ndani na unategemea kuanza kutumika rasmi mwezi Julai, 2013. Kadhalika, Wizara imekamilisha Mkataba wa Makubaliano kati ya Wakaguzi wa Ndani na Wateja wake na pia kutoa kanuni za maadili ya wakaguzi wa ndani. Miongozo hiyo ina lengo la kuboresha utendaji kazi wa ukaguzi wa ndani.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imefanya kaguzi na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wahusika katika miradi sita ya ujenzi. Miradi hiyo ni skimu za kilimo cha umwagiliaji Morogoro; Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma; Hospitali ya Mkoa wa Dodoma; Barabara ya Tunduma - Sumbawanga; Barabara ya Gairo – Dodoma – Kintinku; na Barabara ya Morogoro – Gairo. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu ukaguzi wa ndani kwa kufuata viwango vya kimataifa vya

ukaguzi wa ndani kwa wakaguzi wa ndani 364 wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, mafunzo yanayohusu mfumo wa malipo wa *EPICOR* yametolewa kwa wakaguzi wa ndani 80 kutoka Wizara tisa na Wakala wa Serikali moja.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kusimamia na kuimarisha ukaguzi wa ndani katika Mwaka wa Fedha wa 2013/20 14 Wizara itatoa miongozo ya ukaguzi wa ununuzi; ukaguzi wa mfumo wa malipo ya mishahara; ukaguzi wa bajeti; udhibiti wa ndani pamoja na ukaguzi wa kiufundi kwa wakaguzi wa ndani wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa Wakaguzi wa ndani na Wajumbe wa Kamati za Ukaguzi kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu matumizi na uzingatiaji wa nyaraka za ukaguzi na miongozo iliyotolewa. Vilevile, Wizara itafanya mikutano elekezi kwa wakaguzi wa ndani wa Wizara, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kujadili kwa pamoja changamoto na kuweka mikakati ya kuboresha ukaguzi wa ndani Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kujenga uwezo kwa Maafisa Masuuli na timu zao za menejimenti juu ya sheria, kanuni na taratibu za fedha na ununuzi kwa lengo la kuwawezesha kufanya kazi zao vizuri na hivyo kufanikisha kupata Hati Safi za Ukaguzi. Aidha, mafunzo haya yataboresha uandaaji wa vitabu vya hesabu ambavyo ndiyo msingi wa ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili viandaliwe kwa mujibu wa viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliendelea kutekeleza yafuatayo: Kufanya ukaguzi wa hesabu za mafungu yote ya Wizara na Idara za Serikali, Mikoa ya Tanzania Bara, Halmashauri, Mashirika ya Umma, Balozi na Wakala wa Serikali; kukamilisha ripoti tano za ukaguzi wa ufanisi -*Value*

*for Money Audit* ambapo taarifa zote hizi zimewasilishwa hapa Bungeni tarehe 11 Aprili, 2013; ukaguzi wa Mashirika 50 ulikuwa unaendelea katika hatua mbalimbali za ukaguzi; Ofisi imeendelea kukiimarisha Kitengo cha Ukaguzi na Ufanisi kwa kutoa mafunzo kwa watumishi saba na kukipatia vitendea kazi zaidi. Aidha, ofisi iliendelea kulipia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 53 waliopo katika vyuo mbalimbali na kugharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 400. Vilevile, ujenzi wa ofisi unaendelea katika Mikoa ya Dodoma na Rukwa na unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Ofisi itatekeleza shughuli zifuatazo: Kuendelea kutekeleza mkakati wa kuwaondoa wakaguzi katika ofisi za wakaguliwa ambapo kwa kuanzia, ofisi inatarajia kupanga ofisi Dar es Salaam, Mwanza, Tanga, Tabora, Iringa na Kagera; kuanza ukaguzi wa mapato na matumizi ya vyama vyote vya siasa nchini ili kukidhi matakwa ya sheria ya vyama vya siasa na kuendelea kufanya mazungumzo na Msajili wa Vyama vya Siasa namna ya kutekeleza Sheria ya Gharama za Uchaguzi; na kuziimarisha Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali – *Public Accounts Committee (PAC)* na *Local Authorities Accounts Committee (LAAC),* Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa kuzijengea uwezo kwa njia ya mafunzo, tafiti na ushauri kwa kuzingatia mahitaji – *Based on Training Needs Assessment (TNA).*

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na kuhakiki matumizi ya fedha za Halmashauri zinazopelekwa vijijini, pamoja na kufuatilia salio la fedha ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha; kushiriki kikamilifu katika zoezi la ukaguzi wa mali katika Halmashauri zote, Mikoa, Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali ili kuhakikisha kumbukumbu za mali na fedha zinaingizwa kwenye vitabu; kushiriki kikamilifu katika jukumu jipya la kukagua Taasisi za Umoja wa Mataifa ambapo ofisi inaingia mwaka wa pili wa kuwepo kwenye Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa -*UN Board of Auditors;* kufanya kaguzi

sita za thamani ya fedha na kupanua wigo wa ukaguzi wa fedha *(Regularity Audit);* kuendelea na uunganishaji wa Ofisi za Ukaguzi zilizoko mikoani na makao makuu kwa kutumia Mtandao Mpana - *Wide Area Network (WAN);* kuimarisha ukaguzi wa kiutambuzi - *Forensic Audit;* na kuongeza idadi ya watumishi kwa kuajiri watumishi wapya 141.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa MKUKUTA huratibiwa na Wizara kupitia Mpango wa Ufuatiliaji na tathmini ya MKUKUTA Awamu ya Pili - *MKUKUTA II Monitoring Master Plan.* Mpango huu umeainisha viashiria vya kupima utekelezaji wa Malengo ya MKUKUTA II, Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015 na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara iliandaa na kusambaza ripoti zifuatazo: Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA - *MKUKUTA Annual Implementation Report (MAIR 2011/12);* Ripoti ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu – *Poverty and Human Development Reports (PHDRs 2011);* na Ripoti ya Maoni ya Watu - *Views of the People Report 2012* kuhusu jitihada za kupunguza umaskini. Ripoti hizi zinachambua kwa kina mwenendo wa viashiria katika kila lengo la MKUKUTA kwa kuainisha mafanikio, changamoto na hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya MKUKUTA II, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa *Small Enterprenuer Loan Facility (SELF),* ambao jukumu lake kuu ni kujenga uwezo wa asasi ndogo za fedha kwa kuzipatia mikopo na mafunzo ya utaalamu wa fedha, ili ziweze kuwafikia wajasiriamali wadogo na kati hususan katika maeneo yenye uhaba wa huduma za fedha. Asasi hizo ni pamoja na Vyama vya Akiba na Mikopo *(SACCOS),* Benki za Wananchi Vijijini *(VICOBA)* na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi Aprili, 2013, Mradi wa self umetoa mikopo ya shilingi bilioni 8.32 kupitia asasi ndogo za fedha zipatazo 66 kwa walengwa 5,198. Aidha, Mradi wa *SELF* umetoa mafunzo kwa wajasiriamali wapatao 1,330; watendaji 289 wa asasi wakiwemo Maofisa Mikopo, Wajumbe wa Kamati za

Mikopo, Watunza Vitabu vya Hesabu na Wajumbe wa Bodi; na Maofisa Ushirika 113 kutoka Wilaya mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa MKUKUTA II; kufanya tafiti na uchambuzi wa kitaalamu kuhusu mwenendo wa umaskini na kutoa elimu juu ya utekelezaji wa MKUKUTA; Kuandaa Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA II; Ripoti ya Hali ya Umaskini Nchini; Kuhamasisha wadau ngazi zote kuhusu masuala ya MKUKUTA na Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Aidha, Wizara itakamilisha utafiti wa kutambua programu za kinga ya jamii na fursa za maendeleo kwa makundi tete *(Vulnerable Groups)* ili kuboresha utekelezaji na ufahamu kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Mradi wa *SELF* utaendelea kutoa huduma za mikopo kwa wajasiriamali wadogo na kujenga uwezo wa asasi ndogo za fedha hususan katika maeneo ambayo hayajafikiwa. Aidha, ili shughuli za mradi kuwa endelevu, Mradi wa *SELF* utafanyiwa maboresho ya kimuundo na kuufanya kuwa Kampuni inayojitegemea chini ya Udhamini wa Serikali ambapo mapendekezo hayo yapo katika hatua ya Rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara iliendelea kuzifanyia marekebisho sheria mbalimbali ili kuweka usimamizi mzuri wa kodi na fedha za umma. Baadhi ya sheria zilizofanyiwa marekebisho ni sheria mbalimbali za kodi ambazo zilipitishwa kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2012 *(The Finance Act, 2012)* na Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu iliyofanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali iliyopitishwa na Mkutano wa Bunge wa mwezi Februari, 2013. Aidha, marekebisho ya Mkataba wa Cotonou unaohusu ushirikiano baina ya nchi za Jumuiya ya Ulaya, Afrika na Visiwa vya Caribbean ambapo Tanzania ni mwanachama, yalipitishwa na Bunge lako Tukufu kupitia Azimio la Bunge katika Mkutano wa mwezi Novemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia iliandaa kanuni mbalimbali ili kuwezesha usimamizi na utekelezaji wa Sheria za Kifedha. Baadhi ya kanuni zilizotolewa ni zile za kuanzisha *Credit Reference Databank* ya Utunzaji wa Taarifa za Wateja wa Benki na Taasisi za Kifedha, pamoja na *Credit Reference System*; Matumizi ya Vifaa vya Kielektroniki katika Ukusanyaji wa Kodi ya Mapato; Usimamizi wa Marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa abiria wa ndege ambao siyo Raia wa Tanzania; Kanuni za Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu; na Kanuni za Sheria za Uwekaji Stempu kwenye kazi za Wasanii.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara itaendelea kukamilisha maandalizi ya kuwezesha kutungwa kwa Sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani – *Value Added Tax (VAT),* Sheria ya Utawala wa Kodi - *Tax Administration Act*, Sheria ya Hoteli - *Hotels Tax Act,* Sheria ya Takwimu, Sheria ya Msajili wa Hazina na Sheria ya Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini - *Government Employees Provident Fund (GEPF);* zote hizi zitashughulikiwa. Aidha, Wizara inatarajia kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, pamoja na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ili kuihuisha kulingana na mazingira ya sasa ya uchumi. Vilevile, Wizara itaandaa kanuni mbalimbali zitokanazo na sheria hizi ili kuwezesha utekelezaji wake uwe mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara imetoa mafunzo kuhusu dhana ya Ubia kwa watumishi 33 wa Serikali na wa Sekta Binafsi. Aidha, watumishi 60 wa Serikali na wa Sekta Binafsi wamepata mafunzo ya kina kuhusu kutathmini Andiko la Awali la Miradi ya *PPP.* Vilevile, Wizara inakamilisha kuandaa kanuni za *PPP (PPP Finance Regulations)* zitakazotumika kutathmini Miradi ya Ubia. Kadhalika, Wizara imepokea maandiko *(Feasibility Studies)* na kufanya uchambuzi wa awali na kutoa ushauri katika Miradi ya Bandari ya Mtwara, Bandari ya Mwambani - Tanga, Bandari ya Kasanga Kigoma na Barabara ya Dar es Salaam - Chalinze.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/ 2014, Serikali inatarajia kupitia upya muundo wa vitengo vya *PPP* na kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Ubia; kuhamasisha watu kuhusu dhana ya biashara ya ubia; na kutoa mafunzo ya ubia kwa wadau. Aidha, Serikali itaanzisha Mfuko wa kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Ubia *(PPP Facilitation Fund).* Lengo la Mfuko huu ni kugharamia upembuzi yakinifu wa miradi inayoanzishwa kwa mfumo wa *PPP.*

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Kitengo kimeendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku *(Suspicious Transaction Reports),* ambapo taarifa 29 zilipokelewa na kuchambuliwa, kati ya hizo matokeo ya uchambuzi wa taarifa kumi ziliwasilishwa katika vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria *(Law Enforcement Agencies).* Aidha, Kitengo kimefanya ukaguzi wa watoa taarifa na kuimarisha mifumo ya kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi. Vilevile, Kitengo kimetoa mafunzo kwa makundi 357 ya wadau ikiwemo kutoka Sekta ya Benki na Taasisi nyingine za Kifedha, Sekta ya Ujenzi, Asasi zisizo za Kiserikali, Wanasheria wa Kujitegemea, Wahasibu na Wakaguzi wa Kujitegemea, Kampuni za Bima, Michezo ya Kasino na taasisi zinazojihusisha na Masoko ya Mitaji na Dhamana.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu imepanga kutekeleza yafuatayo: Kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku na kuwasilisha matokeo ya uchambuzi kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria; kuandaa miongozo ya ukaguzi *(Inspection Manuals)* kwa sekta mbalimbali za watoa taarifa; kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Kitengo na wadau wengine katika nyanja mbalimbali za udhibiti wa fedha haramu; kuandaa na kuhuisha miongozo ya utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu kwa

watoa taarifa wa taasisi mbalimbali; na kufanya tathmini ya viashiria hatarishi vya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Tume ya Pamoja ya Fedha imewasilisha katika ngazi zinazohusika mapendekezo na matokeo ya tafiti ya Usimamizi wa Deni la Taifa baina ya pande mbili za Muungano. Tume pia inaendelea na Tafiti za Mfumo Bora wa Kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Tume imefanya Tafiti ya Uhusiano wa Mwenendo wa Uchumi na Mapato ya Muungano kwa lengo la kubaini hali ya mapato kutokana na ukuaji wa uchumi na kushauri njia bora ya kuimarisha mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Tume inatarajia kukamilisha Ripoti za Tafiti ya Mfumo Bora wa Kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tafiti ya Uhusiano wa Mwenendo wa Uchumi na Mapato ya Muungano na kuwasilisha mapendekezo yatokanayo na tafiti hizo kwenye ngazi husika. Aidha, Tume inakusudia kufanya tafiti kuhusu uwekezaji kwa lengo la kubaini na kushauri njia bora za kuimarisha uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Habari, Elimu na Mawasiliano kwa Umma. Wizara imeendelea kusimamia na kuboresha mawasiliano kati yake na wadau kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara imetoa elimu kwa umma kuelezea majukumu, mafanikio na changamoto za Wizara kupitia maonesho ikiwa ni pamoja na Saba Saba, Nane Nane, Maadhimisho ya Kumbukumbu ya Uhuru wa Tanzania Bara; makala maalumu ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne; machapisho; vyombo vya habari vikiwemo Magazeti, Redio, Tovuti, Televisheni na Vipeperushi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara itaendelea kuandaa vipindi vya redio na televisheni, kuandaa machapisho na makongamano mbalimbali na kushiriki katika maonesho ya kitaifa kwa ajili ya kuelezea majukumu na utekelezaji wa shughuli za Wizara.

Aidha, Wizara itakamilisha uandaaji wa Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina jumla ya Watumishi 1,313. Kati ya hao, Watumishi 819 ni Wanaume na Watumishi 494 ni Wanawake. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kujenga uwezo wa watumishi wake ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hatua hizo ni pamoja na kupeleka watumishi 365 katika mafunzo ya muda mfupi na watumishi 57 katika mafunzo ya muda mrefu, kuthibitisha watumishi 11 kazini, kupandisha vyeo watumishi 404, kuboresha mazingira ya kazi kwa kukarabati baadhi ya ofisi na kununua vifaa vya ofisi. Aidha, Wizara imeendelea kutoa huduma stahiki kwa Watumishi wa Wizara wanaoishi na Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara inatarajia kuajiri watumishi 115 wa kada mbalimbali; kupandisha vyeo watumishi 614; na kuthibitisha watumishi kazini waliomaliza muda wao wa majaribio. Aidha, Wizara inatarajia kuwapatia watumishi 200 mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao, kutoa elimu kuhusu magonjwa sugu na kuwapatia lishe walioathirika na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utendaji wa Mashirika ya Umma pamoja na Taasisi zake. Majukumu yaliyotekelezwa kwa kushirikiana na *Consolidated Holdings Corporation (CHC)* ni pamoja na kuendelea na zoezi la urekebishaji wa mashirika yaliyo na matatizo katika Sekta za Usafirishaji, Madini, Mawasiliano, Utalii na Fedha.

Mheshimiwa Spika, Taarifa za Hesabu za Mashirika ya Umma 103 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilichambuliwa na mapendekezo kutolewa kwa Bodi za Wakurugenzi, Watendaji Wakuu wa Taasisi na Wizara husika kwa lengo la kuboresha utendaji na uangalizi wa mali ya umma. Aidha, uchambuzi wa

Miongozo ya Kiutendaji ya Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo ni Kanuni za Fedha 25, Miundo ya Utumishi 27, Kanuni za Utumishi 21 na Miundo ya Taasisi sita ulifanyika na vibali vilitolewa. Vilevile, Muundo na majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina umeidhinishwa na umeanza kutumika. Kadhalika, Ofisi ya Msajili wa Hazina imepata ofisi katika Jengo la *CHC* Mtaa wa Samora na tayari watumishi wamehamia katika ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kusimamia utendaji wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika na Taasisi za Umma na kuboresha Utawala Bora kwa kuingia Mikataba ya Utendaji *(Performance Contracts)* na Bodi za Mashirika ya Umma; kusimamia mikakati ya kurekebisha Mashirika ya Umma na uperembaji *(Monitoring and Evaluation)* wa Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa; na kuimarisha usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma ili kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kukamilisha taratibu za kutunga sheria mpya na kuwajengea uwezo Watumishi. Aidha, taratibu za kujaza nafasi mbalimbali kulingana na muundo zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2012, *CHC* ilifuatilia na kuyafanyia tathmini mashirika 170; kati ya hayo, mashirika 42 yalibainika kufanya kazi kwa faida, mashirika 70 yanafanya kazi kwa hasara na mashirika 58 hayafanyi kazi. Zoezi la tathmini juu ya utendaji wa mashirika hayo ili kuainisha kiini cha matatizo na kupendekeza hatua za kuchukua linaendelea. Aidha, mapato ya *CHC* katika kipindi hicho yalikuwa shilingi bilioni 7.68 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.3 zilizopatikana katika kipindi kilichoishia Desemba, 2011. Kuongezeka kwa mapato kumetokana na juhudi za ukusanyaji wa madeni na ufuatiliaji wa ukusanyaji wa madeni chechefu ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya

Biashara. Katika mwaka 2013, *CHC* ilipanga kubinafsisha au kurekebisha mashirika 27. Vilevile, *CHC* inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 11.35 ikiwa ni mapato kutokana na ukusanyaji wa madeni chechefu, uuzaji wa viwanja na majengo, ufilisi wa makampuni, ukusanyaji wa madeni yanayotokana na ubinafsishaji na riba.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za pensheni, Wizara imeanza utaratibu wa kulipa Pensheni kwa vipindi vya miezi mitatu mitatu badala ya vipindi vya miezi sita sita kuanzia Januari, 2012. Katika utaratibu huu, Wastaafu wanalipwa pensheni ya miezi miwili mapema *(in advance),* badala ya miezi mitano iliyokuwa inalipwa katika utaratibu wa awali. Pensheni inalipwa mwishoni mwa miezi ya Julai, Oktoba, Januari na Aprili. Aidha, Wizara imeendelea na kazi ya kuweka kumbukumbu za Wastaafu waliopo kwenye Daftari la Pensheni la Hazina kwenye Mfumo wa Kompyuta ujulikanao kwa jina la *SAPERION* kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa zao. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2013, kumbukumbu za Wastaafu 106,030 ziliwekwa kwenye mfumo wa kompyuta yetu. Zoezi hili litaendelea kufanyika katika mwaka 2013/2014 ili kukamilisha uhifadhi wa kumbukumbu za Wastaafu wote wanaolipwa kupitia Wizara ya Fedha (Hazina).

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu shughuli za Mifuko ya Pensheni iliyo chini ya Wizara ya Fedha. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF),* Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF)* na Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini *(GEPF).*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2013 Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF),* ulisajili wanachama 332,067. Katika kipindi hicho, Mfuko pia ulikusanya jumla ya shilingi bilioni 446.12. Kati ya makusanyo hayo, michango ya wanachama ni shilingi bilioni 374.76 na mapato yatokanayo na vitega uchumi ni shilingi bilioni 71.36. Matarajio ni kukusanya jumla ya shilingi bilioni 749.10 ifikapo mwisho wa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Aidha, thamani

ya Mfuko hadi tarehe 30 Aprili, 2013 ilifikia shilingi bilioni 1,112.24 na unatarajiwa kufikia shilingi bilioni 1,226.59 mwezi Juni, 2013. Jumla ya shilingi bilioni 422.16 zilitumika kulipa mafao ikiwa ni pamoja na mafao ya kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi, sawa na asilimia 93.21 ya lengo la mwaka. Vilevile, ili kuongeza wigo wa wanachama, Mfuko umeanzisha mpango maalum wa kuchangia kwa hiyari kwa watumishi wa sekta rasmi na isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Mfuko unatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 680.55. Kati ya makusanyo hayo, michango ya wanachama ni shilingi bilioni 539.18, na mapato yatokanayo na vitega uchumi ni shilingi bilioni 141.37. Aidha, thamani ya Mfuko inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 1,522.01. Mfuko unatarajia kulipa kiasi cha shilingi bilioni 522.32 kwa ajili ya mafao mbalimbali ikiwa ni pamoja na kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi, ambapo jumla ya wanachama wapatao 7,647 wanatarajiwa kustaafu kwa mujibu wa sheria. Vilevile, Mfuko unatarajia kuwekeza kiasi cha shilingi bilioni 1,211.39 kwenye maeneo mbalimbali ya vitega uchumi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini *(GEPF)* hadi kufikia Machi, 2013 umesajili jumla ya wanachama 6,755, wakiwemo Wananchi waliojiajiri wenyewe katika sekta isiyo rasmi. Katika kipindi hicho, michango ya wanachama ilifikia kiasi cha shilingi bilioni 22.74 sawa na asilimia 64.60 ya malengo ya mwaka mzima. Mapato yatokanayo na vitega uchumi yamefikia shilingi bilioni 11.64, ambayo ni sawa na asilimia 72.75 ya malengo ya mwaka mzima na thamani ya Mfuko imeongezeka na kufikia shilingi bilioni 190.0 Machi, 2013. Aidha, Mfuko umelipa mafao ya shilingi bilioni 7.13 hadi kufikia Machi, 2013 na kufungua ofisi katika Manispaa za Temeke, Kinondoni na Ilala kwa lengo la kusogeza huduma karibu na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Mfuko utaendelea na jitihada zake za kuboresha huduma kwa wanachama, kutanua wigo wa wanachama, kukuza mapato yatokanayo na uwekezaji na kusajili

wanachama wengi zaidi kupitia Mpango wa Hiari wa kujiwekea akiba ya uzeeni na wa lazima. Aidha, Mfuko unatarajia kusajili jumla ya wanachama 16,500 na kukusanya michango yenye thamani ya shilingi bilioni 40.50. Vilevile, mapato ya vitega uchumi yataongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 19.24 na thamani ya Mfuko huu inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 227.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF),* katika mwaka 2012, ulikusanya shilingi bilioni 229.1 kutokana na michango ya wanachama, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 21.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 188.1 zilizokusanywa mwaka 2011. Ongezeko hili lilitokana na waajiri kuzingatia sheria kwa kuleta michango kwa wakati na uandikishaji wa wanachama wapya. Aidha, idadi ya wanachama imeongezeka kutoka 180,049 mwaka 2011 hadi 203,981 mwaka 2012. Mfuko pia ulilipa mafao ya jumla ya shilingi bilioni 99.4. Mafao hayo ya *PPF* yalijumuisha na mafao ya elimu ambayo hulipwa kwa ajili ya kusomesha watoto wasiozidi wanne wa mwanachama aliyefariki akiwa kazini. Mwaka 2012 Mfuko ulisomesha watoto 1,333 kwa gharama ya shilingi milioni 683, ikilinganishwa na watoto 1,392 waliosomeshwa mwaka 2011 kwa gharama ya shilingi milioni 573. Watoto hawa husomeshwa kuanzia elimu ya chekechea hadi kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, mapato yatokanayo na uwekezaji yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 91.4 mwaka 2011 hadi kufikia shilingi bilioni 105.5 kwa mwaka 2012, ikiwa ni ongezeko la asilimia 15.4. Aidha, thamani ya Mfuko huu kufikia Desemba, 2012, ilikuwa imeongezeka kufikia shilingi bilioni 1,089.8 ikiwa ni ongezeko la asilimia 21.8 ikilinganishwa na thamani ya Mfuko ya shilingi bilioni 894.5 iliyokuwepo Desemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, Mfuko unatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 281.7, kuandikisha wanachama wapya 72,000 kutoka sekta ya umma na binafsi na kukusanya shilingi bilioni 125.6 kutokana na uwekezaji ifikapo

Desemba, 2013. Aidha, thamani ya Mfuko inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 1,302.68.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na changamoto kadhaa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo Wanachama kulalamikia kiwango kidogo cha mafao kitolewacho na baadhi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pale wanapostaafu. Vilevile, kuna suala la malimbikizo ya madeni yanayotokana na Mifuko kugharimia utekelezaji wa Miradi ya Serikali. Aidha, katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo, Serikali kupitia Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii, imepanga kutathmini uwezo wa Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii na kupendekeza viwango vya mafao na kuhakikisha kwamba, Mifuko hiyo inakuwa endelevu. Vilevile, Serikali inaendelea kulipa madeni ya Mifuko ya Jamii kwa awamu na pia imeunda kamati ya kuchambua na kuhakiki madeni mengine ya baadhi ya Mifuko hiyo ili kupendekeza njia endelevu ya kulipa mafao stahiki.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* imeendelea kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maboresho wa mwaka 2008/2009 - 2012/2013 ambao umekuwa msingi wa kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato mwaka hadi mwaka. Katika jitihada za kuongeza mapato ya ndani, Wizara kupitia *TRA* imetekeleza yafuatayo: Kuanzisha mfumo wa kimtandao wa kuwasilisha *tax returns;* kufanya tathmini maeneo hatarishi katika Utawala wa Sekta za Umma; kuweka mfumo wa taarifa wa *RADDEX 2* na kutoa mafunzo kwa watumiaji; kusambaza Mfumo wa Ki-elektroniki wa Kufuatilia Usafirishaji Mizigo *(Electronic Cargo Tracking System);* na kuboresha mfumo wa utunzaji kumbukumbu na Taarifa za Magari. Aidha, *TRA* imekamilisha uandaaji wa Awamu ya Nne ya Mpango wa Maboresho (2013/2014 - 2017/2018) unaotarajiwa kuanza kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na *TRA* itaendelea na azma yake ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani

kwa kupanua wigo wa makusanyo na kuchukua hatua mbalimbali za kisera na kiutawala katika maeneo ya mapato yatokanayo na kodi. Serikali itaendelea kuwa makini kuhakikisha kwamba, kodi inalipwa na inalipwa kama inavyostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Bodi ya Rufani za Kodi *(TRAB),* imepokea jumla ya rufani 127 na kusikiliza na kutolea maamuzi rufani 95. Bodi pia imetoa elimu kwa walipa kodi kuhusu taratibu za kukata rufaa za kodi na sheria za kodi katika Mikoa ya Tabora, Singida na Shinyanga. Aidha, Bodi imeandaa *Tanzania Tax Law Reports* kwa rufaa zote zilizoamuliwa mwaka 2009 - 2010 ambapo kwa sasa ripoti hizo zipo katika hatua ya mwisho ya uchapishaji vitabu. Kwa upande wa Baraza la Rufani za Kodi *(TRAT),* jumla ya rufani 31 zimepokelewa, kati ya hizo rufani 29 zimesikilizwa na kutolewa maamuzi. Baraza pia limetoa elimu kwa walipa kodi kuhusu taratibu za kukata rufaa za kodi na sheria za kodi katika Mkoa wa Mwanza. Katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara kupitia Bodi ya Rufani na Baraza la Rufani za Kodi itaendelea kutoa elimu kwa walipa kodi juu ya taratibu za kukata rufaa za kodi na kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi na Baraza juu ya taratibu za kutatua migogoro ya kodi itokanayo na Sheria za Kodi zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, Bodi ya Rufani inatarajia kuchapisha *Tanzania Tax Law Reports* za mwaka 2011 – 2012 kwa ajili ya rejea kwa wadau wake.

Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara kwa kupitia Benki Kuu imeendelea kutekeleza mabadiliko chanya katika Sekta ya Fedha ili kuhakikisha kuwa, sekta hiyo inachochea maendeleo ya jamii na ukuaji wa uchumi. Mabadiliko ya Sekta ya Fedha yamesababisha utendaji mzuri wa Taasisi za Fedha, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya mabenki kutoka benki 49 mwezi Februari, 2012 mpaka benki 51 mwisho wa mwezi Februari, 2013. Aidha, rasilimali za mabenki zimeimarika zaidi na kufikia shilingi trilioni 17.3 mwezi Februari ambapo mikopo iliyotolewa kwa sekta binafsi imefikia shilingi trilioni 8.8.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Benki Kuu ya Tanzania imetoa Mwongozo wa Huduma za Kibenki kwa kutumia Wakala wa 2013 (*Guidelines on Agent Banking for Banking Institutions*, 2013), ambao ulianza kutumika mwezi Februari, 2013.

Mheshimiwa Spika, kutolewa kwa mwongozo huu ni sehemu ya mpango wa kuweka mazingira yatakayowezesha kupanua wigo wa huduma za kibenki na kuhakikisha usalama wa benki mbalimbali zitakazojihusisha na mfumo wa utoaji huduma za kibenki kwa kutumia Mawakala. Mfumo huu utarahisisha upatikanaji wa huduma bora na nafuu za kibenki.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu imeunda Kamati ya Kitaifa ya Udhibiti wa Mfumo wa Fedha *(Tanzania Financial Stability Forum)* ili kusaidia kuimarisha ushirikianona kubadilishana taarifa kati ya wadhibiti wa sekta ya fedha, kama msingi imara kwa ajili ya kuhakikisha uthabiti wa mfumo wa fedha nchini na kupanua wigo wa usimamizi katika mfumo wa fedha kutoka usimamizi unaolenga taasisi moja kwenda usimamizi wa mfumo wa fedha unaolenga sekta nzima ya fedha kwa ujumla wake. Aidha, taarifa inaonesha hali halisi ya udhibiti wa sekta ya fedha inatolewa kila baada ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu za Afrika Mashariki zilikubaliana kutengeneza mfumo wa malipo utakaorahisisha malipo kwa kutumia sarafu za nchi husika. Mfumo huu utakaojulikana kama *East African Cross Border Payment System (EAPS)* umefikia hatua ya majaribio kupitia mifumo ya malipo makubwa *(Real Time Gross Settlement System – RTGS)* ya nchi za Tanzania, Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, mategemeo ni mfumo huu kuanza kutumika kwa nchi hizi tatu ikiwa taratibu zote za kujiungana na mfumo huu zitakuwa zimekamilika mwezi Julai mwaka huu. Aidha, nchi za Rwanda na Burundi zitakapokuwa tayari zitajiunga na mfumo huu. Kuanza kwa mfumo huu wa malipo kutarahisisha malipo katika Jumuiya na kukuza shughuli za kibiashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/ 2014, Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu itaandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya kusimamia mifumo ya malipo nchini *(National Payment Systems Act)*. Aidha, Benki Kuu itaendelea kuandaa sera za kifedha na kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu itafanya tathmini ya mpango wa utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Fedha unaoishia Juni, 2013 na kuandaa mpango wa utekelezaji wa awamu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, Benki Kuu itahakikisha Mwongozo wa Kitaifa kuhusu elimu ya masuala ya fedha (*Financial Education Framework*) unazingatiwa. Mwongozo huu unalenga kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuweka akiba na kutumia huduma za fedha katika shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Maendeleo *Tanzania Investment Bank* - *TIB Development Bank;* katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Benki ilifungua tawi Mkoani Mbeya na ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, hii inafanya benki kuwa na jumla ya matawi matano na ofisi tatu za kanda. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2012, Benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 242.9 ikilinganishwa na mikopo ya shilingi bilioni 181.7 Desemba, 2011, sawa na ongezeko la asilimia 74.8.

Mheshimiwa Spika, mikopo mingi ilitolewa kwenye sekta ya kilimo na usindikaji wa mazao ya kilimo (mikopo hii ni tofauti na ile ya Dirisha la kilimo). Benki ilipata faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 8.6 ikiwa ni ongezeko la asilimia 48 toka shilingi bilioni 5.8 zilizopatikana mwaka ulioishia Desemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, Dirisha la Kilimo katika Benki ya Maendeleo *TIB* liliendelea kutoa mikopo kwa wakopaji mbalimbali kwa riba nafuu. Tangu kuanza kwa dirisha mwaka

2010 hadi kufikia Desemba, 2012, maombi yenye thamani ya shilingi bilioni 40.1 yaliidhinishwa ambapo shilingi bilioni 20.0 (asilimia 49.9) zilikopeshwa kwa makampuni; shilingi bilioni 5.7 (asilimia 14.2) kwa taasisi ndogo za fedha zinazokopesha wakopaji wadogo; na shilingi bilioni 14.4 (asilimia 35.9) kwa vikundi vya kuweka na kukopa *(SACCOS)* ambavyo pia vinafaidisha wakopaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, hii inamaanisha asilimia 50.1 ya mikopo imetolewa kwa wajasiriamali wadogo. Aidha, kuanzia Julai, 2013 Dirisha la Kilimo lililopo *TIB* litahamishiwa katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba, 2013, mikopo inayotolewa na Benki ya Maendeleo *TIB* katika sekta mbalimbali inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 379.2 na faida kabla ya kodi inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 16.6.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na mpango wake wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania – *TADB*. Lengo la kuanzisha benki hiyo ni kutoa mikopo ya muda mfupi, wa kati na mrefu katika sekta ya kilimo inayojumuisha uvuvi na mifugo. Aidha, muundo wa benki ya kilimo na majukumu ya wafanyakazi katika nafasi mbalimbali umeandaliwa. Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wameteuliwa na ajira za maafisa waandamizi wa benki hiyo inatarajiwa kukamilika hivi karibuni. Katika mwaka 2013/2014, shilingi bilioni 10 zimetengwa ili kukamilisha lengo la mtaji wa kuanzia wa shilingi bilioni 100.

Mheshimiwa Spika, Twiga *Bancorp*, katika kipindi kinachoishia Desemba, 2012 Taasisi iliendelea kupanua shughuli zake kwa kufungua tawi moja Mkoani Dodoma na kuifanya taasisi kuwa na matawi matano. Katika kipindi hicho, amana za wateja zilifikia shilingi bilioni 58.41 ikilinganishwa na shilingi bilioni 54.2 Desemba, 2011 sawa na ongezeko la asilimia 7.8.

Mheshimiwa Spika, aidha, mikopo iliyotolewa ilifikia shilingi bilioni 39.43 ikilinganishwa na shilingi bilioni 35.9 kwa

mwaka ulioishia Desemba, 2011 sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Vile vile, Taasisi iliwekeza shilingi bilioni 4.7 kwenye Dhamana za Serikali na Amana katika Benki zingine ikilinganishwa na shilingi bilioni 19.0 zilizowekezwa katika kipindi kama hicho mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka unaoishia Desemba, 2013, amana za wateja zinatarajiwa kufikia shilingi bilioni 73.25 kutoka shilingi bilioni 58.41 za Desemba, 2012; mapato kutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara yanatarajia kufikia shilingi bilioni 12.66 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9.56 zilizokusanywa Desemba, 2012; na mtaji ghafi wa Benki (*Owners' Equity)* unatarajiwa kukua kutoka shilingi bilioni 5.81 hadi shilingi bilioni 7.24 ifikapo Desemba 2013.

Mheshimiwa Spika, aidha, thamani ya mikopo kwa wateja inatarajia kufikia shilingi bilioni 49.10 na uwekezaji katika Dhamana za Serikali na Amana za Muda Maalum kwenye mabenki unatarajia kufikia shilingi bilioni 16.80. Vile vile, Taasisi inatarajia kupata faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 0.48.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Posta *(Tanzania Postal Bank)*; katika kipindi cha mwaka 2012 Benki ilianzisha huduma mpya ya *Platinum Account* inayowalenga vijana walio katika Vyuo Vikuu na Taasisi nyingine za elimu ya juu. Manufaa ya huduma hii ni kuwawezesha vijana kujiwekea akiba na kupitishia mikopo ya elimu. Aidha, Benki iliendelea kupanua mtandao wake kwa kufungua matawi madogo katika ngazi ya Wilaya katika vituo vya Shirika la Posta.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Benki ilianzisha huduma ya POPOTE *Quick Account*, inayomwezesha mteja kupata huduma za benki mahali popote kupitia simu ya mkononi kwa lengo la kuwafikia wananchi walio wengi wanaoishi vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012, amana za wateja zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 120.92 mwaka 2011 hadi kufikia shilingi bilioni 144.56 ikiwa ni ongezeko la asilimia 19.4. Aidha, benki ilitoa mikopo yenye thamani ya

shilingi bilioni 103.34 ikilinganishwa na shilingi bilioni 66.75 mwaka 2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 54.83. Vile vile, uwekezaji katika vitega uchumi vya Benki ya Posta umeongezeka kutoka shilingi bilioni 117.67 mwaka 2011 hadi kufikia shilingi bilioni 146.96, ikiwa ni ongezeko la asilimia 24.9.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, Benki imepata faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 3.59 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.58 mwaka 2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 39.4. Katika mwaka 2012/2013, Serikali iliiongezea Benki ya Posta mtaji wa shilingi bilioni 1.5 na kufanya mtaji wa benki kuwa jumla ya shilingi bilioni 16.82.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013, benki itaendelea na mkakati wake wa kuimarisha huduma zitolewazo kupitia Shirika la Posta kwa kukarabati na kuunganisha katika mtandao wa benki vituo 10 vya Posta vilivyoko Temeke, Tunduma, Kahama, Geita, Masasi, Peramiho, Njombe, Kyela, Simiyu na Kasulu hivyo kuvipa uwezo wa kutoa huduma za haraka. Vituo hivi vitakuwa ni matawi madogo na hivyo kufanya benki kufikisha jumla ya matawi 23. Aidha, benki itafunga vifaa vya kielektroniki katika vituo vya mauzo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Benki inatarajia kupanua wigo wa mikopo kwa kuingia mikataba na Sekretarieti za Mkoa na Jeshi la Kujenga Taifa na kuongeza kipindi cha marejesho kutoka miaka mitatu hadi minne. Kadhalika, Benki inatarajia kupata faida baada ya kodi ya shilingi bilioni 5.11 ikiwa ni ongezeko la asilimia 25.5 ikilinganishwa na faida ya shilingi bilioni 4.07 iliyopatikana mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, huduma za bima; katika mwaka 2012, Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imeendelea na mchakato wa kuanzisha Baraza la Usuluhishi la Bima (*Insurance Ombudsman*) ambapo kwa sasa Mamlaka imekamilisha uandaaji wa Kanuni zitakazoongoza utendaji wa Baraza hilo na kusambaza kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imefungua ofisi katika Jiji la Mbeya kwa ajili ya kutoa huduma katika Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Hii inafanya idadi ya Ofisi za Kanda zilizofunguliwa hadi sasa kufikia tatu ikijumuisha ofisi zilizopo Kanda ya Kaskazini katika Jiji la Arusha na Kanda ya Ziwa katika Jiji la Mwanza. Aidha, Mamlaka inaendelea na maandalizi ya kufungua ofisi nyingine za kanda katika mikoa ya Dodoma (Kanda ya Kati) na Mtwara (Kanda ya Kusini).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Mamlaka inatarajia kuendelea na taratibu za kuoanisha sheria na kanuni za soko la bima katika eneo la Afrika Mashariki na nchi za *SADC*; kuendelea kushirikiana na Vyuo Vikuu vya hapa nchini na nje ya nchi kwa ajili ya kurahisisha utolewaji wa elimu ya juu ili kupatikane wataalam wengi wa fani ya bima; na kukamilisha tafiti za bima ya kilimo na mifugo, bima ya watu wa kipato cha chini *(micro-insurance)* na namna bora ya kuanzisha bima inayofuata Sheria za Kiislam - *Takaful*. Aidha, Mamlaka inatarajia kuanzisha vipindi vya utoaji wa elimu ya bima katika vyombo vya habari, vyuoni na mashuleni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Shirika la Bima la Taifa limeendelea na utekelezaji wa mkakati wa kuligawa Shirika katika kampuni mbili tofauti, moja ya bima za maisha na nyingine ya bima za kawaida. Shirika limeanza kutenganisha hesabu za biashara hizi mbili lengo likiwa kujua uwezo wa kila kampuni kujiendesha kibiashara. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2012, Shirika lililipa madai ya shilingi bilioni 6.79 kwa wateja wake.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2012, mapato ya bima yalikuwa shilingi bilioni 27.87, mapato ya Shirika kutokana na bima za mtawanyo *(reinsurance income)* yalifikia shilingi bilioni 2.08 na mapato kutokana na vitega uchumi yalifikia shilingi bilioni 5.17. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, *NIC* itaendelea na utekelezaji wa mkakati wa kuligawa Shirika katika kampuni mbili kwa mujibu wa Sheria ya Bima ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, masoko ya mitaji na dhamana; katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imekamilisha uanzishwaji wa soko la ujasiriamali (*Enterprise Growth Market*) ikiwemo kutoa leseni na Mafunzo kwa wataalam washauri (*Nominated Advisors*) watakaoshauri kampuni zinazotaka kujiorodhesha kwenye soko la kampuni za ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, soko la kukuza ujasiriamali liko tayari kwa kampuni kujiorodhesha na Mamlaka inaendelea kutoa elimu juu ya fursa zilizopo kwenye Soko hilo. Aidha, Mamlaka imeandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano 2013/2014 - 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imekamilisha utafiti kuhusu mfumo wa kisheria na uendeshaji wa soko la Hatifungani za Manispaa *(Municipal Bond)*. Aidha, Mamlaka inafanya maandalizi ya kuanzisha soko mbadala la hatifungani ikiwa ni pamoja na kuandaa taratibu za soko hilo. Maandalizi yote muhimu yanatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Mamlaka imefanya tafiti nyingine tatu ambazo zinahusu Mfumo wa Kisheria na Usimamizi wa Soko la Bidhaa; muundo wa soko la bidhaa; na uhusiano kati ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na Soko la Bidhaa. Tafiti hizi zitasaidia kuweka mazingira yatakayowezesha uanzishwaji wa Soko la Bidhaa nchini.

Mamlaka pia imetayarisha Mpango Kazi juu ya uanzishwaji wa Soko la Bidhaa ambao unatarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka 2013/2014. Kadhalika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka imepanga kuandaa sera na mpango wa Kitaifa wa maendeleo ya masoko ya mitaji na dhamana.

Mheshimiwa Spika, soko la Hisa Dar es Salaam *(DSE);* hadi kufikia Aprili 2013, hisa zilizoorodheshwa kwenye soko ni hisa milioni 35.4 za ziada na upendeleo za *DCB Commercial Bank*. Kwa upande wa uuzaji na ununuzi wa dhamana, hisa

zenye thamani ya shilingi bilioni 49.25 ziliuzwa. Vile vile, hatifungani za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 379.61 ziliuzwa.

Mheshimiwa Spika, *DSE* iliendelea na mipango ya maandalizi ya uzinduzi wa Soko la Ujasiriamali (*Enterprise Growth Market- EGM*) kwa kupitia upya kanuni za soko na kufuatilia kwa Mamlaka hatua za upatikanaji leseni kwa kampuni za udhamini. Rasimu ya kanuni mpya za soko imewekwa katika tovuti ya *DSE (www.dse.co.tz)* ili kupata maoni kutoka kwa wadau. Aidha, utafiti kuhusu kubadilisha Soko kuwa kampuni inayojiendesha kibiashara umefanyika na *DSE* wataandaa mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/ 2014, *DSE* inatarajia kuweka mazingira yatakayowezesha kampuni za sekta muhimu kama madini na mawasiliano ya simu kuorodheshwa sokoni; kupanua wigo wa huduma za soko na kuimarisha muundo wa Soko kuendana na mahitaji ya ukuaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, *UTT* imeanzisha Mfuko mpya wa uwekezaji wa pamoja unaolenga kuwekeza katika masoko ya fedha na dhamana ujulikanao kama *Liquid Fund*. Mfuko huu unatoa njia mbadala kwa Wawekezaji wanaotaka kuweka fedha zao katika kipindi cha muda mfupi na katika kiwango kilichopo kwenye ushindani. Aidha, kuanzia mwezi Aprili, 2013, *UTT* imeanza kutoa mikopo ili kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, *UTT* inatarajia kuanzisha Mfuko mmoja wa uwekezaji wa pamoja ujulikanao kwa jina *Dollar Fund*. Mfuko huu uliahirishwa kuanzishwa mwaka wa huu wa fedha ili kutoa muda zaidi wa kutathmini mazingira ya uendeshaji wa Mfuko kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya fedha za kigeni nchini. Aidha, *UTT* itaendelea kuhamasisha uelewa juu ya dhana ya uwekezaji kupitia elimu kwa umma kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kitaalam na Huduma nyinginezo Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS)*; katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendesha zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa Tanzania ina idadi ya watu 44,928,923 ambapo Tanzania Bara kuna watu 43,625,354 na Tanzania Zanzibar kuna watu 1,303,569. Serikali imekwishasambaza matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shughuli ya sensa, *NBS* ilitayarisha na kusambaza Takwimu za Msingi *(Core Statistics)* ambazo zilihusisha ukokotoaji wa Pato la Taifa. Aidha, *NBS* ilifanya tafiti za kijamii na kiuchumi na kusambaza viashiria vilivyotokana na tafiti hizo kwa wadau wote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/ 2014, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kutekeleza jukumu lake la kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu rasmi kwa wadau wote nchini kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Takwimu, Sura 351. Vile vile, *NBS* itaendelea na kazi ya uchambuzi na uchapishaji wa makala ya takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi *(NBAA);* hadi kufikia Desemba, 2012, idadi ya Wahasibu waliosajiliwa ilikuwa 4,281, kati ya hao: watunza vitabu ni 208; Wahasibu wahitimu 2,254; Wahasibu waliosajiliwa ngazi ya *CPA* 1,185; Wahasibu waliosajiliwa kama Wakaguzi Hesabu katika ngazi ya *CPA-PP* 452; Kampuni za Ukaguzi Hesabu zilizosajiliwa 166; na Kampuni za Uhasibu zilizosajiliwa 16.

Mheshimiwa Spika, aidha, *NBAA* imekamilisha kuhariri mitaala na silabi za taaluma ya uhasibu ambapo mitihani ya kwanza chini ya silabi mpya inatarajiwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2013/2014. Vile vile, Bodi inaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa Kituo cha Taaluma ya Uhasibu eneo la Bunju - Dar es Salaam unaotarajiwa kukamilika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi *(PSPTB)*, katika mwaka 2012/2013, Bodi imetahini wanataaluma 1,971 ambapo wanataaluma 744 sawa na asilimia 37.7 walifaulu hivyo kufanya idadi ya wahitimu kufikia 20,610 ikijumuisha wahitimu wa Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa. Aidha, Bodi ilitoa mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu 25 kutoka vyuo mbalimbali vya elimu ya juu kwa lengo la kuwajengea uzoefu wa kazi ili waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/ 2014, Bodi inatarajia kutekeleza yafuatayo: kutoa mafunzo endelevu kwa wataalam ili kuboresha uwezo wa utendaji; kuongeza idadi ya watahiniwa wa mitihani na usajili kwa wanataaluma na kuboresha mazingira ya kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/ 2013, hadi kufikia Aprili 2013, Bodi imekusanya kodi ya shilingi bilioni 9.58 sawa na asilimia 85.23 ya lengo la shilingi bilioni 11.24. Aidha, mapato ya Bodi yalifikia shilingi bilioni 4.29 sawa na asilimia 81.01 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 5.37. Katika mwaka 2013/14, Jumla ya shilingi bilioni 15.16 zinatarajiwa kukusanywa na Bodi, ikiwa ni kodi itokanayo na michezo ya kubahatisha. Aidha, mapato ya Bodi yanatarajiwa kufikia 6.68 na ongezeko la asilimia 24.39.

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Mafunzo, katika mwaka 2012/2013, Taasisi ya Uhasibu Arusha *(IAA)* imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika ngazi za stashahada ya juu na uzamili ambapo jumla ya wanafunzi 3,303 walidahiliwa. Aidha, Wanafunzi 1,708 walihitimu katika mwaka wa masomo 2011/2012, katika ngazi na fani mbalimbali hivyo kuifanya *IAA* kufikisha jumla ya wahitimu 8,010 toka mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, *IAA* inakusudia kuanzisha Kituo cha Elimu kwa Njia ya Mtandao (*e-Learning Centre*); kuanzisha Kitengo cha Masomo ya Jioni na kuanzisha Kampasi ya masomo katika Mji wa Babati, Mkoani Manyara.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)*, katika mwaka 2012/2013, Chuo kilifanya maandalizi ya kuanzisha kozi mpya nne za Shahada ya Uzamili za: Uhasibu na Fedha, Fedha na uwekezaji, Menejimenti ya Rasilimali Watu na Biashara *(MBA)* ambayo itaendeshwa kwa ushirikiano na Chuo cha *IIFT* (*Indian Institute of Foreign Trade*) cha India. Aidha, Chuo kilidahili wanafunzi 9,500 katika kozi na fani mbalimbali, ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 1,500 sawa na asilimia 18.75 kulinganisha na mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, chuo kitatekeleza yafuatayo: kuanza maandalizi ya ujenzi wa Kampasi ya Msata yenye uwezo wa kuchukua zaidi ya wanafunzi 15,000; kuboresha ufanisi wa chuo katika utafiti, machapisho na majarida; kuboresha mlingano wa kijinsia; kuboresha mifumo ya habari na utoaji huduma; na kukitangaza chuo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)*; katika mwaka 2012/2013, *TIA* ilidahili wanafunzi 8,379. Aidha, Taasisi imefungua tawi jipya katika Jiji la Mwanza. Vile vile, Taasisi imeendelea na mipango ya kuanzisha tawi katika Mji wa Kigoma ili kuhudumia Mikoa ya Kigoma, Tabora na Rukwa na hivyo kusogeza huduma zake karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, *TIA* inatarajia kuanza maandalizi kwa ajili ya kutoa mafunzo ya Shahada ya Uzamili kwa kushirikiana na vyuo vya nje ya nchi. Matarajio kwa mwaka ujao wa fedha ni kufikia Wanachuo 8,800.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini *(IRDP)* kilifanya udahili kwa wanafunzi 2,394 na kufanya jumla ya wanafunzi kufikia 4,600. Katika kipindi hicho, wanafunzi 1,490 walihitimu katika kozi mbalimbali. Aidha, Chuo kilikamilisha uandaaji wa mitaala na kuanzisha Programu tano (5) mpya kwa ajili ya Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili.

Mheshimiwa Spika, Programu hizo mpya ni Shahada

ya Mipango na Usimamizi wa Rasilimali Watu; Shahada ya Uchumi wa Maendeleo; Shahada ya Mipango Miji na Usimamizi wa Mazingira; Shahada ya Uzamili katika Uchumi wa Maendeleo; na Shahada ya Uzamili katika Mipango na Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Chuo kinatarajia kukamilisha mradi wa ujenzi wa jengo la pili la Taaluma Kampasi ya Dodoma. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuongeza udahili wa wanafunzi na kuwa na mazingira bora katika kutimiza majukumu ya kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – *EASTC*, katika mwaka 2012/2013, Chuo kilidahili wanafunzi 177 katika fani ya Takwimu kwa ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada. Chuo pia kiliendesha mafunzo ya Takwimu za Kilimo chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kushirikiana na Chuo cha *NASA* kilichopo India. Mafunzo hayo yalitolewa kwa Maofisa 30 kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali. Chuo pia kilitoa mafunzo ya muda mfupi ya uchambuzi wa takwimu kwa watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Chuo kitaendesha mafunzo ya muda mfupi kwa nchi zinazotumia huduma ya Chuo ili kuzijengea uwezo na kuongeza idadi ya watumishi wenye uelewa na weledi wa kukusanya na kuchambua takwimu. Aidha, Chuo kinatarajia kuongeza idadi ya kozi kufikia nane. Kozi mpya zinazotarajiwa kuanza kufundishwa ni Shahada ya Takwimu katika Kompyuta, Stashahada za Uzamili katika Takwimu Rasmi na Takwimu za Kilimo na kozi ya Uzamili katika Takwimu za Kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kudhibiti matumizi ya fedha za umma sambamba na kuongeza mapato ya Serikali;

(ii) Kuzingatia kanuni na taratibu zilizoainishwa

kwenye Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA) na upatikanaji wa fedha kutoka kwa wafadhili wa nje;

(iii) Kuwa na Sera ya Mali ya Serikali;

(iv) Kufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi;

(v) Kuwepo kwa mahitaji makubwa ya fedha nje ya bajeti;

(vi) Kuwepo kwa mchakato mrefu wa upatikanaji wa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo hasa mikopo ya kibiashara *(non-conscessional borrowing)*; na

(vii) Kuongezeka kwa malimbikizo ya madeni ya ndani katika mafungu mbalimbali ambayo yameshindwa kuingizwa kwenye viwango vya bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara itachukua hatua kupitia mipango na bajeti zake ili kuhakikisha kuwa changamoto hizi zinapatiwa ufumbuzi katika mwaka 2013/2014 na kuendelea. Ufumbuzi wa changamoto hizi utaelezwa katika hotuba ya bajeti ya Serikali itakayowasilishwa tarehe13 Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, majukumu ya Wizara yalitekelezwa katika mafungu sita ya kibajeti. Mafungu hayo ni Fungu 50 - Wizara ya Fedha; Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 22 - Deni la Taifa; Fungu 21 – HAZINA; Fungu 13 - Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu; na Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha. Aidha, Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo inajitegemea linaombewa fedha Bungeni na Waziri wa Fedha kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Fungu 50 - Wizara ya Fedha, Wizara ilitarajia kupata shilingi bilioni 124.42 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato yasiyo ya kodi kupitia Fungu 50.

Vyanzo hivyo ni pamoja na mauzo ya mali, uuzaji wa nyaraka za zabuni na mapato kutoka katika Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali (Gawio, Michango na Marejesho ya mikopo).

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2013, makusanyo yalifikia shilingi bilioni 37.27 sawa na asilimia 29.95 ya lengo. Makusanyo zaidi yanatarajiwa katika robo ya nne ya mwaka wa fedha baada ya Mashirika mengi kuandaa hesabu za mwaka na ukaguzi wa hesabu hizo kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya Fungu 50 kwa mwaka 2012/2013 yalikuwa shilingi bilioni 98.41 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 546.51 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2013, matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 70.32 sawa na asilimia 71.46 ya makadirio na matumizi ya maendeleo yalifikia shilingi bilioni 311.28 sawa na asilimia 56.96 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; kwa mwaka 2012/2013 yalikuwa shilingi bilioni 75.12 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 6.12 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2013, matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 49.34 sawa na asilimia 65.68 ya makadirio na matumizi ya maendeleo yalifikia shilingi bilioni 1.29 sawa na asilimia 21.08 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, makadirio ya matumizi ya Fungu 22 – Deni la Taifa, yalikuwa shilingi bilioni 2,735.91. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2013 matumizi ya fungu hili yalifikia shilingi bilioni 2,226.70 sawa na asilimia 81.39 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, Fungu 21 – Hazina; katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi bilioni 8,070. Hadi kufikia Aprili, 2013, *TRA* ilikusanya shilingi bilioni 6,580 sawa na asilimia 97.84 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 6,725 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya Fungu 21 kwa mwaka 2012/2013 yalikuwa shilingi bilioni 725.57 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 101.95 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, kiasi cha Shilingi bilioni 50.66 kilifanyiwa uhamisho kuongezea katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi na kufanya makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013 kuwa shilingi bilioni 152.61. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2013, matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 516.61 sawa na asilimia 71.2 ya makadirio na matumizi ya maendeleo yalifikia shilingi bilioni 131.95 sawa na asilimia 86.46 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu kwa mwaka 2012/2013, yalikuwa shilingi bilioni 2.16 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 0.26 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2013, matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 1.01 sawa na asilimia 46.76 ya makadirio, na matumizi ya maendeleo yalifikia shilingi bilioni 0.04 sawa na asilimia 15.38 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha, makadirio ya matumizi ya kawaida kwa Fungu hili yalikuwa shillingi bilioni 1.99, hadi kufikia Aprili, 2013 matumizi yalifikia shilingi bilioni 1.33 sawa na asilimia 66.83 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2012/2013 yalikuwa shilingi bilioni 55.02 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 9.62 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2013, matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 39.51 sawa na asilimia 71.81 ya makadirio na matumizi ya maendeleo yalifikia shilingi bilioni 3.18 sawa na asilimia 33.06 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ya Fedha inakadiria kukusanya mapato yasiyo ya kodi yapatayo shilingi 2,718,102,000 (bilioni 2.72) kupitia Fungu 50 - Wizara ya Fedha na shilingi 124,013,512,000 (bilioni 124.01) kupitia Fungu (7)- Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu na kazi za Wizara kwa mwaka 2012/2013, changamoto na hatua zilizochukuliwa na mpango na malengo ya bajeti kwa mwaka 2013/2014, nawasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa mwaka 2013/2014 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 50, 23, 22, 21, 13, 10, (7) na 45 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 50 – Wizara ya Fedha, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2013/14, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida Sh. 53,011,091,000 (bilioni 53.01). Kati ya hizo mishahara ni sh. 4,564,609,000 (bilioni 4.56) na matumizi mengineyo sh. 48,446,482,000 (bilioni 48.45).

(b) Miradi ya Maendeleo Sh. 233,669,169,000 (bilioni 233.67). Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani – Sh. 10,200,000,000 (bilioni 10.20).

(ii) Fedha za Nje – Sh. 223,469,169,000 (bilioni 223.47).

Mheshimiwa Spika, Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali: Katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida – Sh. 80,831,672,000 (bilioni 80.83). Kati ya hizo mishahara sh. 4,434,410,000 (bilioni 4.43) na matumizi mengineyo sh. 76,397,262,000 (bilioni 76.40).

(b) Miradi ya Maendeleo – Sh. 4,755,547,000 (bilioni 4.76) Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani –Sh. 400,000,000 (bilioni 0.40).

(ii) Fedha za Nje -Sh. 4,355,547,000 (bilioni 4.36).

Mheshimiwa Spika, Fungu 22 – Deni la Taifa, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2013/14, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Sh. 3,319,017,772,000 (bilioni 3,319.02). Kati ya hizo mishahara ni sh. 6,311,772,000 (bilioni 6.31) na matumizi mengineyo ni sh. 3,312,706,000,000 (bilioni 3,312.71).

Mheshimiwa Spika, Fungu 21 – Hazina, katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida Sh. 1,378,142,566,000 (bilioni 1,378.14). Kati ya hizo mishahara ni sh. 2,632,424,000 (bilioni 2.63) na matumizi mengineyo sh. 1,375,510,142,000 (bilioni 1,375.51) ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya Idara na Taasisi zilizo chini ya Fungu hili, nyongeza ya mishahara ya Watumishi wa Serikali na matumizi maalum.

(b) Miradi ya maendeleo ni sh. 38,190,162,000 (bilioni 38.19). Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani- Sh. 7,893,000,000 (bilioni 7.89).

(ii) Fedha za Nje- Sh. 30,297,162,000 (bilioni 30.30).

Mheshimiwa Spika, Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu: Katika Fungu hili kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida – Sh. 1,944,790,000 (bilioni 1.94).

(b) Miradi ya Maendeleo, fedha za nje Sh. 399,985,000 (bilioni 0.39).

Mheshimiwa Spika, Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha: Katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Sh. 2,064,424,000 (bilioni 2.06) kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo,

sh. 362,771,000 (bilioni 0.36) ni kwa ajili ya mishahara na sh. 1,701,653,000 (bilioni 1.70) ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Fungu (7) – Ofisi ya Msajili wa Hazina: Katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida – Sh. 38,088,142,000 (bilioni 38.08). Kati ya hizo sh. 303,192,000 (bilioni 0.30) ni kwa ajili ya mishahara na sh. 37,784,950,000 (bilioni 37.78) ni matumizi mengineyo.

(b) Miradi ya Maendeleo – Sh. 1,665,300,000 (bilioni 1.67). Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani –Sh. 600,000,000 (bilioni 0.60).

(ii) Fedha za Nje -Sh. 1,065,300,000 (bilioni 1.07).

Mheshimiwa Spika, fungu 45- Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi: Katika fungu hili kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida sh. 57,406,414,000 (bilioni 57.40). Kati ya hizo mishahara ni sh. 6,692,935,000 (bilioni 6.69) na matumizi mengineyo sh. 50,713,479,000 (bilioni 50.71).

(b) Miradi ya maendeleo sh. 21,449,100,000 (bilioni 21.45). Kati ya hizo:

(i) Fedha za ndani sh. 15,250,000,000 (bilioni 15.25).

(ii) Fedha za nje sh. 6,199,100,000 (bilioni 6.20).

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara *(www.mof.go.tz).*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2013/2014: Fungu 50 – Wizara ya Fedha, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 – Deni la Taifa, Fungu 23 – Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 10 -Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi na Fungu 07-Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara ilikutana na Wizara ya Fedha kwa nyakati tofauti na kupokea maelezo ya muhtasari wa Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014; pamoja na kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo na mafungu yake kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, aidha, Waziri wa Fedha alitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa Fedha 2012/2013, changamoto za utekelezaji wa kipindi cha mwaka 2012/2013; na malengo na maeneo ya vipaumbele pamoja na makadirio ya Mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Majukumu ya

Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013; Kamati inaipongeza Wizara ya Fedha kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa Mwaka huu wa Fedha ili iweze kufikia malengo yake.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati imeendelea kutoa maoni, ushauri na maelekezo ambayo Wizara ya Fedha imeendelea kuyazingatia katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ambayo ni; kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla; kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje pamoja na matumizi ya Serikali; kufuatilia mipango ya kupunguza umaskini; kusimamia deni la Taifa; upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya miradi ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi; kusimamia Sheria, Kanuni na taratibu za uhasibu, ukaguzi wa ndani wa Serikali, ununuzi wa umma na usimamizi wa mali za Serikali pamoja na kushirikiana na Tume ya Mipango katika kutekeleza mipango ya maendeleo iliyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika Kipindi cha mwaka 2012/2013, bado Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Matumizi makubwa ya Serikali pamoja na kuwepo kwa mahitaji makubwa ya Serikali nje ya Bajeti;

(ii) Kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma sambamba na kuongeza mapato ya Serikali;

(iii) Kuongezeka kwa malimbikizo ya madeni ya ndani katika mafungu mbalimbali ambayo yameshindwa kuingizwa kwenye viwango vya bajeti;

(iv) Kupunguza na kudhibiti Mfumuko wa Bei ili urudi kwenye viwango vya tarakimu moja;

(v) Upungufu katika Sheria ya Msajili wa Hazina na Sheria zilizoanzisha Asasi na Mashirika mbalimbali ya umma;

(vi) Kuwepo kwa mchakato wa muda mrefu wa upatikanaji wa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo hasa mikopo ya kibiashara (*non-conscessional borrowing*);

(vii) Matumizi ya fedha nje ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge;

(viii) Kutozingatiwa ipasavyo kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma; na

(ix) Kutokuwa na Sera ya Mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizi Wizara imejitahidi kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana nazo ikiwa ni pamoja na kupitia mipango na bajeti zake ili kuhakikisha kuwa changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2012/2013, pamoja na changamoto katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2013/2014; Kamati Uchumi, Viwanda na Biashara ilitoa maoni na ushauri juu ya utekelezaji katika maeneo mbalimbali ya kukuza Uchumi, hasa kwenye maeneo yaliyohusu Matumizi na Mapato ya Serikali; Deni la Taifa Misamaha ya Kodi; Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership);* Manunuzi ya Umma; Urasimu uliopo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na vikwazo katika maeneo ya uwekezaji na ufanyaji wa biashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhika na utekelezaji wa baadhi ya ushauri iliyoutoa kwa Wizara na hivyo kuliomba Bunge lako Tukufu lipitishe makadirio ya Wizara hii. Hata hivyo, bado yapo maeneo yanayohitaji kuangaliwa ili kuendeleza ufanisi na tija katika utekelezaji wa kuinua uchumi wa nchi pamoja na nidhamu ya matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sekta ya fedha imeendelea kuimarika kufuatia usimamizi thabiti wa Benki Kuu na hivyo

kuwa na jumla ya benki na taasisi za fedha 51 zenye matawi 559 nchini kote. Rasilimali katika sekta ya mabenki imeendelea kukua na kufikia kiasi cha trilioni 17.9 mwezi Machi 2013 kutoka trilioni 14.7 mwezi Machi 2012, hii inaonesha kuwa mabenki yote nchini yana mitaji ya kutosha (*capital adequate ratio*) ni salama na yanaweza kuhimili misukosuko ya kifedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongezeka kwa idadi ya benki hapa nchini, huduma za kifedha hazijaweza kuwafikia wananchi wa kawaida wakiwemo wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo. Mfumo wa kibenki tulionao unalenga zaidi kuhudumia wafanyabiashara wakubwa, makampuni makubwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, mabenki na taasisi nyingi za fedha zimeendelea kutoa huduma za kibenki na kifedha mijini na hivyo kuwafanya Watanzania wengi ambao wanaishi vijijini kutofikiwa na huduma hizo kwa urahisi, hali ambayo inaufanya uchumi wetu kuwa '*cash based*'. Tafiti zinaonyesha ni asilimia 8 tu ya Watanzania kati ya 100 wanatumia huduma za kibenki na asilimia nne ya watanzania hutumia huduma za asasi ndogondogo za fedha *(MFIs)*.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mwaka 1998 Serikali iliruhusu kuwepo kwa Benki za Wananchi hatua hiyo ilipelekea kuanzishwa kwa benki za wananchi za Mufindi, Mwanga, Mbinga na kadhalika na hadi sasa kuna benki za aina hiyo 11. Benki za wananchi, pamoja na uchache wake zimeweza kutoa mchango mkubwa katika kutoa huduma za kibenki kwa Watanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, aidha *SACCOS* ambazo zilikuwa ni mkombozi wa watu wa vijijini, zimedumaa au kufilisika kutokana na kukosekana kwa usimamizi thabiti kama yalivyo mabenki; hali inayopelekea kuwepo kwa uzalishaji duni katika kilimo - wakulima (kukosekana mitaji), wajasiriamali wadogo kushindwa kukuza biashara zao, kuwepo kwa huduma za kifedha haramu kama *DECI*, wakulima kuuza mazao yako

kwa bei ya chini kwa wakopeshaji binafsi na pia hali ya uwekaji akiba Kitaifa kuwa chini ya kiwango cha *Sub Saharan Africa* cha asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia haya, Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(a) Kuwepo na sheria ya huduma za kifedha kwa watu wa kipato cha chini (*The Microfinance Act).* Asasi nyingi zinazotoa huduma za kifedha kwa watu wa chini hazijasajiliwa na kupewa leseni ya kutoa huduma za kifedha. Asasi hizo zimesajiliwa kwa sheria mbalimbali zikiwepo Sheria ya *NGO's* (2002), Sheria ya Makampuni (2002), *RITA* na kadhalika. Pamoja na usajili huo lakini hazina leseni ya kutoa huduma za kifedha.

(b) Benki Kuu iandae taratibu na kanuni maalum za kusimamia benki za wananchi kama ilivyo kwenye nchi nyingine zenye benki za aina hiyo. Benki nyingi za Wananchi zinatoa huduma za kifedha vijijini tofauti na Mabenki makubwa ya Kitaifa au Kimataifa.

(c) Serikali ianzishe Sheria ya *SACCOS* sambamba na uanzishwaji wa mamlaka itakayosimamia *SACCOS* hizo kama ilivyo kwa nchi ya Kenya. Tanzania haina sheria ya *SACCOS* au *Financial Cooperatives*, kwa sasa sheria inayotumika ni ile ya Ushirika. *SACCOS* ni asasi za kifedha hivyo zina kanuni na unyeti tofauti na ushirika wa aina nyingine.

(d) Serikali isaidie kurasimisha asasi zisizo rasmi. Kumekuwepo na huduma za akiba na mikopo zinazotolewa na asasi zisizo rasmi kama vile Upatu/vibati (*Rotating and Savings Associations-ROSCAS*), Vikundi vya akiba na mikopo *(Accumulated Savings and Credit Associations-ASCAS), VICOBA* na Vyama vya Kufa na Kuzikana. Asasi hizo zimekuwa maarufu sana hapa nchini na zinatoa fursa ya kujenga tasnia endelevu ya fedha lakini havijapewa uzito unaostahili.

(e) Serikali ianzishe Sera ya Maendeleo ya Huduma za Kibenki *(Banking Sector Development Policy)* ili

kujenga mfumo wa huduma za kibenki unaolingana na hatua ya maendeleo na mazingira ya nchi husika pamoja na kutoa huduma ya kibenki kulingana na sekta inayohudumia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/ 2008 - 2012/2013, takwimu zinaonesha kuwa, kiasi cha asilimia 3.1 ya Pato la Taifa lilitolewa kwenye mapato ya Serikali yakiwa kama misamaha ya kodi kwenye *VAT* na Ushuru wa Forodha. Kamati inaona bado kiwango cha misamaha ya kodi kipo juu kwa kiasi kikubwa na hivyo vinaathiri ujazo wa mapato yatokanayo na kodi. Mfano takribani ya asilimia 64 ya wastani wa kodi zote zilizosamehewa katika kipindi cha 2008/2009 - 2011/2012 zilikuwa ni misamaha ya *VAT*, kupitia jedwali la Tatu la Sheria ya *VAT* ambalo hapo awali mwaka 1997, wakati linaanzishwa lilikuwa na vitu vitano tu na sasa lina vitu 27.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kupitia upya Sheria ya *VAT* na kuondoa nusu ya misamaha ya kodi, litapunguza misamaha kwa asilimia 33 na hivyo kuweza kuchangia zaidi ya asilimia sita kwenye Pato la Taifa. Aidha, Serikali iendelee na mazungumzo na Makampuni ya Madini ili kuweza kutoza kodi za mafuta na ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kusimamia vizuri utekelezaji wa Miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la *Millenium Challenge Corporation (MCC)*. Pamoja na changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji, kukamilika kwa miradi hii kwa wakati kama vile Miradi ya barabara, Miradi ya Umeme na Miradi ya Upanuzi wa Mtambo wa Maji Ruvu-Chini itasaidia kuleta maendeleo haraka kwenye maeneo husika na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati inatoa angalizo kuwa, pamoja ya kwamba *MCC* iliamua kuikubalia Serikali ya Tanzania kuanza kuandaa Mpango wa Pili wa Miradi ya *MCC*, upo upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Miradi ya *MCC* hasa ile ya upande wa Miradi

ya ujenzi wa barabara. Serikali iyafanyie tathmini na kurekebisha upungufu huo ili awamu hii ya pili ikamilike kwa wakati kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuipongeza Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (*Gaming Board of Tanzania*) kwa kuweza kutekeleza majukumu na hivyo kuchangia maendeleo ya nchi kiuchumi kupitia kodi inayokusanywa kutokana na michezo ya kubahatisha nchini.

Mheshimiwa Spika, Bodi hii ilianza kuchangia mapato Serikalini hata kabla ya kutungwa kwa Sheria ya Fedha inayohitaji Taasisi za Umma zichangie Serikalini asilimia 10 ya mapato yake. Aidha, takwimu zinaonyesha kuwa kodi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, mathalani, mwaka 2006/2007 makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 2.83, mwaka 2007/08 yalikuwa bilioni 3.9 na kwa kipindi cha kufikia Juni 2012/2013 makusanyo yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 11.24.

Mheshimiwa Spika, hii imetokana na utaratibu mzuri wa bodi iliyojiwekea katika ukusanyaji wa mapato pamoja na kufunga mfumo wa mtandao wa kieletroniki katika maeneo ya michezo ambao unaratibu mzunguko wa fedha na hivyo kupunguza tatizo la udanganyifu. Kamati inashauri kuwa fedha zinazopatikana kwenye michezo ya kubahatisha zitengenezewe Mfuko maalum ambao utatumika kuhudumia jamaii katika sekta ya elimu au afya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa Serikali inakopa ndani na nje ya nchi ili kugharamia miradi ya maendeleo ambayo ina mahitaji makubwa ya fedha ukilinganisha na mapato ya ndani. Malipo kwenye Deni la Taifa ambalo linahusisha mikopo ya nje na mikopo ya ndani kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka yalifikia shilingi bilioni 1146.41, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 29.

Mheshimiwa Spika, angalizo la Kamati ni kwamba, ongezeko la Deni la Taifa haliendani na kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu pamoja na ukusanyaji wa mapato yetu.

Uchumi wa nchi yetu (*GDP growth rate*) tangu 2008/2009 hadi 2011/2012 umeongezeka kwa wastani wa asilimia 6.5 tu, wakati Deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 15.4.

Mheshimiwa Spika, hali hii isipodhibitiwa upo uwezekano mkubwa wa Deni hilo kutokuwa himilivu kwa siku za usoni. Ni muhimu Serikali ikachukua hatua ili kudhibiti kasi kubwa ya madeni yanayotokana na dhamana za Serikali, kuwa na sera nzuri za kibajeti ikiwemo kupunguza mikopo ya kibajeti, pamoja na kuendelea kupanua wigo wa makusanyo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo kubwa la matumizi makubwa kwa upande wa Serikali pamoja na matumizi nje ya bajeti iliyopangwa na kuidhinishwa na Bunge kwenye mafungu ya kila Wizara. Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kudhibiti na kusimamia matumizi ya Serikali pamoja na nidhamu ya matumizi kadri yalivyoidhinishwa kwenye vifungu husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kurekebisha haya, Serikali inahitajika kuendelea kuimarisha sera za mapato na matumizi na maboresho mbalimbali katika sekta ya Umma; kuendelea kuangalia eneo la sera na uendeshaji wa taratibu za kukusanya kodi pamoja na kupanua wigo wa ukusanyaji wa kodi; kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara; kuimarisha uzalishaji na ubora wa bidhaa za ndani na kuweza kuuza nje ya nchi ili kuongeza fedha za kigeni; pamoja na kupitia upya utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi kwa madhumuni ya kushusha misamaha hiyo angalau iwe asilimia moja ya Pato la Taifa kama Kamati ilivyopendekeza huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, Sekta isiyo rasmi ni sekta ngumu kutozwa kodi kwa kuwa haina mfumo rasmi wa ufanyaji wa biashara pamoja na kutunza kumbukumbu za biashara zake. Katika utafiti uliofanywa kwenye nchi 110 duniani, Tanzania inakadiriwa kuwa na sekta isiyo rasmi kiasi cha asilimia 60.2 ya Pato la Taifa, ikiwa ni kiwango kikubwa kuliko kwa nchi

zote za Afrika isipokuwa Zimbabwe, kwa upande wa Kenya ni asilimia 34.3, Malawi ni asilimia 40.3 na Zambia ni asilimia 48.9.

Mheshimiwa Spika, hii ni changamoto kubwa kwa Serikali katika kuhakikisha inatafuta namna au mfumo utakaotumika kuwezesha sekta isiyo rasmi kulipa kodi na hivyo kuongeza mapato makubwa kwa Serikali. Utoaji wa vitambulisho vya Taifa utawezesha kudhibiti shughuli za kila mlipa kodi katika biashara zake na hivyo kuweza kupeleka *TRA return* ya kodi ya mapato kama ilivyo kwa nchi za Kenya na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011, Bunge lilipitisha Azimio la kuongeza muda wa uhai wa mpito wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma *(CHC)* kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hadi 30 Juni, 2014.

Mheshimiwa Spika, lengo la Azimio hilo lilikuwa kutoa fursa kwa *CHC* kukamilisha taratibu za kiutendaji na za kisheria pamoja na kuhamisha kazi zitazokuwa zimebaki kwenda Ofisi ya Msajili wa Hazina pindi kipindi cha mpito kitakapofikia ukomo pamoja na kukamilisha marekebisho ya kimuundo na kisheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo itakabidhiwa majukumu ya *CHC*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio iliyoyapata *CHC* katika utendaji wake bado inakabiliwa na changamoto kubwa kuweza kukamilisha kazi zake kulingana na muda uliopo. Baadhi ya changamoto kubwa zinazoikabili *CHC* ni uwepo wa mashauri 330 dhidi ya Shirika kwenye Mahakama mbalimbali nchini; ukusanyaji sugu wa madeni ya wateja sugu wa iliyokuwa *NBC* ambayo Shirika limerithi; uwezo wa Shirika kuwa mdogo kwa upande wa rasilimali watu, fedha na mfumo wa utendaji ukilinganisha na majukumu waliyopewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa angalizo kuwa, Serikali ihakikishe inaweka mipango na mikakati kuhakikisha kuwa, shughuli zilizobaki za ubinafsishaji zinakamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2014 kama ilivyotarajia. Pia, Serikali lazima

iandae utaratibu wa utekelezaji wa shughuli zitakazobaki baada ya uhai wa *CHC* kufikia kikomo. Maamuzi ya suala hili yanahitaji umakini mkubwa ili kuhakikisha kuwa Serikali haikosi mapato yake toka kwa makampuni yaliyobinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo kubwa la ukwepaji kodi linalofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu wanaoshirikiana na watendaji wa *TRA* pamoja na watendaji wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, udanganyifu huu unatumia mbinu mbalimbali zisizo za halali ili kuhakikisha wanalipa kodi pungufu kuliko wanavyostahili au kutolipa kabisa; mbinu hizi zinahusisha kuficha mauzo halisi, kutotoa risiti kwa mauzo, kuwa na vitabu zaidi ya kimoja, kuwa na mihuri bandia, kudanganya aina ya bidhaa inayoingizwa nchini na kuingiza sokoni bidhaa zilizokusudiwa kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni hivi karibuni *TRA* ilifanya ukaguzi wa dharura na kugundua zaidi ya makontena mengi yenye bidhaa mbalimbali ambayo yanasemekana hayajalipiwa ushuru halali kulingana na bidhaa iliyopo ndani au yamedanganya aina ya bidhaa iliyomo ndani na hivyo kulipa ushuru mdogo isivyo halali.

Mheshimiwa Spika, ukwepaji wa ulipaji wa Mapato ya Nchi ni Uhujumu Uchumi na unawanyonya na kutoa kero kubwa kwa wafanyabiashara waadilifu na pia wananchi. Bunge limekuwa likijadili kila siku na kuibana Serikali wapi itapata mapato yake ili iweze kusaidia kugharamikia kutoa huduma kwa wananchi wa Tanzania, kumbe kuna watu wachache (wafanyabiashara, mawakala wa mizigo na watendaji) wasio na huruma na nchi hii, wanaendelea kuikosesha mapato Serikali bila woga na hivyo kuathiri uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vitendo kama hivi vya ukwepaji wa kulipa kodi ni dhahiri vinahusisha mtiririko mkubwa *(chain)* wa wafanyabiashara, Mawakala wa kutoa mizigo na

watendaji wa Serikali wasio waaminifu. Hapa Kamati inaiuliza Serikali ipo wapi, ilikuwa wapi na inafanya nini mpaka sasa?

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri suala kama hili likitokea kwa nchi kama ya China mnajua nini kitakachofuata kwa wahusika na mali zao zitafanywa nini. Tumekuwa tukiimba wimbo bora kila siku wa uadilifu na utawala bora, haya leo yametokea ni vema Serikali ikatoa kauli juu ya suala hili na hatua stahili ilizozichukua. Kamati inaiagiza Serikali ifanye uchunguzi wa kina juu ya suala hili na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya watakaobainika na ukwepaji wa kodi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, sasa imefikia wakati mashirika yaliyobinafsishwa yaorodheshwe kwenye soko la mitaji ili kuongeza ufanisi wa kodi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kamati inaendelea kuikumbusha Wizara ya Fedha kuwa yenyewe ndio kitovu cha Wizara zote. Kushindwa kuwajibika vyema kwa Wizara hii, mwisho wa siku kutapelekea kushindwa kufikia malengo kwa Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kunisaidia kuiongoza Kamati; Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Waziri wa Fedha na Manaibu wake Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum. Naomba niwashukuru Watendaji Wakuu wa Wizara, Benki Kuu, Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Fedha kwa kuandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya

Bunge hili Tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, Mwenyekiti; Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Margaret Agness Mkanga, Mjumbe; Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mjumbe; Mheshimiwa Ester Lukago Minza Midimu, Mjumbe; Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mjumbe; Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mjumbe; Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mjumbe na Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa David Zakaria Kafulila, Mjumbe; Mheshimiwa Shawana Bukhet Hassan, Mjumbe; Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mjumbe; Mheshimiwa Vicky Pascal Kamata, Mjumbe; Mheshimiwa Naomi Ami Mwakyoma Kaihula, Mjumbe; Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mjumbe; Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mjumbe; Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mjumbe; Mheshimiwa Josephine Jonson Genzabuke, Mjumbe; Mheshimiwa *Engineer* Habib Juma Mnyaa, Mjumbe; Mheshimiwa Mohamed Hamis Misanga, Mjumbe;

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah; Katibu wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Fedha, kama alivyowasilisha mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusiana na Wizara ya Fedha, naomba kuwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara husika kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Dira kuu ya Wizara ya fedha ni kuhakikisha kuwa uchumi unakua kwa kiwango cha juu na matokeo yake kuwanufaisha wananchi wote na kuhakikisha usimamizi thabiti na uwajibikaji wa fedha za umma. Kambi Rasmi ya Upinzani inaikumbusha tena Wizara ya Fedha katika kutimiza wajibu wake ikumbuke kwamba "Maslahi ya Taifa ni zaidi ya Vyama vya Siasa, mahali tunapotoka au dini tunazoziamini. Maslahi ya Taifa ni kwa ajili ya Watazania na hasa Watanzania milioni 30 *(The Bottom 30M)* ambao bado wanaishi katika ufukara mkubwa sana wakikosa huduma muhimu za jamii na wanaoishi vijijini ambapo hakuna umeme, barabara hazipitiki na wanahangaika kutwa kutafuta maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya Taifa sio faida ya wachache wenye kuishi mijini au wanasiasa wanaotafuta ushawishi kwa umma bila kujali matakwa ya umma. Watanzania wanyonge wa vijijini wanajua maslahi yao ni nini". Hivyo, ni vema Wizara ya Fedha itimize majukumu yake kwa kuzingatia maslahi ya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza majukumu hayo Wizara imegawanyika katika idara mbalimbali zenye mafungu yafuatayo: –

- Fungu 50 - Wizara ya Fedha.
- Fungu 21 - Hazina.
- Fungu 22 - Deni la Taifa.
- Fungu 23 - Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.

- Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha.

- Fungu 13 - Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi.

- Fungu jipya ni 7 - Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, tija katika ukuaji wa uchumi ndicho kipimajoto cha afya ya uchumi wa nchi, hivyo uelewa bora wa hali ya uchumi wa Tanzania utaonekana ni kwa vipi uchumi au rasilimali za nchi zinavyotumika katika kuwanufaisha Watanzania na uzalishaji wa ajira mpya katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Fedha kutafakari kwa kina ni kwa nini ukuaji wa uchumi wa Tanzania haupunguzi umaskini. Nchi nyingine katika bara la Afrika zenye kasi ya ukuaji wa uchumi kama nchi yetu, Ethiopia na Uganda, wameweza kuwaondoa zaidi ya asilimia 30 ya wananchi wao katika dimbwi la umaskini katika kipindi cha muongo mmoja (2000 – 2010). Wizara ya Fedha kama msimamizi mkuu wa sera za uchumi imeshindwa kabisa kutafsiri ukuaji wa uchumi wa Tanzania kutoka takwimu kwenda kwenye maisha ya watu wa chini.

Mheshimiwa Spika, hoja za Kambi ya Rasmi ya Upinzani ambao hazijatekelezwa; kwa mwaka wa fedha 2012/2013 tuliitaka Serikali kufanya yafuatayo ili kuongeza wigo wa utendaji na udhibiti wa mianya ya upotevu wa mapato ya Taifa na pia kutoa mwelekeo mpya wa kuongeza ajira:-

(i) Tulisema kwamba *TRA* wanao uwezo wa kukusanya mpaka shilingi trilioni moja kwa Mwezi iwapo tutadhibiti misamaha ya kodi, tutakusanya kodi stahili katika Sekta ya Madini na tutasimama kidete kuzuia ukwepaji kodi wa Makampuni ya Kimataifa. Wizara haijatoa maelezo kuhusu utekelezaji wa ushauri huu.

(ii) Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Mamlaka ya

Manunuzi ya Umma (*PPRA)* kufanya uchunguzi wa kina kuhusu manunuzi ya mafuta ya kuzalisha Umeme, Wizara ndio yenye kusimamia uchumi wa nchi kwa ujumla ituletee Bungeni Taarifa ya Uchunguzi utakaofanywa na *PPRA* kuhusu manunuzi shilingi 1.4 bilioni kila siku ya mafuta kuendesha mitambo ya kuzalisha Umeme. Kwa masikitiko makubwa ukaguzi maalum bado haujafanyika.

(iii) Wizi kwenye mabenki ni moja ya sifa mbaya sana ya mfumo wetu wa fedha na hivyo kusababisha Benki kuweka riba kubwa sana ili kufidia *risk* kama hizi za watu 'kupiga' amana za wateja kwenye mabenki. Kambi Rasmi ya upinzani iliitaka Wizara ya Fedha kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha haramu kudhibiti wizi kwenye Benki za hapa nchini.

Fedha bado zinaibiwa na hivyo kufanya riba kuendelea kupanda na wananchi kushindwa kufanya biashara yenye tija kwa maendeleo yao. Tunataka majibu kuhusu suala hili ambalo linaharibu sifa ya sekta yetu ya Benki.

(iv) Taifa linavyoibiwa kupitia kesi mbalimbali ambazo Serikali imeshtaki au kushtakiwa kwenye Mahakama za Kimataifa. Tulipenda kufahamu ni kwa nini mpango wa kumaliza kesi hii nje ya Mahakama hautekelezwi na vile vile mpango wa kugeuza Mtambo wa kufua umeme wa *IPTL* kuwa wa gesi kwa nini hautekelezwi?

(v) Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata majibu kuhusu fedha zilizoko kwenye *Escrow* Akaunti, Benki Kuu za *IPTL* (Tegeta *escrow*) zimefikia kiasi gani mpaka sasa na usalama wa fedha hizo ukoje?

(vi) Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Serikali kuunda Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta Ndogo ya Fedha *(Tanzania Microfinance Regulatory Authority).* Kwani mamlaka italinda Haki za wanyonge dhidi ya *loan sharks* na wajibu wa wanyonge wenye kuchukua mikopo.

(vii) Katika kuleta uwazi na uwajibikaji wa Mifuko

ya Hifadhi za Jamii, Kambi Rasmi ya Upinzani, ilitaka kama ilivyo kwa Mabenki, taarifa za mahesabu za robo mwaka za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ziwe zinatangazwa kwenye magazeti yanayosomwa zaidi nchini ili wananchi na hasa wanachama wa Mifuko waone namna Mifuko yao inavyofanya kazi. Hili nalo bado halijafanyika.

(viii) "Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilipendekeza kwa Mifuko ya *PSPF* na *PPF* kuangalia namna ya kuwekeza katika maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi na hivyo kuzalisha ajira na kupata wanachama zaidi. Maeneo kama uwekezaji kwenye Bandari na Reli yanapaswa kuangaliwa.

(ix) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia ilipendekeza kwamba fao la Elimu ambalo Mfuko wa *PPF* unatoa kwanza Fao hili liwe fao la lazima kwa Mifuko yote nchini, lakini pia lipanuliwe hadi kufikia elimu ya Chuo Kikuu.

(x) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni bado ilisisitiza kwamba Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii ihamishiwe Wizara ya Kazi na Ajira kama Wizara inayohusika na *social security*.

(xi) Aidha, Mifuko ipunguzwe na kubakia na Mifuko miwili tu, mmoja wa wafanyakazi walio katika sekta binafsi na sekta isiyo rasmi na mwingine kwa wafanyakazi wa sekta ya umma. Kwamba Mifuko ya *NSSF* na *PPF* iunganishwe kuwa Mfuko mmoja kwa ajili ya sekta binafsi na sekta isiyo rasmi na Mifuko ya *PSPF, LAPF* na *GEPF* iunganishwe kuwa Mfuko mmoja kwa ajili ya kushughulika na wafanyakazi wa Sekta ya Umma".

(xii) Kambi ya Upinzani ilitaka kupata maelezo ya kina ni kwa nini Msajili wa Hazina anaendelea kuwa mjumbe wa vikao vya Bodi za Mashirika ya Umma kinyume na sheria?

(xiii) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilitaka kupata maelezo ya Serikali kuhusu uuzwaji wa hisa za Shirika la UDA umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, Fungu 50 - Wizara ya Fedha na taasisi zake; Benki Kuu ya Tanzania na udhibiti wa fedha na sera ya fedha. Benki Kuu ya Tanzania ni chombo cha Kitaifa kinachosimamia masuala ya kibenki na kifedha. Sheria ya Benki ya Tanzania ilifanyiwa marejeo mwaka 2006 na kuipa benki hii jukumu la kusimamia Sera ya Fedha nchini *(monetary policy).*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Benki Kuu imeipa uhuru Benki kuendesha shughuli zake bila kuingiliwa na Serikali. Lengo la msingi la Benki Kuu ya Tanzania ni kudhibiti mfumuko wa bei, kwa sababu lengo hili ndilo litakalohakikisha kuwepo kwa utengamavu wa uchumi mpana utakaosaidia ukuaji endelevu wa uchumi. Aidha, Benki Kuu ya Taifa lolote ndio taasisi pekee yenye takwimu zote nyeti na za uhakika zinazohusu uchumi wa Taifa hilo.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya ukaguzi wa hesabu za *BOT* ya mwaka 2011/2012; Mnamo mwezi April 2013 Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* ilitoa taarifa yake ya ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2011/2012, miongoni mwa mambo ambayo yaliweza kuainishwa katika ripoti hiyo ni pamoja na taarifa ambayo ni ya kustua kwani Benki Kuu imepata hasara kubwa katika mwaka huo wa fedha ya kiasi cha shilingi bilioni 52.431 ikilinganisha na mwaka uliotangulia 2010/2011 ambao *BOT* walipata faida kubwa ya kiasi cha shilingi bilioni 727.793.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika taarifa hiyo ya ukaguzi ya *BOT* yapo mambo mbalimbali ambayo yaliainishwa kama vile uwepo wa fedha za *EPA*, Mikopo mikubwa ya wakurugenzi na wafanyakazi wa Benki Kuu, fedha za *IPTL* katika *Tegeta Escrow account* ya *BOT*, kufungwa/kufilisiwa kwa kampuni ya ubia ya Mwananchi *Company Limited* na mengineyo mengi.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kupata majibu ya kina kuhusiana na masuala yafuatayo yaliyoibuliwa na ripoti hiyo ya ukaguzi:-

(i) Ni utaratibu gani unatumika katika

kuwakopesha wafanyakazi fedha kwa ajili ya nyumba na kununulia magari binafsi na kukokotoa riba ya mikopo kwa wafanyakazi na viongozi wakuu wa *BOT* kwani mpaka tarehe 30 Juni, 2012 walikuwa tayari wamejikopesha shilingi bilioni 55.668, ikilinganishwa na shilingi bilioni 38.965 mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunataka kujua kama fedha hizi ni tofauti na kile kinachoitwa *staff Housing Fund* ambao ni mkopo kwa wafanyakazi unaotokana na faida ya kila mwaka inayopatikana kutokana na shughuli mbalimbali za *BOT*, 2012 Mfuko ulikuwa na kiasi cha shilingi bilioni 34.170 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyakazi wa *BOT* kwa ajili ya nyumba.

(ii) Mfuko wa Elimu wa Mwalimu Nyerere (Mwalimu Nyerere *Scholarship Fund*), mnamo mwaka 2009, *BOT* ilianzisha Mfuko huo kwa ajili ya kuwapa udhamini wasichana kusoma shahada ya kwanza kwa wale ambao watafaulu vizuri masomo ya Sayansi na Hisabati na hadi mwezi Juni 2011 Mfuko ulikuwa na kiasi cha shilingi bilioni 1.715. Aidha, katika mwaka wa fedha 2012, mpaka tarehe 30 Juni, Mfuko ulikuwa na shilingi sifuri. Je, ni utaratibu gani huwa unatumika katika kupata fedha hizi na ni wanafunzi wangapi mpaka mwaka huu wa fedha wamesomeshwa na Mfuko huu na wanasoma vyuo gani?

(iii) Akaunti ya malipo ya nje *(EPA)*, Mpaka tarehe 30.06. 2012 kwa mujibu wa ripoti hiyo akaunti hii ilikuwa na kiasi cha shilingi bilioni 205.743, jeb fedha hizi zina usalama gani mpaka sasa na je, hazitachotwa kama ilivyofanyika mwaka 2005?

Mheshimiwa Spika, aidha, mpaka sasa ni akina nani (orodha ya majina ya watu waliorejesha fedha) na ni kiasi gani cha fedha kimerejeshwa kutokana na ufisadi wa shilingi bilioni 133 uliofanyika katika kipindi cha mwaka 2005? Maamuzi ya Serikali ilikuwa ni kuondoa kabisa akaunti hii ya *EPA* kutoka Benki Kuu. Kwa nini bado akaunti hii ipo Benki Kuu?

(iv) Kwa mujibu wa ripoti ya ukaguzi wa hesabu za *BOT,* katika mwaka wa fedha 2011/2012, ni kuwa *BOT* ilipata hasara ya shilingi bilioni 52.431 ikilinganishwa na faida ya shilingi bilioni 727.793 iliyopatikana mwaka 2011. Tunataka majibu ya kina kuhusiana na hasara hii kwani haiwezekani taasisi nyeti kama hii ipate hasara na Taifa lisiweze kupewa taarifa za kina kuhusiana na chanzo cha hasara hii na ni hatua gani zimechukuliwa mpaka sasa katika kukabiliana na hasara hii.

Mheshimiwa Spika, dhamana za Serikali kwa Mashirika na Taasisi; katika taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2012, Serikali inakiri na kuafiki mapendekezo ya ukaguzi juu ya kutokuwa na viwango vya dhamana kinyume na Sheria ya Mikopo ya Dhamana na Ruzuku, sheria ya mwaka 1974 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huo wa usimamizi wa dhamana za Serikali uamuzi wa kusimamisha utoaji wa dhamana kwa Wizara ambayo imepelekea kuwepo kwa athari katika uendelevu wa madeni, pia ni vipi Serikali inatoa uhakiki wa utendaji kwa Mifuko ya Hifadhi za Jamii ambayo ndio itakuwa imeaathirika na usimamizi huu mbovu wa dhamana za Serikali?

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF)*; taarifa ya *POAC* ya Aprili, 2011 ilionesha *PSPF* ilikuwa ikilipa mafao ya pensheni kwa watumishi waliostaafu kabla ya mwaka 1999 kwa maelewano na Serikali kuwa Serikali itarejesha kiasi kilichotumiwa na *PSPF*. Lakini hadi kufikia tarehe 30/06/2010, jumla ya Sh. 716.6 bilioni zilikwisha kutumiwa na *PSPF* kulipa wastaafu na kiasi hicho kilipaswa kurejeshwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Kamati ilionesha kuwa, Serikali ilikiri kudaiwa na kuahidi kuanza kulipa. Kisha wakalipa shilingi bilioni 30, kumbe baadaye hawakulipa tena na uchambuzi wa *acturials* umeonesha ukubwa wa deni karibu mara mbili ya ilivyokuwa mwaka 2010. Kutokana na barua ya Wizara kwenda kwa Mkurugenzi Mkuu wa *PSPF* ya

tarehe 25 Machi, 2011, Wizara ilisema itairejeshea fedha *PSPF* ndani ya miaka 10 kwa kutenga kwenye bajeti kiasi cha Sh. 71 bilioni kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali iligundua kuwa: Kwanza, Wizara ya fedha haikutenga kiasi cha Sh. 71 bilioni katika bajeti ya mwaka 2011/2012. Kiasi kilichorejeshwa *PSPF* cha Sh. 20 bilioni ndani ya mwaka unaokaguliwa sasa kimelipwa kutoka Mfuko wa Tahadhari *(Contingency Fund)* badala ya kutoka kwenye mafungu yaliyotengwa kila mwaka kama ilivyokusudiwa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Spika, pili, kiasi kilichorejeshwa *PSPF* mwaka 2011/2012 cha Sh. 20 bilioni kilikuwa kidogo kuliko kiasi kilichokusudiwa cha Sh. 71 bilioni (asilimia 28 tu ya kiasi kilichokubaliwa kwa mwaka cha Sh. 71 bilioni) hali ambayo itaathiri uwezo wa kifedha wa *PSPF*.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema katika hotuba yetu ya Ujenzi kwamba, Serikali ya CCM hawatembei kwenye maneno yao, kwani wanatoa ahadi lakini wanashindwa kutimiza. Hivyo basi, Kambi Rasmi yya Upinzani inasema sasa ni muda muafaka wa CHADEMA kupata ridhaa za wananchi kuongoza nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati akifunga Wiki ya Hifadhi Mei 17, 2013 kwenye Uwanja wa Nyerere *Square* Mjini Dodoma, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alisema: "Rasilimali ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeongezeka kutoka Sh. trilioni 3.7 mwaka 2010 na kufikia trilioni 5.3 mwezi Desemba, 2012. tathmini hii imefuta dhana ya watu wachache waliokuwa wanaeneza uvumi kuwa baadhi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ipo katika hali mbaya kifedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma (PSPF) unaidai Serikali mabilioni ya fedha, jambo ambalo Rais Kikwete amesema ni kweli na kufafanua historia ya deni hilo akisema kuwa lilizaliwa Julai,

mwaka 1999 wakati watumishi wote wa Serikali walipoingizwa katika Mfuko wa Hifadhi ambako watumishi hao walitakiwa kulipiwa mchango kiasi fulani na Serikali.

Mheshimiwa Spika, aliendelea kusema, awali deni hili halikujulikana. Lakini maadamu limejulikana litalipwa na kwa kuanzia mwakani Serikali italipa kiasi cha sh. bilioni 50 ikiwa ni sehemu ya kulipa deni hilo. Lengo letu ni kuona kuwa hakuna mfanyakazi atakayekosa mafao yake kwa sababu ya Serikali, yaani mwajiri wake. Hatuwezi kufanya kamari na mafao ya wafanyakazi."

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inapenda kulijulisha Bunge kuwa Wizara ya Fedha haikumpa taarifa za kweli Mheshimiwa Rais. Kwanza ahadi ya kisheria ni kulipa shilingi 71 bilioni kila mwaka kutoka kwenye Bajeti kuanzia mwaka 2011/2012 ambapo toka wakati huo zimelipwa shilingi bilioni 30 tu. Hivyo kumpa Rais taarifa za kwamba zimetengwa shilingi bilioni 50 katika bajeti ya mwaka huu bila kuzingatia miadi ya kisheria ya miaka ya nyuma ya shilingi 110 bilioni ni kumchonganisha Rais na wanachama zaidi ya 300,000 wa *PSPF* waliozagaa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Serikali ieleze shilingi bilioni 110 ambazo hazikulipwa miaka miwili iliyopita na shilingi bilioni 70 za mwaka wa fedha 2013/2014 zitalipwa lini? Serikali ikumbuke kuwa fedha hizi sio hisani bali ni malipo halali ya wastaafu ambao wameitumikia nchi yetu kwa uwezo wao wote.

Mheshimiwa Spika, mbali na tatizo hilo la Serikali kukataa kulipa deni inalodaiwa na *PSPF* bado kuna tatizo la msingi la kutokuwepo kwa mtendaji mkuu, kwani aliyepo anakaimu kwa takribani miaka mitatu sasa. Huu ni uzembe ambao unasababisha maamuzi makubwa ya kiutendaji yanashindwa kufanyika. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kumthibitisha au kuendesha mchakato wa kumpata Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, mafao, pensheni, mirathi na

mapunjo; kumekuwepo na malalamiko mengi sana kuhusiana na pensheni kwa wastaafu waliokuwa ni watumishi wa Serikali katika taasisi mbalimbali, pia kucheleweshwa kutolewa kwa fedha za mirathi kwa familia za marehemu ambao walikuwa ni watumishi wa Serikali. Aidha, malalamiko ya mapunjo kwa watumishi wa taasisi mbalimbali kwa hiari yao waliamua kustaafu kutokana na ahadi walizopewa na taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, ubaguzi wa malipo ya pensheni kwa wastaafu katika jeshi la ulinzi, kati ya wale waliostaafu chini ya mwaka 2006 na wale waliostaafu juu ya mwaka 2006. Mfano mzuri ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi mstaafu, Jenerali Mirisho Sarakikya kwa mujibu wa gazeti la Mwananchi analipwa shilingi 50,000 kama pensheni kwa mwezi, hii ni aibu kwa nchi na udhalilishaji kwa makanda wastaafu. Wakati wenye cheo kama chake waliostaafu kuanzia mwaka 2006 kuja juu wanalipwa pensheni ya 80% ya mshahara waliokuwa wanapokea wakiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo, ni kuwa hata wastaafu wa vyeo vya Brigedia na Makanali chini ya mwaka 2006, pensheni yao kwa mwezi umezidiwa na wastaafu wa vyeo vya chini wa kuanzia mwaka 2006 kupanda juu.

Mheshimiwa Spika, suala hili la pensheni hasa kwa wanajeshi linaleta sononeko kubwa kwa wazee wetu ambao walijitolea maisha yao katika kuhakikisha Tanzania inakuwa salama. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kurekebisha haraka iwezekanavyo viwango vya ulipwaji wa pensheni kwa wanajeshi waliostaafu miaka ya 2006 kushuka chini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai ya mapunjo kwa watumishi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliostaafishwa mwaka 2006, waliamua kuunda Kamati ya Kufuatilia Mapunjo yao, Kamati ambayo inaongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Rashid H. Mohamed, Makamu Mwenyekiti wao Ndugu Bathromeo S. Milanzi na Katibu wao Ndugu Hassan A. Hassan ni kwamba hazina imekuwa ikiwapiga chenga wakati madai yao kwa mujibu wa barua ya tarehe 1 Agosti, 2011 yenye

kumb. Na. J/C.60/4/32/74/19, toka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenda kwa Katibu Mkuu wa Hazina iko wazi, nini hasa wanadai wastaafishwa hao wapatao 638 waliokuwa wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri wa Ofisi ya *AG* kwamba, hakuna haja ya kuunda Kamati ndogo ya kuhakiki madai hayo kama ilvyopendekezwa na kikao cha tarehe 28 Desemba, basi wastaafu hao walipwe madai yao kama walivyoomba na mgogoro huu ufungwe."

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali izingatie ushauri uliotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa kuwalipa wazee hawa ambao walifanya kazi kubwa na kwa uadilifu mkubwa katika kulitumikia Taifa lao ila leo wanaendelea kulia kutokana na Serikali kutokulipa mafao yao.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani *(Internal Auditor General);* Bunge lilipitisha sheria inayoitwa *The Local Government Service ACT, 1982* na sheria hii iliunda "Tume ya Usajili katika Serikali za Mitaa" kwa lengo kuu la kuwa ndicho kingekuwa chombo kikuu chenye mamlaka ya kutoa ajira katika ngazi hiyo ya Serikali. Aidha, kwa sasa kuna chombo kingine kinaitwa "Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma" ambacho kinatoa ajira hadi za watendaji katika ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania, hii sheria iliyotungwa na Bunge ya *The Local Government Service Act*, 1982 imefutwa au majukumu yake yameingizwa kwenye Sheria ya *Civil Service Act, 1989?* Kama bado ipo utendaji kazi wa sheria hiyo ukoje?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo hayo, kutokana na ukweli kwamba katika kufanya usimamizi wa fedha za walipa kodi, vyombo vya Serikali vinavyotakiwa kufanya kazi hiyo ni Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa

Ndani *(Internal Auditor General)* na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(Controller and Auditor General).*

Mheshimiwa Spika, hawa wote mmoja hana nguvu kisheria ya kuhamisha watendaji wanaofanya kazi kwa niaba yake, naye ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwani katika Halmashauri mamlaka ya ajira kwa Wakaguzi wa Ndani sio ofisi yake bali wako Ofisi ya TAMISEMI chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hoja hiyo ni kwamba, hata hao Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri wanakuwa ni sehemu ya utawala badala ya kuwa washauri, jambo hili linatengeneza mazingira ya kifisadi yanayofanywa katika katika ngazi hiyo kutokana na mahusiano yanayojengwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani anakosa mamlaka ya kufanya uamisho ila kwa ridhaa ya Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzifanyia marekebisho sheria husika ili Mkaguzi Mkuu wa Ndani awe na mamlaka ya kuwahamisha Wakaguzi wa Ndani kwa kadri atakavyoona inafaa kama ilivyo kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Fungu 22 - Deni la Taifa; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunatambua kuwa nchi nyingi duniani kama sio zote zinakopa ili kuboresha huduma na kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kimaendeleo na hutumia fedha za walipa kodi katika kuendesha shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Deni la Taifa liliongezeka kwa asilimia 38 kutoka Shilingi trilioni 7.6 mwaka 2008 mpaka shilingi trilioni 10.5 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010/2011, deni hilo liliendelea kuongezeka kutoka shilingi trilioni 10.5 na kufikia kiasi cha shilingi trilioni 14.441. Katika mwaka wa fedha 2011/

2012, Deni la Taifa liliendelea kuongezeka kutoka shilingi trilioni 14.441 na kufikia kiasi cha shilingi trilioni 16.975 mwaka uliofuatia.

Mheshimiwa Spika, katika hali isiyokuwa ya kawaida, Deni la Taifa limeongezeka kwa kasi sana na hadi Disemba, 2012 lilikuwa limefikia kiasi cha shilingi trilioni 21.028 kutoka kiasi cha shilingi trilioni 18.258 Disemba, mwaka 2011 na kati ya hizo asilimia 75.97 zilikuwa ni deni la nje.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ina taarifa kwamba takwimu hizi za Deni la Taifa hazihusishi dhamana ambazo Serikali imezitoa kwa Mashirika ya Umma na Kampuni binafsi. Aidha, ni lazima dhamana katika siku za usoni ziwe ni sehemu ya Deni la Taifa maana tumeshuhudia sasa ambapo Kampuni nyingi binafsi zimeshindwa kulipa mikopo iliyodhaminiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mfano ni malipo ya deni lenye thamani ya shilingi bilioni 60 la kukodisha ndege ya *Airbus* kwa Shirika la *ATCL* kutoka kampuni ya *Wallis Traders* ya Lebanon na Deni lililochukuliwa na Kampuni ya Kiwira *Coal and Power limited* ambayo Mbia wake alishindwa kuendesha mradi wa Makaa ya Mawe Kiwira licha ya kudhaminiwa na Serikali Mkopo kutoka kwenye taasisi za Fedha hapa nchini ambapo sasa Serikali imelipa shilingi bilioni 40 katika Bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunatambua kuwa Serikali ina madeni ambayo hayajajumuishwa kwenye deni la Taifa na hiyo inalipelekea Deni la Taifa kuwa kubwa kuliko linalooneshwa kwenye taarifa mbalimbali za Serikali na ile ya *CAG*, kwa mfano kuna madai ya *PSPF* ya sh. 716,600,000,000 kati ya madai ya shilingi trilioni 6.5 ambayo Serikali inadaiwa na imekubali kuyalipa madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna madeni ya Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini na Citi Bank kiasi cha dola 4,129,298.38 na dola 1,460,000 sawa na shilingi bilioni 8.8 kwa ujumla wake ambazo hazijajumlishwa kwenye Deni la Taifa

wakati zitalipwa na Serikali. Aidha, kuna dhamana mbalimbali zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya Idara, Wizara na Mashirika ya Umma zinazofikia shilingi trilioni 1.250. Chanzo ni ripoti ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na uhimilivu wa Deni la Taifa *(Debt sustainability)* kwani tunajua kuwa Mataifa makubwa yanakopa sana na yana uwiano mkubwa wa Deni kwa *GDP* kuliko sisi. Tatizo letu ni namna ambavyo fedha za mikopo zinatumika. Matumizi ya mikopo tunayochukua sio endelevu maana sehemu ya mikopo hiyo hutumika kwa matumizi ya kawaida badala ya matumizi ya uzalishaji au kuongeza uwezo wetu wa kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kukopa kama ambavyo Mataifa mengine hufanya hivyo, kwetu sisi hii ni kasi kubwa mno ukilinganisha na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa sababu ukopaji unategemea uwezo wa kulipa pia.

Mheshimiwa Spika, hii itasababisha mzigo huu wa madeni kubebwa na kizazi cha sasa na kijacho. Ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika Mashariki, Tanzania bado ina viwango vidogo vya mikopo kama sehemu ya Pato la Taifa *(debt/GDP ratio)*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wakati wenzetu wanakopa ili kuongeza uzalishaji (*capital investments*), sisi tunakopa kwa matumizi ya kawaida. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwepo kwa namna bora zaidi ya kuamua kuhusu mikopo ambayo Taifa linaingia ili kuhakikisha inaelekezwa katika uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya CAG ya mwaka 2012, kuna jumla ya shilingi bilioni 619 ambazo zipo kwenye Deni la Taifa, lakini hazina vithibitisho. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameandika “Uhakiki wa mchanganuo wa madeni ya Taifa kama ulivyokuwa tarehe

30 Juni, 2012 ulibaini kuwepo kwa marekebisho ya Deni ya shilingi 619.8 bilioni ambao uongozi haukuweza kutoa maelezo ya kuridhisha" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni imeshtushwa na kuwepo kwa kiwango kikubwa cha deni ambalo halina vielelezo. Tunataka maelezo ya kina sana na sahihi kuhusu taarifa hii kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Dhamana za Serikali kwa ajili ya makampuni yanayouza bidhaa nje *(Export Guarantee Schemes*) zilianzishwa ili kuwezesha makampuni yetu kumudu kuuza bidhaa nje na kuingizia Taifa mapato ya Fedha za Kigeni.

Mheshimiwa Spika hata hivyo katika mpango huu, Serikali inaelekea kupoteza jumla ya shilingi bilioni 300 kutokana na makampuni yaliyopewa dhamana kutolipa mikopo yao kwenye mabenki. Hii inaongeza deni la Taifa kwa kiwango hicho cha fedha.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaendeleza wito wake wa kutaka Fungu 22 la Deni la Taifa lifanyiwe Ukaguzi Maalum *(Special Audit)* na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili tuweze kujua mikopo hii tunayochukua kila wakati inatumika kufanyia nini na miradi iliyotekelezwa kama ni miradi ya kipaumbele kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Aidha, ukaguzi huu maalum utatuwezesha kama Taifa kujua kiwango halisi cha Deni la Taifa ambalo tunadaiwa.

Mheshimiwa Spika, malipo ya riba na Deni la Taifa; kwa miaka mingi mfululizo tumekuwa tukitenga fedha kwa ajili ya kulipia deni la Taifa pamoja na riba mbalimbali zitokanazo na deni hilo la Taifa .Kwa mujibu wa ripoti ya ukaguzi ya *CAG* iliyoishia Juni, 2012 ni kuwa, tumekuwa tukilipa riba ya deni la Taifa kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2007 hadi 2012 jumla ya kiasi cha shilingi trilioni 1.523, (tazama jedwali namba moja)

Jedwali 1: Malipo ya riba kwa miaka mitano iliyopita (tarakimu katika bilioni):

| **Wadeni** | **2007/08** | **2008/09** | **2009/10** | **2010/11** | **2011/12** |
|---|---|---|---|---|---|
| Multilateral | 20.29 | 26.75 | 26.32 | 51.41 | 2.58 |
| Bilateral | 8.07 | 4.06 | 1.47 | 11.07 | 2.61 |
| Commercial/ Exp | - | 5.09 | 0.81 | 2.58 | 20.42 |
| Jumla ndogo | 28.36 | 35.90 | 28.60 | 65.06 | 85.61 |
| Domestic | 241.64 | 208.35 | 229.39 | 271.64 | 328.75 |
| Jumla kuu | 270.00 | 244.25 | 257.99 | 336.70 | 414.36 |

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2013/ 2014, Fungu 22 *programme* 10 utawala, kasma 100,1 kifungu kidogo 820300, inaonesha kuwa jumla ya sh. 357,304,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kulipia deni halisi la Taifa (*Principal*).

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kifungu 250500 kwa mwaka huu wa fedha zimetengwa jumla ya sh. 425,700,000,000 kwa ajili ya kulipia riba ya madeni ya muda mrefu (*Interest payments on long-term debt to other General Government).*

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kifungu 250100, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kulipia riba itokanayo na Deni la Taifa ni kiasi cha sh. 323,154,880,000 na katika kifungu 250600, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kulipia riba ya Deni la Taifa la ndani *other domestic interest payments not elsewhere classified* kiasi cha sh. 3,087,837,000.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ni kuwa, fedha iliyotengwa kwa ajili ya kulipia deni halisi la Taifa *(loans payment principal*, Kifungu 820300) kwa mwaka huu wa fedha ni sh. 357,304,000,000 wakati fedha iliyotengwa kwa ajili ya kulipia riba itokanayo na Deni la Taifa la nje na ndani kasma 22, (Fungu 250100, 250300, 250400, 250500 na 250600) kwa mwaka huu wa fedha ni sh. 1,021,942,717,000.00.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii ya kutenga

trilioni za fedha kwa ajili ya kulipia riba za Deni la Taifa, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa kuna haja ya kufanyika kwa ukaguzi maalum (*special audit*) ili Taifa liweze kujua kama mikataba ya madeni haya inafuata utaratibu mzuri wa kiwango cha riba ambayo tunatozwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, tunasisitiza ukaguzi maalum kufanyika kutokana na ukweli kuwa, mpaka sasa Serikali haina kitengo maalum kwa ajili ya deni la Taifa na hii inathibitishwa na taarifa ya Waziri wa Fedha ya tarehe 25 Machi, 2013; Maelezo ya Waziri wa Fedha kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwasilisha Mwongozo, matazamio na Upeo wa Bajeti ya 2013/2014, ukurasa wa Nne (4), aya ya pili alisema, nanukuu:

"Serikali iko katika mchakato wa kuanzisha Idara ya Madeni ambayo pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kujenga uwezo wa kufanya upembuzi yakinifu na kuhakikisha usimamizi madhubuti wa Deni la Taifa."

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, haiwezi kuendelea kukubaliana na utaratibu huu wa kukopa bila hata kuwepo kwa idara inayofanya uchambuzi yakinifu wa deni hilo na riba husika kama mkopo unazingatia thamani halisi ya fedha *value for money* ya mradi unaokopewa fedha hizo, hatuwezi kuendelea kulipia deni ambalo hatujui limewekezwa kwenye mradi gani wa maendeleo na manufaa ya mradi husika kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Fungu 13 - Idara ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi; Dira ya Idara hii ni kuimarisha na kudumisha mfumo wa udhibiti wa fedha haramu wenye hadhi ya Kimataifa utakaoimarisha mfumo wa fedha na kudumisha haki kwa jamii, kuleta utulivu wa kisiasa na ukuaji wa uchumi endelevu.

Mheshimiwa Spika, dhahiri kuwa fedha nyingi za Watanzania zilizowekwa kwenye mabenki ya nje kwa kiasi kikubwa ni fedha ambazo hazikupatika kwa njia za halali na kwamba kuna uwezekano wa ukwepaji mkubwa wa kodi.

Aidha, nchi yetu imekuwa katika matatizo makubwa ya fedha za kigeni, jambo ambalo limepelekea kushusha thamani ya shilingi ili kukabiliana na gharama za manunuzi ya bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa, dira hii inashindwa kutekelezeka kwani bado fedha nyingi za nchi hii zinahamishwa na kufichwa kwenye mabenki ya nje na fedha hizo kunufaisha zaidi wenzetu wakati Watanzania wakiachwa hoi bin taaban na hivyo kupelekea uchumi wetu kukosa utulivu na uendelevu kama dira ya Idara inavyosema.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa idara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ilitengewa shilingi milioni 1,944.79 lakini hadi kufikia februari, 2013, fedha zilizotolewa ni shilingi milioni 653.65 tu ambazo ni sawa na asilimia 33.6 ya makadirio. Kwa upande wa matumizi ya maendeleo bajeti ilikuwa ni sh. 267,800,000 lakini hadi februari, 2013, hakuna fedha yoyote iliyokuwa imetolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo za idara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014, fedha za matumizi ya kawaida zimetengwa shilingi milioni 1,944.79 kama ilivyokuwa mwaka 2012/2013 na kwa mwaka 2013/2014 fedha za maendeleo zimetengwa jumla ya sh. 399,685,000.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza kama fedha zinazotengwa hazitolewi kwa utoshelezi na pengine hazitolewi kabisa, je, ni kwa vipi idara hii itafanya kazi zake? Vita dhidi ya fedha haramu sasa ni vita ya Kimataifa. Wizara ya Fedha ni lazima iimarishe kitengo hiki ili kuendana na changamoto iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Fungu (7) - Msajili wa Hazina; Ofisi ya Msajili wa Hazina ndiyo ambayo imepewa majukumu ya kusimamia shughuli za uendeshaji wa Mashirika ya Umma, Taasisi na Wakala za Serikali. Majukumu hayo ni kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwake ni pamoja na: Sheria ya Msajili wa Hazina *(The Treasury Registrar's Ordinance Cap 418* na marekebisho yake); Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992 na marekebisho yake; Tangazo la Serikali Na. 23 la mwaka 1993 la kuvunjwa Kamati ya Rais ya Mashirika ya Umma (*SCOPO*) na mgawanyo wa majukumu yake yaliyokuwa yanatekelezwa na Kamati hiyo kufanywa na Msajili wa Hazina; na pia kupitia Nyaraka mbalimbali zinazotolewa na Msajili wa Hazina. Mwisho, ni ofisi hii kusimamia uandaaji wa ikama na bajeti ya mishahara katika Taasisi na Wakala wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi la ubinafsishaji wa mitaji ya kiuchumi lililofanywa na nchi nyingi za Kiafrika kwenye miaka ya 60 limechangia kuua uchumi wa ndani wa nchi nyingi barani Afrika. Ubinafsishaji huo ulitikisa misingi ya kiuchumi na matokeo yake hadi leo nchi nyingi bado zinahangaika na kukuza uchumi ambao utaendeshwa na sekta binafsi *(Private Sector Led Economy)*.

Mheshimiwa Spika, suala la utaifishaji njia kuu za kiuchumi limechangia kuzorotesha uchumi wa nchi nyingi za Afrika, ni lazima tujiulize ni kwa nini wenzetu wa Ulaya na Asia wanasonga mbele wakati sisi bado tunabaki nyuma" (Kwa mujibu wa Yoweli Kaguta Museveni – Mkutano wa Utekelezaji malengo ya Milenia, Serena *Hotel* Kampala, tarehe 4 Oktoba, 2010).

Mheshimiwa Spika, Mwaka jana tulizungumzia suala hili katika mjadala wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi, Kambi Rasmi ya Upinzani ilitaka kupata msimamo wa Serikali katika suala la ubinafsishaji wa mashirika ya umma, Shirika la *CHC* linasimamia sera ya ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Sera ya ubinafsishaji iliyoanza kutekelezwa mwanzoni mwa miaka ya tisini pamoja na kuleta baadhi ya manufaa imekuwa ikilalamikiwa sana siku hadi siku na wananchi. Malalamiko mengi ni kwamba nchi yetu imetekeleza zoezi la ubinafsishaji vibaya, liligubikwa na rushwa

*(briberization as termed by Joseph Stiglitz)* na uuzaji holela wa mali za yaliyokuwa mashirika ya Umma kama majengo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kampuni nyingi zinapoteza kiasi kikubwa cha fedha na zimeshindwa kutoa ushindani. Nyingi zimeendelea kuwepo kutokana na sababu za kisiasa na uwezo wa Serikali wa kuzifanya ziwepo unatokana na kuungwa mkono na fedha za wahisani. Mfano unaoonesha kuwa Serikali inatumia kampuni hizo kwa maslahi ya kisiasa ni usimamizi wa miundombinu ya umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, umeme wa Tanzania ni wa mgao, wananchi na wenye viwanda wana fursa nzuri ya kutokatiwa umeme mwaka wa uchaguzi, lakini baada ya uchaguzi, kukosekana kwa umeme kunaendelea. Wahisani wanaufanya mfumo wa kisiasa uliopo kuwa endelevu, wanaunga mkono miundombinu inayoanguka kuliko kuangalia ujenzi wa biashara zinazofikiwa na kusimamiwa vizuri, zikiwa na utumiaji na usimamizi wa fedha ambao ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Serikali inapata stahili zake kutokana na ubinafsishaji wa mashirika yake yanayobinafsishwa iliunda Shirika Hodhi la yaliyokuwa Mashirika ya Umma (*CHC*) kwa lengo la kuhakikisha mikataba ya ubinafsishaji inalinda. Aidha, ni jukumu la msingi la Msajili wa Hazina kulinda hisa za Serikali katika ubia wa Serikali na mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, Ofisi ya Msajili wa Hazina *(TR-Treasury Registrar)* imekuwa dhaifu mno katika kusimamia mali za Serikali katika Mashirika. Mifano ya namna hisa za Serikali zilivyouzwa itasaidia kuonesha hali hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza Kampuni ya *Oryx* ilikuwa inamilikiwa na Serikali kwa asilimia hamsini mpaka mwaka 2004. Mwaka 2004, kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina (*TR),* Serikali iliuza hisa zake ambazo ni asilimia 50 kwa bei ya kutupa kwa thamani ya dola 2.5 milioni.

Mheshimiwa Spika, pili, hisa asilimia 25 zilizokuwa za Serikali katika Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa kuuzwa kwa wamiliki wa Kiwanda kwa utaratibu usio wa wazi. Jambo hili limeonesha pia udhaifu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, katika kuthibitisha udhaifu huo Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali alitoa ushauri: "Serikali itapaswa kuangalia uwezekano wa kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi itakayokuwa na jukumu la kudhibiti na kusimamia uendeshaji wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma 176 zenye hisa/mtaji ya jumla ya Shilingi trilioni 12.2 katika kukuza uwajibikaji na uwazi katika kutoa huduma nzuri kwa Umma" (Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ripoti ya Mashirika ya Umma 2011/2012 Ukurasa wa 18).

Mheshimiwa Spika, utendaji mbovu wa Msajili wa Hazina kwa njia moja au nyingine unatokana na uzembe wa Serikali wa kutowathibitisha watendaji au Mkurugenzi badala yake amekuwa akikaimu nafasi hiyo ya juu kwa kipindi chote jambo linalopelekea ashindwe kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya uteuzi au mchakato ambao utajaza nafasi zote muhimu zinazokaimiwa ili kuondokana na tatizo la utoaji wa maamuzi kwa taasisi zetu.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Uwekezaji ya (*NICOL*); Mwaka 2001 ilianzishwa kampuni ya Wazalendo ya uwekezaji iliyokusanya mtaji wake kwa kuuza hisa kwa wananchi takribani Wilaya zote za Tanzania Bara na ikafikisha mtaji wa kiasi cha shilingi bilioni 8.4 kutoka kwa wanahisa wake takribani 48,000.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kuwa hii ni kampuni ambayo imekusanya fedha kutoka kwa wananchi maskini baada ya kuwauzia hisa pamoja kwamba imekuwa haifanyi vizuri siku za hivi karibuni kutokana na migogoro ambayo imeikumba kampuni hii ikiwemo mgogoro wake na Mamlaka ya Mitaji na Dhamana (*CMSA*), jambo ambalo

lilipelekea kufungwa kwa akaunti zote za kampuni hii katika Benki mbalimbali na hivyo kushindwa kutoa taarifa zake za fedha kwa mwaka 2010, 2011 na 2012, jambo lililopelekea kuondolewa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuwaeleza Watanzania hasa wanahisa kuhusiana na mambo yafuatayo:-

(i) Ni nini hatima ya fedha za wanahisa wa kampuni hii ambao ni Watanzania maskini waliohamasishwa kununua hisa, je, fedha zao ziko salama?

(ii) Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na Watanzania kuendelea kununua hisa na kuwekeza kwenye makampuni mbalimbali hapa nchini hasa baada ya uzoefu huu wa *NICOL* na *TOL.*

(iii) Nini athari za mgogoro huu wa *NICOL* kwenye umiliki wa Benki ya NMB kwa hisa milioni 33 ambazo ni sawa na asilimia 6.6 ya hisa zote za Benki hiyo?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha na yale yote ambayo sijayasoma yaingie katika *Hansard*. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante, ni kama umeni-*time* kabisa. Waheshimiwa Wabunge sasa naomba niwataje wafuatao ambao watachangia; Mheshimiwa Zakhia Meghji, Mheshimiwa Omari Nundu, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran na Mheshimiwa Devotha Likokola. Mheshimiwa Zakhia Meghji!

**MHE. ZAKHIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara ya Fedha. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ndiyo Wizara ambayo inapanga, inayopendekeza na pia kusimamia utekelezaji wa Sera zote ambazo zinahusu fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kama vyanzo vya mapato ni vidogo, kama riba katika mabenki ni kubwa, suala la utendaji wa pensheni, *schemes*, sheria zinazohusu fedha na mikopo pamoja na uwekezaji na pia kudhibiti deni la Taifa sote tunanyoosha kidole kwa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, sera zinazotoka Wizara ya Fedha ni sera muhimu sana na kwa maana hiyo, katika mchango wangu huu nitajikita zaidi katika sera zinazohusu masuala ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kama muda utaniruhusu ningependa kuzungumzia maeneo matatu. Kwanza kabisa, sera inayohusu mikopo ya nyumba yaani *Mortage Financing;* pili, sera inayohusu *retention* yaani makusanyo ya fedha yanayobaki pale pale ambapo kunakusanywa, kama katika Wizara au katika Idara, na tatu, mikopo midogo midogo kwa wananchi wa hali ya chini yaani *micro-financing*.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kuzungumzia juu ya mikopo ya nyumba au *mortage financing*. Wizara ya Fedha ilileta Sera na Sheria ya Mikopo ya Nyumba ili kuweza kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kujenga nyumba na kuweza kuishi pia kwenye nyumba bora kwa kuchukua mikopo kutoka benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ni budi tujiulize je, utekelezaji wake upo vipi na unasaidia vipi sehemu kubwa ya jamii ambao ni wananchi wa hali ya chini. Kwa maana hiyo, ni lazima tuangalie riba inayotozwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa riba ya mikopo ya nyumba inayotozwa Tanzania tunaweza kusema kwamba ni kubwa sana. Riba ya juu nafikiri ni kama asilimi 19 na riba ya chini ni asilimia 15. Kwa maana hiyo wastani wa riba

inayotozwa ni kama asilimia 17 ambayo mtu analipa kwa muda wa miaka 20 mpaka 25. Hii ni riba kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mikopo ya nyumba ili iweze kusaidia wananchi na waweze kulipa, wasiweze kufika katikati halafu nyumba zao zikauzwa, ni lazima riba hii iwe na tarakimu moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati nchi kama Australia kwa mfano, riba ni kama asilimia tano tu, kwa maana hiyo unalipa mkopo wako kama vile unalipa kodi yako, badala ya kumlipa mwenye nyumba ile kodi unalipa ile kodi kwenye benki mpaka unaweza kumaliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kuna haja kubwa ya kuangalia sera hii ya riba ya mikopo ya nyumba. Kuna wakati mmoja ambapo hata Gavana wa Benki Kuu, Profesa Ndulu, alishangaa kwamba, iweje mabenki yachaji riba kubwa wakati taasisi ya *Mortage Refinancing Company* ambayo inapitisha mikopo yake kwa wateja kwa kupitia benki zilizoungana ilipata mkopo kwa kuanzia kutoka Benki ya Dunia kwa riba ya asilimia nane(8).

Mheshimiwa Spika, sasa hapa wamepata riba ya asilimia nane, lakini wao wanachaji riba ya asilimia 19. Hata kama tutazungumzia masuala ya *administration cost* na kadhalika, nafikiri hii ni riba kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kwa mfano, mtu akikopa labda milioni 25 kujenga nyumba, kwa asilimia hiyo kumi na tano au kumi na tisa, kwa muda miaka 25 kwa riba hiyo utalipa karibu shilingi milioni 60 mpaka 70, hii ni ngumu sana kwa wananchi kuweza kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara nyingi sana tunaambiwa kwamba Tanzania ingekuwa ina vitambulisho vya Taifa, labda riba ingeweza kupungua, lakini tujiulize kwa sababu wanasema kwamba hawajui mahali watu wanakaa na kadhalika, tujiulize Wabunge hapa ambao wanajulikana

wanaishi wapi, wanafanya wapi, wanapata mshahara gani asilimia ngapi ambayo wanalipa? Ni asilimia kubwa ambayo wanalipa, asilimia 15 mpaka 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, jibu la kusema kwamba kwa sababu tu hakuna vitambulisho vya Taifa nafikiri siyo jibu sahihi, kuna haja ya Wizara ya Fedha ilichukue jambo hili na iangalie ni jinsi gani ambavyo mikopo au riba ya fedha itaweza kupungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka naona kengele ya kwanza imelia, napenda kuzungumzia juu ya kuwashirikisha wananchi wa kipato cha chini kupata mikopo midogo midogo. Ukurasa wa tisa wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, inazungumzia juu ya kuhamasisha uanzishaji wa ushirika wa kuweka na kukopa yaani *SACCOS* na *VICOBA* ili wananchi wengi zaidi wa hali ya chini waweze kujihusisha katika uzalishaji mali, katika kilimo, uvuvi, ufugaji na kadhalika. Kwa maana hiyo, hivi sasa wananchi wengi sana wameitikia wito huo kupitia *VICOBA*.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kwamba amana ya *VICOBA* inachukua karibu bilioni 300 ukichukua kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Lakini tatizo kubwa limekuwa hakuna sera ya *microfinance*.

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante.

**MHE. ZAKHIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Omar Nundu na Mheshimiwa Joseph Selasini ajiandae.

**MHE. OMAR R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote niisifu Serikali na Bunge zima kwa kuja na huu mfumo mpya wa bajeti wa kuangalia Wizara zote tumeona kipi kinahitaji na mwisho wa siku tunakuwa hatuna matatizo ya kubishana pale tunapohitimisha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bajeti ya trilioni kumi na saba na nusu kwa nchi kama ya Tanzania, tunakwenda kwenda tu, lakini siyo bajeti ambayo itatupeleka mbele zaidi. Sasa kama pesa hizo hazikuweza kupatikana, ikawa *business as usual,* mwisho wa mwaka tukakuta kuna Wizara kadha wa kadha ambazo hazikupatiwa pesa hizo. Matatizo yatakuwa ni makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, hapa ndipo ambapo nakwenda sasa kwenye Wizara husika ambayo hoja yake tunai-*discuss* leo. Pamoja na kuwasifu kwa kutoa hotuba nzuri na mikakati mingi, lakini kikubwa mwisho wa siku ni kuwa, Wizara na Taasisi zake zote kwa jumla zijitahidi kile ambacho kinatakiwa kikusanywe, kikusanywe na kipelekwe kule kunakohitajika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina jukumu kubwa sana la kutumia rasilimali yetu ya asili tuliyo nayo ambayo ni binadamu wenyewe na tunao wengi, tuko karibu milioni 45 sasa hivi. Nchi yoyote haiwezi kuendelea kama rasilimali yake hiyo haitumiki na tuna bahati kwa Tanzania. Watanzania kwa umaskini wao wanajitahidi kwa kila njia kutafuta njia ya kujipeleka mbele kimaendeleo, lakini uhusiano uliopo kati ya Taasisi ya Wizara hii na Wizara yenyewe pamoja na wafanyabiashara hawa ambao wengi ni wadogo wadogo, naomba uangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana hapa tuliangalia suala la boda boda ambao walikuwa wanapata unafuu wa kodi kwa kufikiria kuwa wanakusanya milioni tatu. Tukasema wakikusanya milioni nne, ndiyo unafuu wa kodi uanzie hapo.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kuwa boda boda mapato yao ni milioni tano na laki sita, siyo milioni nne. Kwa hiyo, kukurupuka hatuna kusema kuwa milioni nne ndiyo wasilipe kodi, naona halikuwa jambo sahihi. Wataalam walioko kwenye Wizara hii naomba wasifanye uvivu, waangalie mapato na matumizi ya wafanyabiashara wadogo wadogo. Tusiangalie tu kuwa wanalipa kodi kutokana na mapato tuangalie na matumizi yao.

Mheshimiwa Spika, nimesema kuwa kipato cha boda boda na nilifanya mkakati hapa wa kuona gharama zao ni vipi. Ni milioni tano na laki sita kwa mwaka, lakini matumizi yao ukiyafuata ni milioni saba laki moja na kumi na nane elfu.

Mheshimiwa Spika, boda boda hizi zinapata hasara ya zaidi ya milioni moja na si kwamba, ukiwa na boda boda nyingi basi faida inakuwa kubwa kwa sababu kila boda boda moja ni kitengo kinachojitegemea. Mtu hata ukiwa na boda boda tano, hasara ile ya kila boda boda moja utairudia katika boda boda nyingine zote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukiwa na nyingi ndiyo unazidi kupata hasara. Sasa tunaposema anayekuwa na boda boda mbili aanze kulipa kodi, tunawaua, tunawamaliza. Wanachofanya kukwepa hili ni kuwalipa wale madereva mshahara ambao hauendani na hali ya maisha hapa na kufanya hivyo boda boda zao zinamalizika upesi sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Meghji ameliongelea suala la riba na huku linajitokeza. Hatuwategemei hawa wawe na hela zao mfukoni, wanakwenda Benki kukopa pesa, riba kule ni asilimia 20. Ukikopa milioni moja na laki saba na hamsini elfu, unaishia kulipa zaidi ya milioni mbili na ukisema uzilipe kwa miaka mitatu inabidi utenge laki saba na themanini elfu, halafu kama hiyo haitoshi boda boda inatozwa shilingi elfu kumi kwa *fire extinguisher,* boda boda gani inayobeba *fire extinguisher. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu hii elfu kwanza itoeni kabisa, kesho mtasema abebe matairi halafu pia muwa-*charge,* halafu inaambiwa *fire extinguisher* inachajiwa siyo kwa sababu wanapewa, kwa sababu wanatakiwa watu wa *fire* wafanye *inspection.* Hakuna fire yeyote anayefanya *inspection* yoyote kwa boda boda. Hii elfu kumi naomba Mheshimiwa Waziri uitoe kabisa, usipoitoa nashika shilingi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wadogo wadogo na

Tanga ninao wengi wanatoka Lushoto na sehemu nyingine, wanauza njugu kuweza kujikimu. Akinunua kilo tatu za njugu yule anapata kwa mwaka makusanyo karibu milioni tano na laki moja. Ukienda kwa kile Kitengo cha milioni nne, yule anavunja sheria anapata milioni tano na laki moja lakini halipi kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini mwangalie gharama zake za kuuza njugu zile anatumia karibu milioni sita laki sita na tisini na saba. Sasa ukimwambia alipe kodi ni matatizo. Hebu jamani fanyeni kazi, *Accountants* wapo hapa, ndugu yangu Katagira nilikuwa naye *Glasgow* kule anasomea hilo, labda mmwambie mambo haya.

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu ambaye anaanza kutoza kodi kwa mapato wakati hajajua mtu ametengeneza hasara au vipi? Kama mnaona uvivu kufanya hivyo, basi muweke kiwango ambacho napendekeza mpaka milioni saba mtu asitoe kodi na mtu hata akiwa na boda boda kumi zile ni hasara tupu, asitoe kodi. Ndiyo hapo tutaweza kuwapata wafanyabiashara ambao watakuwa katika mazingira ya kuzoea kulipa kodi. Maana wakianza kukwepa kodi huku nyuma, huko mbele ndiyo matatizo hata anapokuwa mfanyabiashara mkubwa hapa nchini, lazima tuwaanzishie huku chini waendelee zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa pesa zitatoka wapi? *Sheraton Hotels* inapokuja kuanzisha biashara Tanzania, ile haitegemei itengeneze faida siku ya kwanza hapa. Lile ni jikampuni kubwa, wanafanya *cross subsidization*. Sasa ni maajabu sisi tunapojipeleka kichwa mbele na kuwapa msamaha. Halafu siyo msamaha wa miaka mitano tu, miaka mitano ikiisha tunawapa msamaha tena. Tunataka kijana wa boda boda alipe kodi, lakini huyu wa *Sheraton* apate msamaha, apate msamaha apate msamaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama akina *Sheraton* hawaji hapa, wanakuja watu wanaokuja kujaribu kufanya biashara hapa, ndiyo wanaohitaji msamaha. Tusiwakaribishe, tusiwakaribishe watu wanaokuja kujaribu kufanya biashara,

halafu anakuja anakopa kwenye mabenki yetu haya. Wanaondoa nafasi za vijana hapa wanaotaka kujiendeleza, wanakopa pesa wao halafu tunawasamehe.

Mheshimiwa Spika, ukiingia hoteli za akina *Sheraton* hizi chupa ya maji ya shilingi mia tatu wakati ule nje, kule unauziwa kwa elfu tatu. Halafu mtu huyu anapewa msamaha wa kodi, inakuwaje? Lazima tutoke huko. Nimesema nchi yoyote watu wake ndiyo wanakwenda mbele kwa Tanzania hii, kitu kikubwa ni biashara na watu wetu wanaojituma.

Mheshimiwa Spika, wanaanzia chini kabisa na wanaendelea na mifano iko mingi. Uingereza pale kulikuwa na mtu anaitwa Allan Michael Sugar, yeye alikuwa anauza maandazi *Liverpool Street.* Akapewa unafuu na nchi yake. Yule mtu alikuja mwaka 1986 akaanzisha televisheni ambayo ina na *video* pamoja, inaitwa *ARMSTRAD* ile *ARMSTRAD Brand ni* Allan Michael Sugar amekuwa *millionaire.* Akina Fred Lake hivyo hivyo. Wenzetu wanaenzi hawa wafanya biashara wadogo wadogo. Sisi tusiwadhalilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Meghji amegusia suala la riba. Riba hapa jamani, inaathiri kweli. Ukitaka kukopa, kwanza kukopa kwenyewe kwa Mtanzania utazungushwa weee, kinachotakiwa hakijulikani pale. *CRDB* ilikufa hapa na mnajua kwa nini ilikufa mpaka ikaanza kufufuka upya, ilikwenda kabisa ikafilisika kutokana na watu wanavyohangaishwa mpaka kupata pesa.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa naongea na Meneja wa *CRDB,* akaniambia Tanga yako hapa, ile mikopo ilifika bilioni 52, watu wakashindwa kulipa. Mtu wa Tanga gani aliyekopa bilioni 52 ashindwe kulipa pale. Kama si hao hao wenyewe maofisini wanayapitisha pitisha tu huko.

Mheshimiwa Spika, sasa tumekwenda tumechukua mabenki yote tumewakabidhi watu binafsi. Lazima tuwe tunaangalia, kuna vyombo vingine huwezi ukakabidhi vyote kwa watu binafsi. Kwa nini isianzishwe benki ambayo itasaidia

wananchi? Mabilioni ya Rais Kikwete ukiyaulizia yamekwenda wapi na akina nani wamepata, vurugu tupu. Watu hawakupata. Kwa nini tusirudi nyuma. Kuna Taasisi ambazo nchi haiwezi kukosa kuwa na Taasisi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Canada wana *National Bank of Canada* pale, pamoja na mapesa waliyonayo. Ile ni benki ya nchi, inatoa riba nafuu na Serikali yenyewe inatafuta njia ya ku-*absolve* hiyo, lazima tuanzishe Taasisi kama hiyo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. OMAR R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja kwanza zile elfu kumi zitakapotolewa pale. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa naendelea, sasa namwita Mheshimiwa Joseph Selasini, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Mussa Zubeir.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kabla sijachangia nami nikupongeze kwa kusimamia huu mfumo mpya wa kujadili Bajeti ya Serikali ambao unaendelea sasa hivi. Vile vile nikupongeze pia kwa sababu ya kuunda ile Kamati ya Bajeti ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia sana katika kupunguza mivutano kati ya Serikali na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nataka kuchangia katika mambo yafuatayo:- Karibu asilimia 70 ya fedha ambazo tunajadili hapa zinaelekezwa katika Halmashauri zetu. Katika miaka miwili iliyopita nilikuwa Mjumbe katika Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Nilichokiona na kinachoendelea kufanyika sasa hivi ni kwamba ndani ya Halmashauri zetu

kuna ufisadi uliokithiri. Karibu nusu ya fedha hizi zinazopelekwa katika Halmashauri zinaishia kwenye mifuko ya watendaji. Sisemi wote, lakini baadhi yao.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinaishia kwenye mifuko ya watendaji kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza ni kwamba, sheria tuliyonayo ya manunuzi, bado ina mianya mingi sana, inahitaji kufanyiwa mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, utashangaa, kitu kinachouzwa dukani shilingi elfu tano, kikiingizwa katika mfumo wa tenda, basi yule mkandarasi atadai shilingi laki tano. Hii siyo siri ni jambo linaloendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama sisi Wabunge tuna dhamira ya fedha zile ziwafikie wananchi kwa ajili ya miradi yao lazima tuhakikishe Sheria hii inatazamwa ili tuweze kuziba hii mianya. Napendekeza ikiwezekana baadhi ya bidhaa Serikali itoe bei elekezi kwa baadhi ya bidhaa. Kwa mfano karatasi, bunda moja la karatasi kila mtu anafahamu, dukani ni sh. 10,000/=, lakini mkandarasi akiipeleka Halmashauri ni sh. 40,000/=. Hivi kweli ni sahihi tunaangalia tu hivi? Zile fedha ni fedha ambazo zingekwenda kwa ajili ya huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinapotea kwa namna nyingine tena kupitia kwa Wakaguzi wa Ndani. Baadhi ya Wakaguzi wa Ndani nadhani wana ubia na Wakurugenzi. Kwa sababu haiwezekani Mkaguzi hana gari, hana Komputa, hana kitendea kazi chochote, anakwenda kuchukua pale kwa Mkurugenzi halafu amkague Mkurugenzi na kugundua kwamba ameiba au ametumia fedha vibaya, halafu huyu Mkaguzi wa Ndani atoe maelezo yanayotosheleza haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni lazima tuitenganishe Idara ya Mkaguzi wa Ndani na Mkurugenzi Mtendaji. Ili hii Idara ijitegemee na ripoti za hii Idara zisiende kwa Mkurugenzi

Mtendaji, ziende katika utaratibu kama utaratibu wa *CAG*. Kwa jinsi hiyo tutadhibiti wizi mkubwa sana ambao unatokea ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu kucheleweshwa kwa fedha za maendeleo kwenye Halmashauri. Fedha zote tunazoidhinisha hapa, mwisho wa siku lazima Wizara izipeleke kwenye Halmashauri kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kiasi kikubwa sana fedha hizi huwa zinachelewa na zikichelewa miradi inachelewa kukamilika. Zinakwenda kwenye robo ya mwisho ya mwaka. Sasa Sheria ya Manunuzi inapoanza kutumika, ni kwamba fedha zile zinashindwa kutumika na matokeo yake zinarudi Hazina na miradi mingi sana inachelewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naiomba Serikali kama kweli dhamira ni kusukuma maendeleo ya wananchi wetu, basi ni vema sana fedha hizi zikaenda kwenye Halmashauri kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia, ni Sera ya *Microfinance.* Wananchi wengi sana vijijini mpaka leo hii fedha zao ziko mchagoni na ziko mchagoni kwa sababu benki kubwa ziko mijini tu, hizi benki za biashara, *NBC, NMB, CRDB* ni benki za mijini. Wananchi wetu kule vijijini hawana utaalam, hawana ujuzi, hawana mazoea ya kutumia mabenki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, kama kweli tunataka kuendeleza watu wetu. Hakuna mfanyabiashara anayefanya biashara kwa pesa zake mfukoni hayupo. Wafanyabiashara wote tunaowafahamu wakubwa na wanaofahamika, wanafanya biashara kwa kutumia fedha za mzunguko kwenye mabenki. Sasa tunataka wananchi wetu waendelee wataendelea kwa pesa kutoka wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali

ikamilishe Sheria na Sera ya *Microfinance* ili wananchi wetu wapate nafasi ya kuanzisha benki zao ndogo ndogo vijijini. *SACCOS* tulizoanzisha zigeuzwe kuwa *banks, VICOBA* na kadhalika vya Mama Likokola, watu waweze kukusanywa, waweze kufundishwa namna ya kukopa.

Mheshimiwa Spika, katika hili nataka niendeleze pale alipofikia Mheshimiwa Nundu, kwamba, watu wetu wanajitahidi sana, mama zetu vijijini wanajitahidi sana, lakini wanakwamishwa kwa sababu ya sera na taratibu ambazo tunaziweka sisi wenyewe za kuwahujumu. Amezungumza suala la boda boda ni kweli. Boda boda wanazungushwa, wanahangaishwa kila Wilaya, hakuna Jimbo ambalo mateso haya boda boda hayapatikani.

Mheshimiwa Spika, kule kwangu Rombo sasa hakuna mradi mzuri wa Watendaji wa aina mbalimbali, baadhi ya Polisi na baadhi ya watu *TRA* kama kukimbizana na vijana wa boda boda na hili ni lalamiko kubwa, kila mahali tunalizungumza, lakini halisikilizwi.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hivyo, sitaki niseme kwamba eti utengenezwe utaratibu wa kukwepa kodi, lakini ziwekwe kodi za kueleweka ili walipa kodi wawe rafiki kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika hili ningependa pia niwazungumze wafanya biashara wakubwa. Ni lazima sasa hivi Watanzania tupunguze au tuondoe kabisa fikra za kufikiri kwamba kila mfanyabiashara mkubwa ni mwizi, kila mfanyabiashara mkubwa ni fisadi, hapana, hii si kweli. Wako wafanyabiashara wakubwa waaminifu sana, wanalipa kodi na kodi hii ndiyo inayotusaidia. Lakini wako wafanyabiashara au baadhi ya wafanyabiashara wakubwa ambao pia wanakwenda utaratibu wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme, naipongeza *TRA,* imeleta mabadiliko makubwa sana katika mfumo wa kodi katika nchi yetu na imefanya kazi kubwa pamoja na kwamba

tunaitaka ifanye zaidi. Ukiangalia ulipaji wa kodi kwa miaka 10 iliyopita na sasa hivi kuna tofauti kubwa kabisa. Sasa mimi naiomba *TRA* itengeneze urafiki na wafanyabiashara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, atafuatiwa na Mheshimiwa David Kafulila na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo ajiandae.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwanza kwa kupata nafasi hii nikiwa na wingi wa afya. Niipongeze Wizara ya Fedha kwa hotuba yake nzuri na yenye mwelekeo na naunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninachotaka kuwaelewesha Watanzania ni kwamba, umefika wakati tunatakiwa lazima tukubali kidogo tulichonacho, halafu tutafute mbinu za kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipofanya hivi siku zote hatutaweza kuendelea mbele. Yaani tukikataa ukweli au kama utakuwa unakimbia kivuli chako ambacho unacho, basi huwezi ukafikia popote. Nazungumza haya nikiwa na maana halisi kuna baadhi ya watu nafikiria kwenye Taasisi zetu na Wizara zetu wameligundua hilo, lakini bado kuna kuganda ganda na kusita sita.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mzima wa *PEMANDU* ambao huu tuliuhisi kwamba pengine ungekuwa ni faraja na ni mkombozi wa Tanzania, lakini naona kwenye bajeti hii bado tunasuasua na tulikwishafikia hatua nzuri. Niliona ni wakati muafaka umefika kuanza kufanya hili suala ili tukaenda nalo.

Mheshimiwa Spika, kati ya yaliyozungumzwa humo kwenye huo mradi wa *PEMANDU,* kwanza Serikali ilikula

hasara sana, ilipeleka watu kule Malaysia kwenda kusoma, watu wameitwa wamekuja huku; ndio pale Tanzania tunaposifika kwa kuhifadhi makabrasha yenye thamani, wakaja watu kwa maelezo yetu tu, wakayachukua yale maelezo, *note* ndogo wakaenda wakafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna nguzo tano za *BFR* hii *Big Fast Results.* Kwanza ni Uongozi Thabiti uliodhamiria kuleta mabadiliko na kuipeleka nchi mbele, kutekeleza vipaumbele vichache kwa nguvu na kuelekeza rasilimali nyingi zaidi katika vipaumbele hivyo; haya mambo jumla yako matano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ningeishauri Serikali. Serikali, ilianza hili suala vizuri, lakini bado iliweka vipaumbele karibu sita; sasa ndio pale ninaposema jamani tunatakiwa tukubali hali tuliyokuwanayo.  Naona kama kweli kwa mwaka tuna uwezo wa kukusanya trilioni 17 na katika hizi karibuni trilioni saba zinakwenda labda kwenye mishahara, basi naona hata hivi vipaumbele tuvipunguze, twende na kama kimoja ama viwili na si aibu kwa sababu, ndio fedha yetu ya ndani tunayoweza kukusanya. Kutegemea Wahisani na watu wa nje, tusitegemee kama tutafika mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoweka miradi mikubwa kama hii ya kutaka ku-*generate* nchi, kuitoa hapa ilipo kwenda sehemu nyingine, halafu ndani yake tukaweka na asilimia ya kutegemea Wahisani, kwa kweli tunakuwa hatufiki mahali.

Mheshimiwa Spika, Wahisani hawa hawapendelei sisi tuendelee kabisa na watakuwa wako tayari kutusaidia kwenye miradi kama ya vyura Kihansi, ambayo inatupotezea muda au kuileta ile mifupa ya mjusi mkubwa, haya mambo hayatuendelezi; huku wataleta fedha nyingi, lakini tutakapowapa miradi kama tunawaambia tuna shida ya umeme au tuna masuala ambayo, kama wakijua kwamba, hili likifanikiwa tutakuwa tumekwenda hatua mbili mbele, hawawezi wakatusaidia mia kwa mia. Kazi yetu itakuwa tunakwenda na kurudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni afadhali tukategemea fedha zetu ndogo za ndani tukaamua kama ni mradi mmoja au ni miwili basi, tukafanya huo ukakamilika, ukaisha. Hawa Wazungu wanasema *if you want to please all, you please none,* kama unataka kufurahisha wote, hutafurahisha hata mmoja. Ni lazima kwa wengine kutakuwa kuna manung'uniko na vilio, lakini tukisema kwamba, hebu tupeni mradi mmoja ambao tukiufanya utakuja kusaidia baada ya miaka mitatu mbele, basi tufanyeni hivyo.

Mheshimiwa Spika, hao watakaokabidhiwa hizi dhamana za kufanya hivyo, wajijue wana kitanzi kwa sababu, wamezuia fedha za walipa kodi wa Tanzania nzima kwa sababu, tunaweza tuka-*dump* fedha nyingi pale kwa mategemeo ya kwamba, pale ndipo patakapokuja kutusaidia kutukwamua kutoka hapa kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa huyo atakayekuwa na dhamana hiyo itatakiwa atoe *time frame,* awe na uhakika wa muda kwamba, kwa mradi huu mtakaonipa na fedha hizi mtakazonipa, basi ndani ya miaka mitatu tutakuwa tumeondoka hapa na kuelekea safari nyingine. Baada ya miaka mitatu, hakuna lililotokea, ajijue yeye ana kitanzi hakuna kitu kingine; ndio tutaweza kuendelea, kinyume cha hapo hatuwezi kufika, tunatakiwa kwanza tuwe na imani ya kutaka kujisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapotaka kufanya jambo, kama ni Waziri au ni nani, jambo la kwanza ujiulize, hivi *I am doing this for the sake of what?* Unajiuliza kwamba, hiki ninachotaka kufanya nataka kufanya kwa maslahi ya nini au ya kitu gani? Jibu, hana haja ya kukaa kwenye vyombo vya habari, akijiuliza tu mwenyewe, basi jibu atalipata tu, kama ni kwa maslahi yake mwenyewe binafsi ama kweli anataka kulisaidia Taifa. Sasa akifikia hatua hii, hapa tutakwenda tu kwa sababu hata majanga na matatizo na Mungu naye atamwangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya hawa watu wa

*PEMANDU* waliokuja hapa, wameeleza. Kwanza tuwe na mikakati, tuwe na ujasiri, tuwe wakweli na mwisho Mungu na yeye vile vile anasaidia kwa ile nia uliyokuwa nayo, lakini kama nia yenyewe ni mtu kutafuta nafasi, akipata aanze kuvutia upande wake ukweli hatutafika. Ndipo hapo niliposema kwamba, ni vizuri tufikie hatua basi, mtu awe anajiuliza na ajijue kwamba, ana kitanzi kwa sababu, amechukua fedha za mwaka mzima za walipa kodi wa Tanzania tumepeleka upande mmoja, wengine wanasikitika, nafikiri, tunaweza tukafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nisije nikasahau, kuna suala la *NMB* kule Zanzibar, inafanya kazi vizuri sana, lakini ningemwomba Waziri, basi awaambie hawa watu watuongezee matawi, angalau tupate mawili au matatu kwa pale Unguja. Kwa sababu, ukweli, hili lilipigiwa kelele sana limeshajaa watu pale. Unguja nzima ni eneo moja tu na ukitazama Benki nyingine kama *Barclays* wapo mpaka Mwanakwerekwe na maeneo mengine kule, wanafanya kazi za vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *mini tiger.* Hili suala lilikuwepo kwenye bajeti iliyopita na kuna fedha kidogo zilitolewa karibu bilioni 10 na *point* na hazijakwisha zile fedha. Sasa ninachoshangaa tumemaliza na tunaingia kwenye muhula mwingine hakuna chochote, yaani kuko *silence* na ndio yale ya kugawagawa fedha, ndio yale niliyoyasema kwamba, unapotaka kuwafurahisha wote, huwezi kumfurahisha hata mmoja.

Mheshimiwa Spika, kuna bilioni 10 zilishaanza kutolewa kwenye bilioni 50.2, bado fedha nyingine zinahitajika. Zimetoka hizo 10, sasa hizi nyingine safari hii hazimo tena, yaani zile ndio zitakuwa zimetoka na huku tunakokwenda hatujui huu mradi utakwisha vipi na mradi huu ungeweza kutoa ajira kwa vijana wengi sana na kuweza kukusanya hizo kodi ambazo tunazitarajia kwa huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha, aeleze hili suala kama ndio halipo tena

na zile fedha zetu za Tanzania bilioni 10.9 ndio zimeshakwenda **harijojo** kwa masuala haya ambayo tunakwendanayo kama hivyo nilivyosema huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, lingine kulikuwa kuna suala la upande ule wa Zanzibar. Kulikuwa kuna watu walizuiliwa kule nanihii zao, lakini hili lilikuwa ni tatizo la *TRA,* hata Wizara ya Fedha, hili suala watakuwa wanalijua. Kuna watu walizuiliwa *licence* zao, lakini imegundulika kwamba, matatizo haya yametokana na watu wa *TRA* kuvujisha zile *password.*

Mheshimiwa Spika, kuna magari kwa ufupi yamezuiliwa yako pale Dar-es-Salaam, yanatakiwa yalipiwe ushuru. Kuna viroja vimefanyika, wakishirikiana na watu wa *TRA,* lakini ukweli huyu mhusika ambaye yeye ndio kazuiliwa hii *license* yake ya *Clearing and Forward,* yeye hakuwa na matatizo hayo na hili wameligundua. Sasa naomba basi wafanye utaratibu huyu mtu aweze kuendelea na ile kazi... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa David Kafulila, atafuatiwa na Mheshimiwa Kombo.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kujadili Wizara muhimu kabisa, pengine kuliko Wizara zote ambazo tunazijadili katika Bunge la Bajeti. Unapojadili Wizara ya Fedha, maana yake unajadili, kwa kiasi kikubwa, namna gani tunaweza tukajenga uwezo wa kujitegemea kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana kwamba, Taifa letu lina uwezo mkubwa sana wa mipango kuliko Mataifa mengi duniani, kuliko Mataifa mengi katika Afrika, lakini tuna uwezo mdogo sana; tuna Serikali, yenye uwezo mdogo sana katikia kusimamia mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ambalo linakabili

Taifa hili kwa sasa, ni namna gani tunaweza tukakusanya mapato ya kutosha kuweza ku-*finance budget,* kuweza kutoa huduma za afya, kuweza kutoa huduma za elimu. Kiwango kikubwa sana cha umaskini wa leo, kinatokana na uwezo mdogo wa Serikali, kukusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ziko wazi. Mwaka 2010 miongoni mwa maeneo ambayo tunakabiliwa na tatizo hili ni kwenye eneo la madini. Mwaka 2010 ikapitishwa Sheria hapa kwamba, *TRA* sasa ianze kukusanya fedha kutokana na migodi hii ya madini kama kodi, lakini uwezo wa *TRA* kukusanya kodi kwenye migodi ya madini ni mdogo mno. Sio mdogo kwa bahati mbaya, ni mdogo kwa makusudi kwa sababu, kuna watu wanafaidika na huo udhaifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makampuni ya Madini yanapandisha gharama za uzalishaji kila kukicha, bei ya dhahabu ikiongezeka na wao wanaongeza bei ya uzalishaji, ili kupunguza kodi. Wakati bei ya dhahabu ni dola 300, wao wanasema gharama ya uzalishaji kwa gramu 30, yaani *ounce* ni 200. Wakati bei ya dhahabu inapanda mpaka 1,800/=, wao wanaongeza gharama ya uzalishaji kwa gramu 31 ni dola 1,200; yaani wanaongeza bei, wanaongeza gharama ya uzalishaji kadiri bei ya dhahabu inavyoongezeka, kupunguza sehemu ya faida ili kuweza kukwepa kodi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi vitu viko wazi, lakini bahati mbaya sana ni kwamba, waliopewa dhamana ya kufanya hivyo, hawafanyi na hawafanyi kwa makusudi. Ilitakiwa Kanuni ziandaliwe kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hiyo, tangu mwaka 2010 mpaka leo Serikali imeshindwa kuandaa Kanuni kwa ajili ya kuratibu jambo hilo, sababu ni nini?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 kwenye Sheria hiyo hiyo, kilipitishwa Kipengele ambacho kinaruhusu Makampuni haya ya madini kwa sababu, yanakwepa kodi kutokana na kuficha takwimu zao, kutokana na kuficha mapato yao, yawe *listed* kwenye soko la mitaji pale *DSE, (Dar-es-Salaam Stock of Exchange),* lakini mpaka leo yamegoma.

Mheshimiwa Spika, Sheria ipo, lakini Wizara imeshindwa kuandaa Kanuni, ili kusudi haya Makampuni yawe *listed* pale. Yakiwa *listed* pale ni kwamba, mtajua sasa *transactions* zote ambazo zinahusiana na mgodi, kwa hiyo, *governance* ya mgodi itakuwa wazi, lakini pia faida itapatikana.

Mheshimiwa Spika, leo *TBL* Serikali, ina 4% tu, lakini *TBL* inaingiza kwenye Serikali fedha nyingi kuliko *Airtel* ambako *Airtel* tuna 40%. Hizi ni hesabu za darasa la pili tu kwamba, inawezekanaje Kampuni ambayo tuna hisa 4% iingizie Serikali zaidi kuliko kampuni ambayo tuna 40%? Ni kwa sababu, *TBL* imekuwa *listed* pale *DSE,* imekuwa *listed* kwenye *Stock Market,* lakini *Airtel* tangu mwaka juzi, tangu mwaka jana mpaka leo Serikali, mmekataa ku-*list* hisa zenu, sio zote hata 10% tu; lengo hapa mki-*list* pale kwenye Soko la Mitaji ni kwamba, hesabu zote za Kampuni zitafahamika, mnagoma nini? Sasa watu wakichachamaa, mnasema kwamba, hawa watu wana matatizo, sio kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo duniani kote, hata vinchi kama vya Sri-Lanka, ambavyo kimsingi vimekaa na vita muda mrefu, eneo la benki bado ni tatizo katika nchi hii. Nchi kama Sri-Lanka, wao benki zao zote, yaani *financial institutions* zote, benki na taasisi nyingine za fedha kama *insurance* zote zinakuwa *listed* kwenye Stock Market, lengo ni kuhakikisha kwamba, yale mabenki yanafanya majukumu ambayo yalikusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania leo ni nchi ambayo ina benki nyingi kuliko nchi zote za *SADC,* tuna benki 51, lakini huduma za kibenki ziko chini sana kwa sababu, mabenki mengi hayafanyi kazi za kibenki yanafanya ma-*deal* ya *money laundering;* wanasafirisha fedha tu hawa, ndio maana benki zinaongezeka, lakini huduma za kibenki zinashuka. Namna mojawapo ya ku-*control* hiyo hali, haya mabenki yote moja ya *condition* yawe *listed* kwenye *Stock Market* pale, ili kusudi tu-*own,* tumiliki hata 10% tu, hesabu zao zote zitafahamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Fedha inahusika pia na masuala ya ubinafsishaji. Hii nazungumza kwa mara nyingine tena kwamba, kama kuna maeneo tulifanya makosa na tunaendelea kufanya makosa na Serikali, inaendelea kufanya mikakati ya kuficha hayo makosa ni kwenye eneo la ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, wakati tunabinafsisha, moja ya malengo ya kuanzisha lile soko la hisa, ilikuwa ni kwamba, mashirika yote yatakayobinafsishwa yaweze kuwa *listed* pale hata kwa asilimia ndogondogo kwa lengo la ku-*manage* soko huria.

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka leo, tumebinafsisha mashirika takribani 320, lakini mashirika pekee ambayo yamekuwa *listed* pale ni mashirika saba tu, mashirika mengine yote yamegoma, yameigomea Serikali. Yamegoma kwa lengo la kuficha taarifa zao, ndio maana tunashindwa kufaidika na ubinafsishaji kwa sababu, haya mashirika yangekuwa *listed* pale, tungekuwa na mtaji mkubwa. Kwenye uchumi, *Stock Market* ndio *barometer* ya uchumi kwa sababu, watu wengi watashiriki pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inahusiana na Benki ya *NBC,* kwenye Kamati tulijadiliana pale. Benki ya *NBC* kuna madeni ambayo mpaka leo wanasema ni madeni kichefuchefu, takribani bilioni 60. Wakati wa utaratibu wa kutoa mikopo ile, watu wamekopeshwa kwa dhamana ambazo haziendani na mkopo aliochukua.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake *CHC* imeshindwa kurudisha madeni yale kwa sababu, mtu amekopa mkopo wa bilioni 10, ameweka dhamana ya milioni 10. Kwa hiyo, hata ukichukua dhamana yake haina maana yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, tunataka majina ya watu wote waliokopa *NBC* yaletwe Bungeni, kama ni Kampuni, Kampuni na wamiliki waletwe Bungeni hapa tujue. Maana kuna wengine ni matajiri wako mtaani, lakini kwa sababu mlikosea

wakati wa mchakato mzima wa utoaji wa mikopo, mpaka leo tunashindwa kuwakamata; bilioni 60 *is a lot,* nchi inashindwa kutengeneza madawati miaka 50, lakini kuna watu wanamiliki bilioni 60, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba kuishauri Serikali na Wizara hii. Bado kuna mashirika kadhaa takribani 40 ambayo bado hayajabinafsishwa, nawashauri ingawaje hamshauriki, haya mashirika yawe *listed* pale hata kwa asilimia kwenye *Stock Market.* Mnagoma nini? Mnafaidika nini? Haya ni maeneo muhimu sana ya ku-*manage* mapato ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla muda wangu haujaniishia, naomba nigusie jambo la Bandari. Katika maeneo ambayo kuna udhaifu mkubwa wa Serikali hii ni kwenye ku-*manage* mapato pale Bandarini. Kwanza kuna watu ambao wanapandishiwa bei, lakini pili, kuna watu ambao hawalipi kabisa; yaani kila kitu matatizo, wengine hawalipi na wengine wanapandishiwa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati tumezungumza pale kwamba, Serikali, ifanye uchunguzi madhubuti. Walifanya uchunguzi wa takribani wiki mbili tu, Serikali, imepoteza takribani milioni 900 kwa wiki mbili tu, sasa kwa muda mrefu, mpaka leo ni kiasi gani ambacho kimepotea, kama ni miaka mitano, wiki mbili milioni 900, miaka mitano inakuwaje?

**SPIKA:** Ahsante. Ulikuwa unasema mambo mazuri mpaka nimesahau saa. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa nimwite Mheshimiwa Kombo Khamisi Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Mansoor Hiran.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kupata nafasi. Nianze kwa kusema ukitaka kujua tabasamu la mtoto, basi mtilie kitu chenye ladha tamu

ndani ya kinywa chake. Lakini ukitaka uone uchungu wa mtoto, basi vile vile mtilie kitu kinachoitwa shubiri ndani ya kinywa chake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, kwa miaka 50 Watanzania sote tumemeza shubiri. Ni kwa sababu zifuatazo: Tanzania tuna madini ya dhahabu, almasi, *uranium, tanzanite,* lakini mapato tunayopata ni madogo zaidi kuliko mapato ambayo wanayapata wageni wale ambao wanamiliki migodi ile. Kwa hivyo, hii ni njia moja ambayo Watanzania tumelishwa shubiri kiasi ambacho Serikali yetu inakosa mapato ya kuweza kuendesha nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni suala zima la bandari. Niungane na wenzangu, pale Bandarini pana karibu ma-*container* 600; ma-*container* haya 600 bado mengine hayajalipiwa ushuru na wengine wanatafuta njia ya kuyahamisha kupeleka Uganda au Kenya kwa sababu, wameshindwa kulipia ushuru pale.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lazima tuwe na mfumo rafiki, utakaowezesha wafanyabiashara wakubwa pamoja na wafanyakazi wa *TRA,* waweze kushirikiana ili biashara zetu ziweze kwenda kwa uaminifu na kwa uadilifu.

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo linaturudisha nyuma ni ushuru. Biashara inayochukuliwa nje ikaletwa Tanzania, ushuru unaotakiwa kulipia pale ni mkubwa zaidi kuliko malipo unayolipia nje. Gharama unayochukulia nje ni ndogo zaidi kuliko ushuru unaotakiwa ulipie pale. Kwa hiyo, ni lazima Serikali, ilifikirie hili ili iweze kuingiza mapato.

Mheshimiwa Spika, la pili niseme kwamba Tanzania Mwenyezi Mungu katujalia kuwa na vyanzo vingi vya mapato lakini bado tunashindwa kuvitumia. Tunayo bahari kuu, bahari kuu Tanzania bado haijatumika kwa manufaa ya Watanzania. Wanaokuja kuitumia bahari kuu ni watu kutoka nchi nyingine. Wanaingia na vyombo vyao, wanachukua samaki, wanapeleka kwao, Tanzania haiingizi chochote. Wakati miaka kumi nyuma iliyopita, Chama cha Wananchi *CUF* kiliwahi kuishauri Serikali kwamba ijenge viwanda vya kusindika samaki na vilevile iweke kituo cha mafuta ambapo meli kubwa kutoka nje zitakapofika pale zitaingiza mafuta pale na vilevile itajulikana wamevua samaki wa kiasi gani, wana thamani gani na kitakachopatikana pale kitaingia Serikalini lakini mpaka leo hili halijafanyika. Hivyo basi, naomba ushauri utakaoonekana kwamba unamaana na utaleta tija kwa nchi, usiangaliwe kwamba unatokana na chama gani au unatokana na nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niseme kwamba ni kweli karibu 50% ya fedha za maendeleo zinazokwenda kwenye Halmashauri haziendi kwenye miradi ambayo imekusudiwa. Sasa basi, nasema hili kwa sababu haya yanatokana na baadhi ya Madiwani wetu na hata Wakurugenzi wao, baadhi yao hawana uelewa wa masuala ya fedha. Naomba kwa nguvu zote kwamba suala hili lifuatiliwe ili liweze kupatiwa ufumbuzi unaofaa ili fedha za wananchi zisipotee ovyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Serikali kutumia zaidi fedha kuliko kuzalisha. Hili la kutumia fedha zaidi kuliko kuzalisha ndilo linalopelekea Serikali yetu kutegemea zaidi wafadhili na wahisani kuliko fedha za ndani. Naiomba Serikali yetu tamko lake ililolitoa mwaka jana kwamba watapunguza matumizi litekelezwe kwa sababu kama tamko lile halikufuatwa na leo tukasema kama fedha hizi tunazipeleka kwenye *OC,* bado tutakuwa tunarudi kulekule nyuma ambako tuliisema kama fedha hizi hazitatumika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niseme kila mfanyakazi ajue kuwa ni mstaafu mtarajiwa na kama kila mfanyakazi ni mstaafu mtarajiwa, sote humu miongoni mwetu baadaye

tutakuwa wastaafu. Kuna baadhi ya Wabunge au wote wanapostaafu, akitimiza miezi mitatu utafikiria ni mzee wa miaka mia moja na hamsini. *(Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante. *(Kicheko)*

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, sikumaliza lakini nitapeleka kwa maandishi.

**SPIKA:** Ahsante. Nilikuwa nashangaa Mbunge anakuwa mstaafu au ameanguka sasa ndio na mwenyewe anaitwa mstaafu? Mheshimiwa Devotha Likokola atafutiwa na Mheshimiwa Mansoor.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Waziri na Watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, tumeona Wizara hii imeendelea kujitahidi katika kutekeleza majukumu yake na hasahasa kutuletea sera za kuangalia uchumi wetu lakini vilevile sera za kuangalia sekta ya fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kuangalia masuala mazima ya uchumi wetu, naomba kuishauri Serikali na kuisisitiza kwamba bado wananchi hawajaridhika na hali halisi ya uchumi. Wananchi wetu bado wana hali ngumu ya uchumi na kwa maana hii Serikali inatakiwa iangalie ni kwa nini wananchi hawa wanahangaika katika kukuza uchumi wao. Hali ya umaskini bado ipo na kwa maana hiyo, ni lazima Serikali ionyeshe dhamira ya dhati ya kuondoa umaskini wa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri ametuambia kwamba katika kuangalia masuala mazima ya sekta ya fedha, tutakuwa na idara ya kuendeleza sekta ya fedha nchini lakini ahadi hii Mheshimiwa Waziri alishaitoa tangu

mwaka jana. Tungependa kusikia leo, utekelezaji wake umefikia wapi, Idara hiyo imeshaundwa, Mkuu wa Idara hiyo ni nani na nini kimefanyika kwenye hiyo Idara? Haiwezekani tukaendelea na ahadi mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tuliishauri Serikali ishirikiane sana na taasisi ya *TAMFI* katika kuendeleza sekya ya fedha. Napenda kujua, wameshirikiana katika maeneo gani na kumekuwa na mafanikio gani katika kuendeleza sekta ya fedha. Pia napenda kujua Mheshimiwa Waziri na Wizara hii ina dhamira gani ya kuwatoa wananchi ambao wanatumia huduma rasmi za kifedha kutoka asilimia ngapi kwenda asilimia ngapi kwa mwaka huu ili tuendane na takwimu na tuweze kuhoji kiukamilifu.

Mheshimiwa Spika, bado tunamwomba Waziri, mwaka jana aliahidi mwaka huu angeleta Sheria ya *Microfinance* lakini hajaleta bado. Tunaomba afanye haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la *community bank,* nashindwa kuelewa, Serikali haizipendi *community bank* au wananchi hawapendi *community bank* kwa sababu gani wananchi wamehangaika. Ukiangalia humu ndani Wabunge ndiyo wamekuwa ma-*promoter* wa *community bank,* Wabunge ndiyo wanahamasisha *SACCOS,* Wabunge ndiyo wanahamasisha vikundi vya kuweka na kukopa, hii ni kazi ya Wabunge? Ni nini *role* ya Serikali katika ku-*promote community bank* na ime-*promote community bank* ngapi kipindi cha mwaka jana mpaka mwaka huu. Hii ni aibu. Haiwezekani Waheshimiwa Wabunge wanahangaika kwenda kutafuta vibali vya *community bank* na katika haya ninayosema nina ushahidi. Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakihangaika na wananchi wao katika kuwatengenezea mifumo ya fedha, haiwezekani, naomba Serikali mchukue jukumu lenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie benki za biashara, nashukuru zimetoa mikopo kwa wafanyabiashara wakubwa, wamefanya kazi nzuri lakini bado kuna

changamoto. Masharti ya kufungua akaunti katika beni hizi ni magumu sana na wananchi wanahangaika sana lakini bado kuna foleni kubwa sana kwenye benki hizi! Hivi ni nini kifanyike ili wananchi waweze kupata huduma kwa urahisi katika benki hizi? Inapofika mwisho wa mwezi kwenye Wilaya zetu ukienda kwenye benki utaona huruma, haiwezekani jamani! Hawa wananchi wa Tanzania tayari wana miaka hamsini ya uhuru, hawawezi wakakaa kwenye foleni kama miaka ya zamani lazima tuendane na sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie benki ya Twiga. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri mwaka jana aliisaidia benki hii lakini tunataka aongeze msaada wake kwa sababu benki hii sasa imekuwa ni mkombozi mkubwa sana na imesaidia sana vikundi na wananchi wa ngazi ya chini. Tunaomba benki hii ifanye huduma zake kama benki nyingine. Ni benki ambayo inaweza kusaidia sana kwa sababu kwanza ni benki ya Serikali na ili ionyeshe mfano wapeni nguvu. Ukienda kwenye benki ile na mimi nawahamasisha hata Wabunge waende kwenye benki ile huduma ni nzuri sana lakini bado hawana nguvu ya kutosha. Aidha, nafurahi kwamba Serikali pia imeangalia benki ya Posta na naomba mipango hiyo iendelee.

Mheshimiwa Spika, bado naomba kuzungumzia suala la *rural financial strategy.* Mimi sielewi *strategy* hii iko wapi na nani anai-*hold* maana yake siku zote tunaambiwa kuna mkakati wa kuendeleza masuala ya fedha kwa wananchi hususan vijijini, huo mkakati mbona hauonekani, mbona hautekelezeki? Tunaomba kwa kweli tujitahidi.

Mheshimiwa Spika, *BOT*. Pamoja na kwamba ukimwangalia Mheshimiwa Gavana Ndulu, ana nia ya dhati ya kuendeleza masuala ya *housing microfinance,* masuala ya *financial literacy* lakini *speed* imekuwa ndogo. Naomba Benki Kuu iongeze *speed* yake kwa sababu huduma za fedha bado ni tatizo kubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, tuna suala zima la *TRA,* wanafanya kazi nzuri lakini bado kwa kipindi hiki kumekuwa na

malalamiko makubwa sana hasa kwa wananchi wanaotoa mizigo yao bandarini. Kumekuwa na tatizo la *system,* mara mtandao, mara nini na wananchi wengi mizigo imebaki bandarini na kwa maana hiyo ukienda madukani sasa hivi bei zimepanda na mbaya zaidi wafanyabiashara wetu wamechanganyikiwa. Wale wafanyabiashara wanafanya zile biashara kwa kuchukua mikopo na kwa maana hiyo ukiwacheleweshea muda wao wa kutoa mizigo bandarini, wanaongezewa riba, *charges* mbalimbali, kwa hiyo, tunawachanganya wafanyabiashara wetu. Wafanyabiashara wa nchi hii wakichanganyikiwa, kodi haitapatikana, pesa haitapatikana na Serikali itakuja kuchanganyikiwa, haiwezekani, ni lazima wafanyabiashara wetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mansoor.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri na Manaibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya na watendaji wake wote. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Kamishna wa *TRA* kwa kazi nzuri anayofanya na timu yake.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia mambo machache yafuatayo. Kwanza, ni deni la Taifa. Nimeona kwenye kitabu cha Wizara, wamelenga sana kulipa madeni ya nje tu, madeni ya ndani naona kama hawayatambui

kabisa. Madeni ya ndani ni mengi, yako ya Walimu, wazee wastaafu, Halmashauri zinadaiwa madeni makubwa, naomba wajipange kuyalipa madeni hayo. Naomba niikumbushe Wizara kwamba hawa watu wa ndani wanaotudai ndiyo watu waliotupa kura za kuja huku. Kwa hiyo, naomba hizo kura tusiziharibu, tunataka kurudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze tena kwenye Sheria ya Manunuzi. Sheria hii inapandisha bei ya bidhaa zinazonunuliwa na Halmashauri zetu kwa kiasi kikubwa. Mimi nashauri Wizara itoe bei elekezi ya vifaa muhimu ambavyo vinanunuliwa na Halmashauri zote kwa mfano simenti, nondo na kadhalika. *EWURA* wanatoa bei elekezi ya mafuta, nao wangeanzisha kitu kama hicho, itatusaidia kupunguza gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TANESCO.* Wizara hii imetoa ruzuku ya mabilioni ya fedha kwa ajili ya kuendesha mitambo ya *TANESCO* na kununua mafuta mazito. Naomba Wizara itoe taarifa rasmi Bungeni, imetumia shilingi ngapi nje ya bajeti iliyopitishwa na Bunge hili mwaka huu? Pia nimeona kwenye bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka kesho, fedha walizoziomba hazitoshi, kwa hiyo, mwaka kesho pia wamepanga kutumia fedha nje ya taratibu ya kupitishwa na Bunge. Naomba Waziri atupe maelezo kuhusu masuala haya.

Mheshimiwa Spika, manunuzi ya magari. Kila Wizara, Idara na Taasisi hununua magari kivyake bila kuwa na *central system* ya kulinganisha bei. Pia kwenye manunuzi ya magari wanaingia kwenye mtego wa kupata *warranty* ya miaka mitatu mpaka mitano, sasa wale wauzaji wa magari wanapata faida kwenye vipuli vya kuuza kwa miaka mitatu mpaka mitano. Unaweza ukanunua gari kwa Sh.200,000,000/= lakini matunzo ya gari lile kwa miaka mitano inakuwa Sh.600,000,000/= mpaka Sh.800,000,000/= kwa sababu miaka ile mitano ya *warranty* wale watu hawana masharti, wanauza vipuli kwa bei wanayotaka wao. Mimi nashauri Serikali inaponunua magari pia iongee na wale wauzaji wa magari

watoe orodha ya vipuli vitakavyohitajika kwenye miaka mitatu ya *warranty* na bei zake, washindaniwe pia kwenye bei zile za vipuli ili ujue gari lile moja litakugharimia shilingi ngapi kwenye miaka minne ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *China Tanzania Logistic Centre,* huu mradi ulioletwa na Wizara ya Viwanda na Biashara andiko tumelipata kutoka kwa *EPZ* ambalo linazungumzia mambo mazuri sana. Mimi nashauri Wizara ya Fedha, ifanye uchambuzi wa kina kuhakikisha kwamba hiyo *China Tanzania Logistic Centre* haitaathiri viwanda vyetu vya ndani na haitaathiri mapato ya nchi. Pia kuna sentensi moja wameweka kwenye hilo andiko ambayo mimi sielewi vizuri ningeomba Wizara inieleweshe, wanasema kwamba huo mradi utatoa ajira ya moja kwa moja ya zaidi ya watu 25,000. Sasa mimi nashangaa kwenye hekari 60, ajira ya watu 25,000 zitatoka wapi, naomba andiko la kina liletwe ili tuweze kufahamu vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nashukuru kwa kuniokolea muda ili niweze kutangaza yafuatayo:-

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba mchana huu watakuwa na kikao katika ukumbi namba 227.

Tangazo lingine, nadhani watalitawanya maana wengi wameondoka, kwa miaka mingi tumekuwa na utaratibu wa kutembelewa na Wabunge wa Mabunge mengine na sisi pia tuna utaratibu wa kutembelea Mabunge ya wenzetu. Wabunge wachache wanaweza wakajiweka pamoja wakawa rafiki wa Bunge lingine lakini utaratibu haujawekwa vizuri, tunaendelea kuratibu hilo.

Tuna urafiki kati ya Wabunge wa Bunge la Uingereza, *The House of Commons* na sisi na kwa utaratibu ule ndiyo iliyosaidia hata kufuatilia zile fedha za rada. Mhimizo ulitokana

na Wabunge wanachama hapa na Wabunge wa Wanachama *House of Commons*. Kwa hiyo, wale wakaishinikiza Serikali yao mpaka tukarudishiwa zile fedha.

Juzi mimi nilipata mwaliko wa kwenda kushiriki kwenye Bunge la Oman, kwa sababu nilikuwa na shughuli nyingine akaenda Naibu Spika na mwisho wa mwezi huu, Spika wa Oman anakuja hapa. Moja ya kitu ambacho walikubaliana alipokuwa kule, kuundwe urafiki wa Wabunge wa Bunge la Tanzania na wale wenzetu wa Oman. Kwa hiyo, wale ambao wangependa kuwa katika kikundi hicho cha urafiki na Wabunge wa Oman, leo hii kutakuwa na kikao, nafikiri ukumbi wa Msekwa, ukumbi wa Msekwa inaelekea kuna mikutano mingi, mtajua huko huko, naomba mkitoka hapa muende kule ambapo huko mtaelekezwa mambo mengi zaidi. Tutaorodhesha na nchi nyingine ambazo zinatafuta urafiki huo ili na sisi tuwe na vikundi vya namna hiyo.

Hivyo hivyo kuna vyama vingi vya Wabunge vinaanzishwa hapa, hivi sasa kuna Chama kingine wanaanzisha karibuni, hakija-*take root,* kinaitwa Chama cha Wabunge wenye Kupambana na Magonjwa ya Kuambukizwa, watatoa maelezo yao. Vyama hivi vinatambulika katika Mabunge yote, ni vyama visivyo vya Serikali, ni kama *NGO's* lakini za Bunge.

Kwa leo, naomba wale wanaotaka kuwa na urafiki na Wabunge wa Oman waende katika ukumbi wa Msekwa, watawakuta wataalam pale watawaelekeza.

Sina matangazo ya ziada, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wale wote ambao walikuwa wanastahili kupata nafasi ya kuchangia, walimalizika asubuhi. Kwa hiyo, kwa sasa nitaanza kuwaita

wasaidizi wa mtoa hoja. Nitaanza na Naibu Waziri, ni *revenue or what*, ni dakika ishirini ishirini, Waziri ni dakika arobaini.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Aidha, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhanah Wataala* ambaye ametuwezesha jioni hii ya leo kukutana tena katika kukamilisha ungwe yetu hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema chochote, naomba kuunga mkono hoja iliyotolewa hapa na Waziri wa Fedha na vilevile naomba kuwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii. Napenda kuwataarifu kwamba kutokana na muda, sote kwa pamoja hatutaweza kujibu hoja zote ambazo zimetolewa lakini tutajitahidi kujibu kadri inavyowezekana na nyingine tutajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kujibu hoja ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Devotha Likokola. Hoja zake zote zilikuwa za msingi sana na kama mwanamke mwenzangu, nampongeza sana kwa kuweza kutetea wanawake kujiwezesha kiuchumi, kupitia *VICOBA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza lilikuwa, ni vipi Serikali inashirikiana *TAMFI*. Kwanza napenda kumwambia, kama tulivyokuwa tumetoa miadi katika Bunge lililopita kwamba Wizara ya Fedha itaanzisha Idara ya *Microfinance* ambayo pamoja na mambo mengine sasa itaanza kushughulikia hivi vikundi vidogovidogo mfano SACCOS pamoja na *VICOBA*, vyenyewe kwa mfano kama *VICOBA* vinajiona havina mahali pa kukaa *particularly*, lakini tunasema sisi Wizara ya Fedha sasa tunaanzisha hiyo Idara na muundo upo katika hatua za mwisho kukamilika. Kwa hiyo, ni taratibu tu ambazo tunakamilisha na mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara hii itakuwa iko tayari pale Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, tuwataarifu tu akina mama ambao wako kwenye *VICOBA,* mama yao atakuwepo pale na sisi sote tutakuwa tunashirikiana katika kuhakikisha kwamba kuna mazingira mazuri ya *VICOBA* kuweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alikuja na swali lingine kuhusu takwimu za watumiaji fedha nchini. Sisi kama Serikali tunaelewa na tunapata machungu sana kuona kwamba kwa jitihada ambazo tunaweka, maana kama tunaweka *policies* nzuri, tunaweka sheria nzuri kushajihisha *community banks*, *commercial banks* ziweze ku-*enshrine* nchi yetu, *target* hasa ni yule mwananchi wa kawaida. Hata hivyo, kutokana na mazingira yenyewe ya kibiashara, kutokana na *complicated system* za *finances*, bado kabisa jamii kubwa ya Watanzania haikuweza kuwa *captured* katika *formal financial system*. Kutokana na ripoti ya *FINCOP* inatuambia kwamba, *only* 12% ndiyo wapo kwanza katika mfumo rasmi wa kibenki. *This is real very small amount* lakini 4.3% ndiyo ambao wako kwenye hizi *microfinance* ambazo ziko rasmi *particularly* lakini 27% *only* ndiyo wako katika asasi ambazo ziko rasmi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaona jamii iliyo maskini ambayo inataka kujikwamua kutoka katika umaskini, asilimia 56% haina *access* na hizi *financial institutions. This is real depressing* ukilinganisha na jitihada nyingi sana ambazo zimefanyika, tunaweka mikakati madhubuti kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na hizi huduma za kibenki. Tunakotaka twende sasa, *coming* 2015, tunaweka sasa mikakati madhubuti kwa kushirikiana na wewe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote, *target* yetu sisi kama Serikali tufikie 50%. Kwa hiyo, tushirikiane sote kwa pamoja maana hii siyo kazi ya Serikali, Serikali ni *structure*, lakini sisi sote tunajukumu hili la kusajihisha sasa watu wawe wanapata hizi *financial access*, lengo, waweze kujikwamua kiuchumi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Likokola, tunakwenda kwenye 50% *by* 2015 na hii inakwenda sambamba na kuwawezesha wanawake, maana inategemea na huduma nzuri za kijamii. Kama hujajenga barabara nzuri, mwanamke akatoka akafanya biashara yake, *we can not reach there*. Kama hujaweka miundombinu mizuri ya maji, mwanamke awe na *access* na *clean* and *safe water* ili muda wake mwingine aweze kufanya vitu vingine, *we can not reach there*. Kwa hiyo, hii yote inategemea sana na kuimarishwa

kwa sekta nyingine lakini hiyo ni ndio Sera ya Serikali hii ambayo inaongozwa na CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna *issue* ya *community banks,* zipo lakini bado, hii ndio sasa tunaweza tuka-*link* na ile *small percentage* ya watu bado hawajawa na *access* ya *finance*. Ni *role* ya Serikali *in one part* lakini Mheshimiwa Mbunge, Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane kwa pamoja, ku-*promote community banks*, *whatever it takes,* Serikali tumeweka miundombinu lakini tusaidiane sote kwa pamoja sasa kuhakikisha kwamba *community banks* zinafanya kazi. Ni *role* ya Serikali kuweka *policies*, kuweka sheria, kuwezesha *community banks ku-enshrine*. Vilevile hili jambo sasa la ku-*promote community banks*, ni letu sote sisi kama Serikali lakini pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Nakuomba Mheshimiwa Likokola, kwa vile umekuwa mstari wa mbele, maana mpaka unajulikana kama mama *VICOBA,* kama vile tunavyokuita mama *VICOBA*, basi ushirikiane na sisi kuhakikisha kwamba tuna-*promote community banks. (Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni benki za biashara, kweli hili limejitokeza, benki za biashara ziko mbali sana na mwananchi wa kawaida. Hili tunaliona na kwa vile huko tunakokwenda tunataka kila mtu aingie, basi tutahakikisha kwamba benki za biasahara nazo zinafanya liwezekanalo kuhakikisha kwamba mwananchi wa kawaida anapata mkopo, tena kwa masharti ya kawaida. Nalo hili tutashirikiana na sekta nyingine, kwa sababu benki ya biashara, kwa sababu na wao wanafanyabiashara, kama unakwenda huna zile *credible documents*, kidogo wanaanza kuingia wasiwasi, anahangaika, mwananchi mwingine mwenyewe anahangaika, *simply* kwa sababu kuna vitu vingine ambavyo vinakosekana. Tuwashajihishe wananchi wajitokeze kupata vitambulisho kwa sababu kina *advantage* nyingi *including* hii ya kupata fedha. Kwa hiyo, hili haliji peke yake, tunaweza tukaweka miundombinu, pengine *interest rates* zikashuka, lakini kwa sababu kama mwananchi mwenyewe hana *details*, hana *identity*, hii benki ya biashara kama inavyoitwa inakuwa haina *confidence* ya kuweza

kumkopesha huyu mwananchi. Hili nalo liwe linafanyiwa kazi na ninyi Wabunge pamoja na sekta nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo yalikuwa mengi, labda niondoke hapo, niende kwenye hoja ya Mheshimiwa Rajab. Yeye alileta kwa maandishi lakini bado hoja zake zilikuwa zina msingi na amenitishia hapa kwamba anaweza akazuia mshahara wa Waziri. Kwa upande wake yeye aliona kwamba Pemba *ASYCUDA++* haifanyi kazi**,** *I do know for how long*, lakini takwimu nilizokuwa nazo mimi *ASYCUDA++* Pemba inafanya kazi. Tatizo lipo na siyo kwa Pemba tu, tatizo lipo kwa mfumo huu wa *ASYCUDA++* kutokana na *network*. *Sometimes* inawezekana biashara inakwenda lakini *network* iko chini sana. Kwa hiyo, hilo lipo, inawezekana Mheshimiwa wakati unatembeatembea, wakati uko huko Jimboni na kwingineko, *timing* ilikuwa ndiyo hiyo. Hapa ninazo *data* ambazo tumefanya *transaction* kule Pemba, kwa Machi 2013, kulikuwa na *transactions* tano na hizi zote zimefanyika kwa kutumia hii *ASYCUDA++* lakini Aprili kulikuwa na *transaction* nne, *ofcourse* kutokana na mfumo mzima wa biashara Pemba hauko *active* kuliko Unguja au kulinganisha na Dar es salaam. Hata Juni hii, sasa hivi tumeweza kufanya *transaction* moja kwa kutumia *ASYCUDA++*. Kwa hiyo, nataka nikupe *confidence* Mheshimiwa Mbunge kwamba *ASYCUDA++* inafanya kazi Pemba isipokuwa kuna matatizo ya mtandao. Hili tunalirekebisha kwa sababu tunachotaka sisi wafanya biashara wawe wanapata *access* kwani *ultimately* ndiyo Serikali anapata mapato, kwa hiyo, tunataka kila kitu kiende sawa lakini sisi tutalichukua na tutalifanyia kazi. Kimsingi linafanyika, ni *techinichal problems*. Tunachokifanya sasa kupitia *TRA* wameagiza ku-*increase* ile *bandwith* ambayo pengine tu *sometimes* transactions zinakuwa kubwa na zile *system* haziwezi kubeba.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine na ambayo imetolewa na wengi ni kuhusiana na shughuli za *CHC*. Kama sote tunavyojua Azimio la kukamilisha shughuliza za *CHC* ni Azimio la Bunge, ni mpaka Juni 2014. Baada ya hapo, Ofisi ya Msajili wa Hazina, itachukua kazi ambazo zitakuwa zimebakia. Hata hivyo, nalo hili lilikuwa linakwenda pamoja

na kuimarishwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina. Naomba kuchukua fursa hii, kuwafahamisha kwamba Msajili wa Hazina ili aweze kufanya kazi zake kwa nafasi, kwanza, tumerekebisha Sheria mwaka 2010, lakini lingine ni kwamba tumemtoa katika lile jengo letu la Wizara na tumempeleka katika jengo la *CHC* na awe anafanya kazi zake kule *coming July first*. Hiyo itategemea Waheshimiwa Wabunge pia, tupitishe bajeti hii ili kumwezesha sasa Msajiri wa Hazina aweze kufanya kazi zake kama zinavyostahiki.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, *organization structure* pia tayari imeshakamilika chini ya mamlaka husika *(PIC)* lakini muundo nao vilevile umewekwa kwa ajili ya kuhudumia masuala ya urekebishaji na ubinafsishaji wa mashirika ya umma, kazi ambayo imekuwa ikifanywa na *CHC* lakini muundo sasa wa *TR* umewekwa *in such a way* kuweza kufanya kazi hizo. Vilevile katika *TR* ndani yake kuna kitengo hicho cha kushughulikia uperembaji wa mashirika ambayo yamebinafsishwa, uperembaji maana yake ni *monitoring and evaluation*. Tumepata jengo hilo kama nilivyokuarifuni, Wizara sasa inakamilisha zile taratibu za kuchukua baadhi ya watumishi na kuwapeleka kule. Kwa hiyo, hivi ndivyo ambavyo Serikali imeweza ku-*strengthen capacity* ya *TR* kwa sasa hivi, kuweza kufanya kazi zake kama ambavyo inatakiwa lakini vilevile kujitayarisha kwa ajili ya kuchukua kazi ambazo zitakuwa zimeachwa na *CHC* wakati muda wake utakapokuwa umekamilika. Kwa hiyo, tunajitahidi, nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge kwamba mtupitishie bajeti yetu hii ili sasa kuweza kufanya kazi zetu kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala jingine, ambalo limetolewa na Mheshimiwa Said Mussa Zuber. Yeye kwa maoni yake, anasema kwamba hii *speed* ya *Big Result Now,* aliita PEMANDU, *initiative* yetu sisi kama Tanzania tumesema *Big Result Now (BRN),* hakuna kusuasua. Nataka kumhakikishia kwamba tumeji-*commit*, tuna-*determine*, tutafanya kazi. *Big Result Now* kuna *initiative* nyingi, kuna *innovation* nyingi kule zimetokea katika sekta ambazo tumezipa *priority* mfano kilimo, elimu, maji hata *resource*

*mobilization*. Kwa hiyo, *Big Results Now* haijaja tu yenyewe kimyakimya, labda kama ndiyo sawasawa na mikakati mingine, imekuja pamoja na kuangalia mapato zaidi, wapi tutapata kwa ajili ya kutekeleza yale ambayo tunayaweka kule. Siyo hivyo tu, uzuri wa *Big Result Now*, inaanisha *implementation time frame*, nani atafanya hii kazi na mwaka gani itakuwa imekamilika. Kwa hiyo, hii ni *initiative* nzuri, tui-*support* na kuna baadhi ya Mawaziri hapa tayari tumeshasaini hata zile *performance contract* na kila Waziri ameshaji-*commit* kwamba hiki ndicho ambacho kitafikiwa kwa muda ambao umewekwa kutokana na ile mipango kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna *issue* nyingine ya Mheshimiwa Zuber kuhusiana na tawi la *NMB* Zanzibar, hili tumeliona. Mimi mwenyewe *at one point in time* nilikuwa *NMB* pale, hali ilikuwa mbaya yaani utaweza ukafananisha pale *NMB* Zanzibar kama uko Muhimbili, watu wamelala chini, watu wengine wapo mpaka saa saba usiku wanakuambia wanasubiri kuchukua mishahara yao. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Zuber pamoja na Waheshimiwa Wabunge tutalifuatilia kwa sababu mimi mwenyewe nimeliona, tutahakikisha kwamba kunafunguliwa matawi mengine pale Zanzibar, hali ni mbaya. Mimi binafsi nimekwenda, nimetoka machozi kuona mtu anasubiri pesa yake mwenyewe lakini unam-*intimidate* kiasi gani? *It was real very bad, that scene was very bad,* kwa hiyo, hili tutalifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *issue* ya hawa ambao wamefungiwa leseni, kesi zimekuja kwetu sisi na ukiwasikiliza *TRA they have a point*, ukisikiliza na hawa wengine, *they have a point*, lakini kikubwa hapa mimi nachotaka kuwaambia hawa watu wa *clearing and forwarding agents* kwamba hukumu zilizotolewa za kufungiwa kama wana maelezo zaidi na kutokana na wengine ambao tumezungumza nao wana maelezo zaidi, basi wafanye *appeal* katika hii *Tax Appeal Board,* sisi kama Wizara ya Fedha tutawafahamisha hao *TRA or whoever* wakitaka maelezo zaidi lakini waende waka-*appeal*. Kama itaonekana kwamba hawana makosa, nina imani kwamba hizi kazi zao zitafunguliwa maana *TRA* wanataka mapato, tunabanwa hapa ndani tunataka

mapato. Kwa hiyo, *the only thing* ni hao watu kufanya biashara lakini niwahakikishie kwamba hata wakufungulia, kutakuwa na *tight management* kuhakikisha hata hizo biashara wanazozifanya zitakuwa zinafanywa katika uangalizi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na Sheria na Sera za *Microfinance,* wengi wameelezea hapa, bado hazijawa tayari. Tunawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Sera ya *Microfinance* iko katika hatua za kukamilika chini ya *BOT* na hii tutaifanya *agency* kwa sababu *microfinance institution* nyingi ndipo wananchi wengi wa kawaida wanapoponea. Tukienda kwenye *commercial bank*, hatuingii hapo, kwa hiyo, nadhani hili ni jambo ambalo tutalifanya haraka kuangalia hasa wananchi nao wanapata *financial inclusion.*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala lingine kuhusiana na wananchi wa kawaida kutoelewa faida ya *Capital Market and Security Authority* ama *Dar es Salaam Stock Exchange,* wengi hawaelewi, ni kweli hatukatai, lakini sisi hili tunalichukua kama Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba elimu inatolewa kupitia vyombo vya habari tena kwa lugha nyepesi kabisa ambapo mwananchi anaweza akaelewa kwa sababu wako wananchi wana pesa lakini hawajui...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kutokana na muda, naomba kuunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Naibu Waziri mwingine, nikisema aliyemaliza wa kwanza wewe utakuwa wa pili, sasa niseme mwingine tu, karibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa

kunipa nafasi hii kuchangia hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, napenda na mimi vilevile kutoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa maoni yao, nasaha na maelekezo waliyotupatia wakati wa kuchangia. Napenda vilevile kuwashukuru kwa miongozo mingi ambayo imetolewa na kwa kweli tumeiona kuwa itakuja kutusaidia katika kuboresha shughuli zote zinazoendana na Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, napenda kuchangia maeneo machache kwa sababu muda hautaruhusu, nitaomba yale ambayo tutashindwa kuyajibu sasa hivi, tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nianze vilevile na mimi kwa suala zima la mashirika yaliyobinafsishwa/ kuorodheshwa katika soko la mitaji. Mashirika yaliyobinafsishwa/kuorodheshwa kwenye soko la mitaji ili kuongeza ufanisi wa kodi na masuala mengine yote yanayoendana na uwekezaji wa aina hii, ni kweli yapo mashirika mengi ambayo mpaka sasa hivi tayari yameshaorodheshwa katika soko la mitaji. Kuna yale ambayo bado na ambayo Serikali ina hisa zake, uamuzi wetu ni kuwa sisi kama Serikali kwanza, tutamalizia kanuni zinazohitajika kwa ajili kuwezesha zoezi hili kufanyika halafu sisi tutatoa mfano kwa kupeleka zile hisa zetu sisi Serikalini kwenye soko la mitaji. Naamini hiyo itachochea na wengine kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuwa kwa nini uchumi wa Tanzania haupunguzi umaskini pamoja na kuwa unakuwa, jibu lake kwa kweli, ni kuwa uchumi wa Tanzania umekuwa ukikua kwa wastani, lakini pamoja na hayo inaonekana kuwa kiwango cha umaskini hakijashuka vya kutosha, japo kinashuka. Tathmini zinaonyesha kuwa tatizo kubwa liko katika vijiji na sehemu ambazo wako watu wengi ambao ndiyo tunategemea umaskini huu uondolewe kwa haraka zaidi. Hii yote ni kutokana na miundombinu na taasisi nyingi bado hatujaweza kuzifikisha kule. Hii haina maana kuwa Serikali

haijataka kufanya hivyo kwa sababu tunaelewa wazi maana nzima ya kuondoa umaskini kwa Watanzania wengi ambao wako vijijini na hii itakuwa ndiyo njia pekee ya kufanya nchi yetu ifikie lengo la kuwa nchi ya mapato ya wastani mwaka 2025. Suala lingine ni kuhakikisha kuwa elimu ya kujitegemea katika masuala ya ujasiriamali, ufundi ambavyo vitawezesha wananchi wengi zaidi kujitegemea kwa kujiajiri katika sekta mbalimbali hasa kilimo, zitaendelea kutolewa kwa bidii zaidi ikiambatana na uwezeshwaji wa mitaji ambayo tumetoka kulizunguza sasa hivi, ikiambatana na utoaji wa pembejeo mbalimbali na vitu mbalimbali vitakavyowezesha wananchi wengi zaidi kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, suala la mifuko sikutaka kuliingilia sana kwa sababu Mheshimiwa Saada amelizungumzia lakini labda nije kwenye suala lingine lililozungumzwa kuhusiana na masuala ya Mifuko ya Hifadhi kuwa kwa nini na yenyewe haijiorodheshi au haitangazi kwenye magazeti na vyombo vya habari taarifa za uendeshaji wao. Nilitaka kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa mfumo wa Mifuko ya Hifadhi ni tofauti na mabenki, kwani Mifuko haitengenezi faida bali inatengeneza ziada ya kulipa mafao ya wanachama wao. Hivyo bila kuwa na mfumo wianifu katika Mifuko yote, hatutaweza kuwawekea taratibu za kutangaza kwa sababu kwanza inaweza ikapeleka *message* tofauti kwa wananchi wasipoweza kuelewa kwa nini Mfuko huu unaoneysha hivi na mwingine unaonyesha hivi. Vilevile sheria iliyotengneza Mifuko hii, haiwawajibishi Mifuko kutoa taarifa kama mabenki yafanyavyo kwa kila *quarter*. Kwa sababu gani? Mfuko hata ungeweza kutoa taarifa kwa kila *quarter*, isingekuwa tofauti kubwa sana, kwa sababu Mifuko inaenda kwa umri wa wachangiaji, sasa *quarter* moja na *quarter* nyingine bado mwaka ni uleule. Kwa hiyo, bado taarifa utakazozipata pale hazitasaidia sana kuonyesha tofauti.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja kwamba kwa nini Mifuko ya *PSPF* na *PPF* isiwekeze katika maeneo ambayo yanazalisha ajira kama vile reli na bandari. Kuwekeza katika reli na bandari kwa Mifuko inawezekana au isiwezekane kufuatana na jinsi gani uwekezaji huo utaleta faida kwa

Mifuko. Ikumbukwe kuwa Mifuko ni fedha ambayo imewekwa pale kwa ajili ya kuja kulipa mafao. Uwekezaji katika reli na bandari, inaweza ikachukua muda mrefu sana kiasi kwamba ikaathiri ulipwaji wa mafao. Hata hivyo, hii haizuii kwa Mifuko kama vile *PSPF* na *PPF*, kuangalia na kutathmini kama inawezekana kuwekeza katika sekta hizo. Vilevile kama mnavyojua kuwa Mifuko hii tayari inawekeza katika sekta nyingine nyingi ambazo zinazalisha ajira, zinazalisha faida ambayo inawezesha kulipa mafao kwa wanachama wao.

Mheshimiwa Spika, nataka kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii yaani *SSRA*, kwa kushirikiana na Benki ya Tanzania, tayari imetoa miongozo ya uwekezaji tangu mwaka 2012, ambayo imezingatia maeneo yenye tija kwa wanachama wake kwa manufaa ya kiuchumi na hii ikiwa ni pamoja na kutengeneza ajira. Kwa hiyo, kuna miongozo maalum ambayo inawasaidia hata wao wenye Mifuko kutambua ni maeneo gani ambayo ni salama zaidi kwao kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala vilevile kwamba fao la elimu liwe katika Mifuko yote kama lilivyo *PPF*. Vilevile kulikuwa kuna suala lililofuatana na hilo, juu ya fedha za wanahisa wa *NICOL*, je, ziko salama? Napenda kujibu hili kuwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji ya Dhamana imechukua hatua mbalimbali kulinda maslahi ya wawakezaji wa Kampuni ya *NICOL*, ikiwa ni pamoja na kuzuia kuuza hisa ambazo Kampuni ya *NICOL* imewekeza *NMB* baada ya kubaini kuwa fedha ambazo zingepatikana zingewekezwa katika maeneo ambayo yanayohatarisha maslahi ya wanahisa. Kwa hali hii, tayari inaonyesha kuwa fedha hizi ziko salama. Mali ya wanahisa katika Kampuni ya *NICOL*, ziko salama na kwa hisa za *NMB* peke yake thamani ya hisa imekua kutoka shilingi bilioni 4.6 tangu mwaka 2005 na kuwa shilingi bilioni 52 kufikia Juni, 2013. Hili ni ongezeko kubwa ambalo linaonyesha wazi kuwa amana hizo ziko salama.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia kuna hoja kuwa Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na Watanzania

kuendelea kununua hisa na kuwekeza kwenye makampuni mbalimbali hapa nchini hasa baada ya uzoefu huu wa *NICOL* na *TOL*. Napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa Serikali ingependa kuwahakikishia wawekezaji na wananchi kwa ujumla kuwa hali ya Masoko ya Mitaji ni shwari na hatua stahiki za kulinda maslahi ya wawekezaji, hususan katika *NICOL*, zimechuliwa na Serikali kupitia *Capital Market and Securities Authority*. Soko la Hisa limekuwa likionyesha kuboreka kwa vigezo muhimu vya kupima ufanisi wa soko, hususan thamani ya hisa zote, yaani *market capitalization,* zilizoorodheshwa. Wastani wa bei umekuwa ukipanda kila mwaka. Kampuni ya *TOL*, imekuwa ikiimarika na wameanza kupata faida, shilingi milioni 119 tangu 2011. Vilevile kuna kampuni zinazofanya vizuri kama vile Kampuni ya Bia, Kampuni ya Sigara, Kampuni ya Swisport, Kampuni za Saruji za Tanga na Twiga, Benki za *CRDB*, *NMB* na Benki ya Wananchi wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa kuna hoja ambayo ilitolewa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa la kampuni za kigeni kufanya huduma za Uwakala wa Forodha. Kwa mujibu wa Sheria za Forodha za Afrika ya Mashariki, taratibu za kutoa leseni za Uwakala wa Forodha haubagui aina ya kampuni au wamiliki wake. Utaratibu uliopo sasa unawataka wanaoomba leseni kufanya mtihani wa Uwakala wa Forodha. Waliofuzu hupewa leseni baada ya kukidhi mahitaji mengine ya Forodha pamoja na kuwa na ofisi ya uhakika. Hata hivyo, tumezingatia ushauri na tutaangalia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki usajili wa makampuni hayo ili kulinda maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hili la *TRA,* nitamwachia Mheshimiwa Waziri mwenyewe atakapokuja kuzungumza atalijibu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa vilevile na suala la Sheria ya Manunuzi ya Umma. Rasimu ya Kanuni za Ununuzi wa Umma imekamilika. Hata hivyo, utekelezaji wa Kanuni hizo, unasubiri kukamilika kwa marekebisho ya baadhi ya Sera na Sheria za sekta nyingine ili kuwa na uwiano katika utekelezaji

wake. Maeneo ambayo yanapaswa hufanyiwa marekebisho ni pamoja na Sera ya Sheria ya *PPP*, hususan katika ushughulikiaji wa zabuni zenye maombi *(unsolicited bids),* yale maombi ambayo yanakuja yenyewe tu, watu wanajitoa tu kuwa wanataka kuja kuwekeza nchini, kwa hiyo, wanaleta maombi yao. Sasa inabidi nayo pia yasimamiwe ili kuhakikisha kuwa hawa wanaoleta maombi kama haya, je, wao ndiyo ambao watakidhi ubora na usalama wa uwekezaji nchini kote kama vile ambavyo wangekuwa wengi wameomba kuwekeza katika nchi yetu. Eneo lingine ni Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011, kuhusu uteuzi wa wajumbe Mamlaka ya Rufaa za Zabuni na masuala yahusuyo mwingiliano wa maslahi kati ya wahusika wa zabuni. Hivyo, Serikali imeona umuhimu wa kufanya marekebisho hayo kwanza ndipo utekelezaji wa Kanuni mpya za Ununuzi uanze.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ambayo imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kiasi, juu ya hali ya kifedha ya Mfuko wa *PSPF*. Katika kuhakikisha kwamba suala la madeni ya Mfuko wa *PSPF* linapatiwa ufumbuzi, Serikali imeunda Kamati inayochambua mapendekezo mbalimbali yaliyopo na kushauri hatua sahihi ya kulipa deni hilo. Mapendekezo yaliyopo hadi sasa baina ya *PSPF* na Serikali ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ilipe deni la mchango ya awali la shilingi bilioni 716 kwa awamu kwa kipindi cha miaka 10.

(ii) Serikali iongeze kiwango cha michango kufikia asilimia 25 ili kuendelea kupunguza nakisi ya Mfuko.

(iii) Serikali itoe hati fungani maalum *(special long term interests bond)* ili kuweza kufikia nakisi iliyopo.

(iv) Serikali kulipa michango ya kabla ya 1999 kwa watumishi wastaafu katika miaka mitano.

(v) Serikali ihamishe baadhi ya hisa zake mbalimbali ili kufidia nakisi ya *PSPF*.

(vi) Serikali ihamishe baadhi ya umiliki wa majengo kwa Mfuko wa *PSPF* ili waweze kuutumia kwa ajili ya kuzalisha mapato.

(vii) *PSPF* kubadili fomula ya ukokotoaji wa makato.

Mheshimiwa Spika, hayo ni mambo ambayo yamependekezwa lakini bado hayajapitishwa kwa sababu lazima yafanyiwe kazi kuona jinsi gani yatafaa kutumika. Nataka kuonyesha tu kuwa tayari hatua zinachukuliwa katika kushughulikia hili suala la kifedha la *PSPF*.

Vilevile kulikuwa kuna masuala ya kuangalia jinsi gani ambavyo *PSPF* watawekeza katika miradi inayozalisha kwa muda mfupi badala ya ile ya muda mrefu ambayo inazuia fedha muda mrefu katika sehemu moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii iliyoundwa imeanza kazi yake na imeandaa hadidu za rejea na kikosi kazi kinajumuisha wajumbe kutoka Wizara ya Fedha, Kazi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Msimamizi wa Mifuko (*SSRA*) na Benki Kuu ya Tanzania. Kamati hii itaangalia pia madeni ya Serikali yanayohusu mikopo iliyotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa ajili miradi ya maendeleo ya Serikali ili kuangalia usalama wake na jinsi gani ambavyo itaendelea kusimamiwa vizuri. Aidha, Serikali inatekeleza hatua za kulipa madeni ya *PSPF* na hadi sasa shilingi bilioni 30 zilizokasimiwa katika bajeti ya mwaka 2012/13 zipo katika mchakato wa kulipwa na vilevile malipo yaliyoahidiwa kwa mwaka ujao wa fedha shilingi bilioni 50 na zenyewe pia zitaendelea kutolewa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee katika suala hilohilo kwa masuala ya wastaafu. Kulikuwa kuna suala la mafao ya wastaafu na maswali kuhusu wafanyakazi wanaostaafu na kulipwa mafao ya kustaafu na Wizara ya Fedha. Wanaolipwa mafao hayo na Wizara ya Fedha ni wale wote waliostaafu kabla ya tarehe 1 Julai, 2004, tarehe ambayo Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma *PSPF* ulianza kulipa; Wanajeshi na Usalama wa Taifa

wanaoendelea kulipwa mafao ya kustaafu na Wizara ya Fedha kwa sababu wao siyo wanachama wa Mfuko wowote wa Hifadhi ya Jamii; watumishi wenye mamlaka mbili za ajira yaani walioajiriwa Serikali Kuu na kuhamia Serikali za Mitaa au Mashirika ya Umma na sehemu za ajira ya Serikali Kuu; wenye ajira za mikataba; viongozi wa Kitaifa Wastaafu; Marais; Makamu wa Rais; Mawaziri Wakuu; Viongozi wa Kisiasa; Wabunge; Wakuu wa Mikoa na Wilaya; Maafisa wa Serikali ambao pensheni yao ni asilimia 80 ya mshahara wa maafisa wa ngazi zao walioko madarakani na ambao ni wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya jamii na hulipia ile tofauti ya pensheni kati ya inayolipwa na Mfuko husika na asilimia 80 ya mashahara wa walioko madarakani.

Mheshimiwa Spika, Maafisa wanaolipwa pensheni ya asilimia 80 ya maafisa wa ngazi zao walioko madarakani viongozi wa kitaifa wastaafu; Majaji wastaafu kuanzia Julai, 1999, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Mstaafu (*CAG*); *Inspector General* wa Polisi Mstaafu; Kamishna Mkuu wa Magereza Mstaafu na Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu. Wastaafu wanaolipwa na Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma, ni watumishi wenye ajira ya kudumu na malipo ya uzeeni katika mamlaka ya ajira ya Serikali Kuu waliostaafu kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, sambamba na suala hilo, kulikuwa pia kuna suala la kima cha chini cha pensheni cha Sh.50,114 kinacholipwa kuwa ni kidogo na kuwa hakikidhi mahitaji muhimu ya mstaafu. Serikali imekuwa ikiboresha kima cha chini cha pensheni kila hali ya uchumi ilipokuwa ikiruhusu na itaendelea kuboresha kima cha chini cha pensheni. Serikali itaboresha kima cha chini cha pensheni katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 kwa kuzingatia uwezo ulipo sasa. Kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza katika hotuba yake, pensheni kwa wastaafu inalipwa kwa vipindi vya miezi mitatu, mitatu, ambapo pensheni ya miezi miwili hulipwa mapema katika kila kipindi kwa lengo la kuhakikisha wastaafu hawapati shida.

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa na masuala ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na upungufu wake kuwa bei zimekuwa zikipandishwa sana wakati tenda zikitumika na kushauri kuwa Serikali iweke bei elekezi. Napenda kujibu haraka haraka kuwa, Serikali imechukua hatua kadhaa katika kuimarisha ununuzi wa umma, lengo ni kuzidi kudhibiti na pia kuwezesha kufanyika kwa ununuzi wenye tija kwa taifa. Katika Bunge la Novemba, 2011, Sheria mpya ya Ununuzi ilipitishwa na utekelezaji wa Sheria hiyo utapunguza sana mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria ya Ununuzi ya 2004. Moja ya hatua ambazo zimechukuliwa na ambazo zimesisitizwa na Sheria mpya, ni matumizi ya mikataba inayosimamia ununuzi wa bidhaa na huduma mtambuka (a *common used items)*. Katika utaratibu huo, bidhaa zote zilizoorodheshwa kama bidhaa mtambuka, huwekewa bei elekezi. Ili kufanikisha hilo, Serikali imeanzisha Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini *(GPSA)* ambapo moja ya majukumu yake ni kusimamia mikataba ya bidhaa na huduma mtambuka.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa mtoa hoja, una dakika 40. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kuwashukuru Naibu Mawaziri wangu kwa majibu yao mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, nachukua nafasi hii, kuwashukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Fedha, Kambi ya Upinzani kwa mawazo yao na mwisho nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kushiriki mjadala huu ambao umetusaidia sisi Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwashukuru hao, nichukue nafasi hii vilevile kuwashukuru Waheshimiwa

Wabunge wote waliopata nafasi ya kuzungumza ambao walikuwa 10. Hii ni kujumuisha pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, pamoja na muwasilishaji wa hoja ya Upinzani. Vile vile nachukua nafasi hii kuwashukuru wale wote waliowasilisha maoni yao kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Viwanda. Katika mapendekezo yake yote, kuna pendekezo moja zito ambalo nafikiri lipewe nafasi ya kulisemea. Ametaka Serikali tueleze kwa kifupi au tunavyofahamu tatizo la makontena lilivyo bandarini, kwa sababu limeathiri mapato ya Serikali kama Kamati ilivyoeleza. Kwa sababu ya uzito wa hoja, nami nachukua nafasi hii kupitia Bunge hili na vivyo hivyo kufikisha ujumbe huu kitaifa kueleza nini Serikali imekifanya baada ya kusikia tatizo hilo na hali ikoje. Ni kweli, kuanzia tarehe 8 Aprili mpaka 31Mei, *TRA* walifanya kazi ya ukaguzi wa makontena, baada ya kuwa na taarifa za ukiukaji wa kodi. Mpaka dakika hii kontena ambazo zimekuwa *profiled* ni 522 na ambazo zimechekiwa ni 498 na zilizoonyesha kuwa na mizigo tofauti na *declaration* ni 188. Hizi kontena 188 zimekusanywa kodi ya Sh.1,249,672,076/=, ni kodi ya ziada tuliyoikusanya baada ya ku-*check* hizo kontena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa *exercise* hii, inaonyesha kwamba, kuna ukweli wa aina hii kwamba kumekuwa na ukwepaji wa kodi kwa kipindi fulani lakini *TRA* wameifanya hiyo kazi na kupatikana kodi hiyo ambayo ingepotea kwa ukwepaji.

Mheshimiwa Spika, sasa katika kukagua makontena, *criteria* ambazo zinatumika ziko tano, ya kwanza, wanaangalia aina ya mzigo ulivyoelezwa kwenye *declaration*. La pili wanaangalia nchi ambako mzigo huo unatoka *(country of origin).* Tatu, mhusika mwenye mzigo. Nne, nani anafanya ile *clearing agent, identity* ya *clearing agent* halafu tano, wanalinganisha na historia ya mwingizaji wa mizigo. Hizi *criteria* tano zinasaidia kubaini uharaka wa ku-*screen container.*

Mheshimiwa Spika, lakini matatizo ambayo yamejitokeza yamelega katika maeneno manne. Makontena haya ambayo nimesema ni 188 yaliyobainika kwamba yalikuwa na mizigo ambayo ilikuwa si sahihi kama ilivyoandiwa, hoja moja ni kwamba kulikuwa na hitilafu katika *declaration*, ilikuwa ni tofauti na hali halisi ya mzigo iliyokuwa ndani ya kontena. Pili, makontena mingine yalikuwa na mizigo ya ziada. Tatu makontena mengine yalikuwa na aina tofuti na mzigo ulivyojazwa kwenye makaratasi na nne, wajazaji wengine wali-*declare* thamani ndogo ya mzigo kuliko hali halisi ya mzigo wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kulijulisha Bunge hili kwamba ni aina gani ya mali zilizokithiri katika makontena yaliyobainika yamekiuka taratibu. Aina ya mizigo ni kama, kwanza, *CPU* yaani *computers,* kinakuwa *declared* kitu tofauti ndani unakwenda kuzikuta *computer*. Pili, *mosquito nets* ambazo zinakuwa zimeandikwa kwamba huu ni mzigo wa *mosquito nets* kumbe ni mzigo mwingine ndani ni kwa sababu *mosquito nets* hazichajiwi. Tatu, ni *monitor* za *computers*. Nne, ni nguo mbalimbali. Tano, ni *solar panel.* Sita, ni aina ya mizigo ya *alminium*. Hii ndiyo historia iliyojitokeza katika kukagua makontena hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua gani? Serikali baada ya kufanya kazi tumegundua la ziada kwamba kuna udanganyifu mwingine unatumia mtandao yaani *fake documents* kwa ajili ya kufanya *declaration* na *clearing agents* wengine sio wema.

Mheshimiwa Spika, karatasi hii ninayoionyesha kama mfano ni aina ya mihuri mbalimbali ambayo imebainika kuthibitisha kwamba wamefanya *clearing*. Sasa *documents* za namna hii zikiwasilishwa, nyingine ni *fake*. Kwa hiyo, nina sampuli za ofisi mbalimbali zinazoonyesha mihuri yao inayotumika kwa ajili ya kufanya kazi ya udanganyifu. Serikali tumechukua hatua ya kufuatilia na kubaini ofisi hizi na chanzo cha matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, pia katika hili Serikali tunaelekeza kwamba utaratibu wa *direct release* ya mizigo usimamishwe. Watu wote wanaoagiza mizigo tunataka wakaguliwe ili Serikali ipate kitu kinachostahili. Serikali haitaki mtu aonewe lakini inataka kila mtu alipe anachostahili kulipa kwa kodi ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona niliseme hilo kwa kirefu kwa sababu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Viwanda na Biashara ameielekeza Serikali itoe maelezo na haya ndiyo maelezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo kuna hoja za Kambi ya Upinzani. Namshukuru Mheshimiwa Silinde ameorodhesha vitu vingi na Serikali tumechukua nafasi ya kuvifanyia kazi na kuja na majibu. La kwanza, ametaka Serikali itoe ufafanuzi kwa kiwango gani takwimu za uchumi wa kitaifa zinaonyesha kwamba uchumi unakwenda vizuri lakini umaskini unapungua kidogo sana au inaonekana hakuna *impact*. Hoja hii ni sahihi. Takwimu za ukukaji wa uchumi yaani kwa *GDP average* kutoka 2000 mpaka 2012, *GDP* imeongezeka kwa wastani wa kati ya 6.9% mpaka 7%, ni *growth rate* lakini umaskini kwa wastani toka 2000 mpaka 2012 umepungua kwa 2.1% tu. Kwa hiyo, ukiangalia hilo, utagundua kwamba kweli *notion* hii, hakuna uwiano ulio na msukumo unaofanana katika ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa umaskini. Tunahitaji sisi kama Serikali kuja na sera na mikakati mipya kusaidia namna ya kupunguza umaskini. Hii ni hoja ya ukweli na Serikali tumeifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tumefanya nini? Serikali tumekuja na kitu tunasema *financial inclusion,* maana yake tunaweka mikakati ya kuangalia walio wengi ambao ni 75% ya wananchi wa Tanzania wako vijijini, hawa ndiyo hawaguswi na ukuaji mkubwa wa uchumi na ukuaji mkubwa wa uchumi umeonyesha kwamba upo katika *transport sector, construction* na *financial sector* lakini *sector* hizi zinaajiri watu wachache ukilinganisha na sekta inayoajiri walio wengi, sekta inayoajiri walio wengi ni sekta ya kilimo na kwa wastani katika miaka 10, sekta ya kilimo imeongezeka kwa 4.3%. Kwa hiyo,

*growth rate* ya kilimo imekuwa ndogo ukilinganisha na *growth rate* ya sekta nyingine na ndiyo maana walio wengi wakawa wameachwa kidogo nje ya mfumo wa ukuaji wa haraka.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali tumeangalia na tumechukua majukumu ya kuangalia kwamba tuboreshe sekta ya vijijini. Tunaangalia namna gani tutapeleka pembejeo za kilimo kwa kuboresha na kuimarisha utengaji wa mafungu katika bajeti ili shughuli hii iweze kuwa na *impact* kwa wananchi walio wengi. Tunaangalia namna ya kuboresha barabara vijijini, tunaangalia uwekaji wa umeme ili usambae haraka na tunaangalia namna tutakavyosaidia upatikanaji wa maji vijijini. Wananchi wetu wakiwa na vitu ambavyo ni vya muhimu katika maisha na kuwasaidia waweze kuendelea kiuchumi basi kilimo kitapanda. Kwa hiyo, kwa kuchukua hatua hizo, tuna hakika tatizo hili litatatuliwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Silinde alichosema ni sahihi na sisi hayo ndiyo majibu ya Serikali kwamba tunalifanyia kazi suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Silinde amesema kwamba kwa hali tuliyonayo *TRA* inavyokusanya fedha kwa kusema kweli kulingana na hali halisi kama misamaha ya kodi ingeondolewa au ingepunguzwa, makusanyo ya kila mwezi walau yangefikia *one trillion*, hapa pana changamoto kidogo. Mimi sipingani sana na hoja hii, nasema kuna changamoto kwa maana mbili. Kwanza, sasa hivi, tunachokusanya kwa wastani kwa kila mwezi kinaelekea kati ya shilingi bilioni 750 mpaka 800, hayo ni makusanyo ya *TRA*. Kwa hiyo, anachosema Mheshimiwa Silinde kwamba tungeweza tukafikisha *one trillion* inawezekana tukitatua changamoto, kwa mfano, changamoto hii tuliyosema ya makontena bandarini.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni misahama ya kodi kama alivyosema Mheshimiwa Silinde lakini changamoto ni kwamba Waziri wa Fedha kwa kawaida hana mamlaka mwenyewe kusamehe kodi, kodi anazozisamehe Waziri wa Fedha ni zile mlizoidhisha ninyi

Waheshimiwa Wabunge kwa kupitia Sheria. Waziri wa Fedha anachokifanya ni kuitazama sheria inamruhusu asamehe kitu gani alichoidhinishiwa na Bunge kwa mujibu wa sheria iliyopo. Kwa hiyo, sisi Serikali tumefanya maamuzi ya ku-*review* ile sheria na italetwa hapa Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge muamue ni maeneo gani yapunguzwe ili Waziri wa Fedha asiwe na mamlaka ya kuitumia sheria ile apendavyo. Kwa hiyo, mpunguze madaraka ninyi Waheshimiwa Wabunge mliyonipa kwenye sheria. Kwa hiyo, hili nasema ni changamoto lakini tutashirikiana wote kwa pamoja kuangalia maeneo ya kupunguza ili tuweze kuwa na misamaha mingi isiyotuletea tija katika uchumi, sheria yenyewe tunairekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, msemaji wa Kambi ya Upinzani anasema kwamba tuliagizwa sisi Serikali kuiagiza *PPRA* ifanye ukaguzi wa manunuzi ya mafuta ambayo kwa maelezo yake ni kwamba Serikali inatumia *1.4 billion* kwa siku kwa ajili ya kulipia mafuta kuendesha umeme. Hoja ya Kambi ya Upinzani ni kwamba tupeleke *PPRA* wakakague wathibitishe kitu gani kinatokea kule. Serikali tumeshaagiza na *PPRA* kwa taarifa niliyonayo wanafanya ukaguzi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine kutoka Kambi ya Upinzani ilikuwa inasema kwamba mfumo wa mabenki Tanzania umekithiri wizi yaani kinachotokea katika mabenki ni wizi na kwamba wizi unaotokea katika mabenki unatokana na mfumo mbovu wa *banking system*. Tumelichunguza suala hili na kwa taarifa tuliyonayo ni kwamba mifumo ya benki ya utendaji iko imara. Mimi mwenyewe nimefanya kazi katika *banking system* kwa miaka mingi kwa hiyo ninasema kile ninachokifahamu na nilichopata mpaka leo lakini wizi unatokea katika mabenki, umekuwa unapitia katika *ATM*. Benki Kuu hivi ninavyozungumza tayari wameshachukua hatua kwa ajili ya kwenda kwenye *version* nyingine ya *Euro System ATMs* ambazo zipo imara, *reliable* zinazoweza zikapunguza wizi wa kutumia *ATM*. Kwa hiyo, nawaomba kwa pamoja tuwe na subira wakati Benki Kuu inalifanyia kazi hili kwa *ATMs* zilizoonyesha zina hitilafu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la Kambi ya Upinzani ambalo wametushauri vizuri ni kwamba tutazame namna ya kuondoa kesi nyingi za Serikali ambazo ziko Mahakamani ambazo zinatuletea gharama kubwa tuka-*settle out of Courts.* Hoja ina *both ways* yaani ina *merits* na *demerits*. *Merits* ni kwamba ikiwa Serikali ina *weak point* basi ni vizuri tuka-*settle out of Court* kwa sababu kuendelea ndani ya Mahakama kunakuwa na hasara kwa sababu hakuna *prospect* ya Serikali kushinda lakini pale tunapokuwa na *strong points* kama Serikali ,tukiondoa tuka *settle out of Court,* inakuwa ni hasara kwa Serikali na kwa wananchi wanaoi-*finance* Serikali iwepo. Kwa hiyo, ni *case to case,* kama tuna hoja kubwa au hatuna hoja ushauri huo unakuwa mzuri.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine kutoka Kambi ya Upinzani imehoji kwamba ni muda sasa *microfinance institutions* hazina *regulatory framework,* ni kweli mpaka dakika hii tulitarajiwa kuwa tungekuwa tumefikia hatua kubwa lakini hivi ninavyozungumza Benki Kuu wanaendelea kutengeneza sera itakayoongoza utayarishaji wa kanuni ili kanuni za *microfinance* ziweze kutolewa. Kwa hiyo, hili ndiyo jibu lake.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyoletwa na Wabunge wa Upinzani ni kwamba wanaona kuna umuhimu wa Mifuko ya Jamii iweze kutoa *report* kila *quarter* kama vile inavyofanywa na mabenki ili wananchi waweze kuwa na upeo na kuelewa hali ya usalama wa fedha zilizokuwa katika hizo hifadhi za jamii. Kwa kusema kweli na mimi naona kuna *strong point* lakini tatizo tulilonalo kwa dakika hii ni kwamba mabenki tuliyonayo yanatumia mifumo tofauti kwa hiyo *frequency* ile ya kutoa *publications,* hatuwezi tukatumia sheria ile ambayo inalazimisha mabenki ya-*publich on quartely basis* tukaitumia kwa ajili ya Mifuko hiyo mpaka Sheria iliyoanzisha Mifuko hiyo iweze kusema hivyo. Lingine ni kwamba *actuarial valuation,* nazo zinafanyika na zile ndiyo huwa zinatupa *indicator* ya hali halisi ya *risk* au hapana katika Mifuko hiyo. Pia lingine ni kwamba kulingana na Sheria ya Mifuko, *audit report* zinafanyika mara moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na maswali mengine ambayo kwa muda uliopo na kwa umuhimu wa kuwa majibu ambayo yanakidhi matakwa ya Waheshimiwa Wabunge tumeyaweka kimaandishi ambapo yatakapokuwa yamemalizika, tutaomba tuwasilishe kwa Waheshimiwa Wabunge. Kuna hoja nzuri na kuna maswali mengi na mengine ndiyo kama hivi yamebaki lakini tunaonelea kwamba ni hekima tuyaweke kimaandishi ili Waheshimiwa Wabunge baadaye waweze kuwa na kitu kilichokamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue nafasi kuwaomba Waheshimiwa Wabunge muiunge mkono bajeti hii ili ipite, nikae vizuri kutengeneza fedha niwape ili muweze mkanufaika na bajeti. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba mniunge mkono kuidhinisha bajeti hii na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono na umetuachia dakika ishirini na tano. Tunaendelea na hatua inayofuata.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kif. 1001 *Administration and Human Resource Management* … ……Tshs. 38,088,142,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kif. 3001 *Public Debt Management* … … .Tshs. 350,000,000/=
Kif. 3002 *Expenditure Management* ... Tshs. 25,400,000,000/=
Kif. 3003 *Financial Management* … …. Tshs. 45,905,681,200/=
Kif. 3004 *Financial System* … … … … ......Tshs. 4,757,360,800/=
Kif. 3005 *Sub Treasury Arusha* … … ….........Tshs. 170,000,000/=
Kif. 3006 *Sub Treasury Coast* … … … …........Tshs. 149,000,000/=
Kif. 3007 *Sub Treasury Dodoma* … … …... Tshs. 339,000,000/=
Kifl. 3008 *Sub Treasury Iringa*… … … …........Tshs. 160,880,000/=
Kif. 3009 *Sub Treasury Kagera*… … … ….... Tshs.151,000,000/=
Kif. 3010 Sub *Treasury Kigoma* … … ….......Tshs. 160,000,000/=
Kif 3011 *Sub Treasury Kilimanjaro* … … …....Tshs.167,000,000/=
Kif. 3012 *Sub Treasury Lindi* …… … … …......Tshs.156,000,000/=
Kif.3013 *Sub Treasury Mara*…… … … .......…Tshs.152,000,000/=
Kif 3014 *Sub Treasury Mbeya*… … … ….........Tshs.154,000,000/=
Kif 3015 *Sub Treasury Morogoro* … … ….......Tshs.205,400,000/=
Kif. 3016 *Sub Treasury Mtwara* … … …..........Tshs.177,100,000/=
Kif 3017 *Sub Treasury Mwanza* … … …........Tshs.160,000,000/=
Kif. 3018 *Sub Treasury Rukwa* … … … …......Tshs. 159,000,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3019 *Sub Treasury Ruvuma* … … …Tshs.150,000,000/=

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Hapa tupo *Sub Treasury Ruvuma,* kuna kile kifungu 220900 *Training Foreign,* naona mwaka jana hawakutengewa fedha za *training* nje ya nchi na mwaka huu pia hawajatengewa fedha lakini maeneo mengine naona wametengewa. Ni kwa nini watumishi wa *Sub Treasury Ruvuma* hawapewi fedha na wao kwenda kujifunza mambo huko nje?

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu 220900, *Training Foreign*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA SALUM MKUYA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ruvuma bado tuna wafanyakazi ambao ni wapya na kama unavyoona tunaanza kwanza kuwa-*training domestically* kabla hatujaenda kuwa-*train outside* ili wawe na *capacity* kwanza ya kufanya kazi za pale ndani.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko Yoyote)*

**MWENYEKITI:** Naomba msiniandikie barua, mimi nipo kazini hapa. Tunaendelea. *(Kicheko)*

Kif. 3020 *Sub Treasury Shinyanga* ….........…Tshs. 149,000,000/=
Kif. 3021 *Sub Treasury Singida* … ….......... …Tshs.150,000,000/=
Kif. 3022 *Sub Treasury Tabora*… … … ......…Tshs.152,000,000/=
Kif. 3023 *Sub Treasury Tanga*… … … ….......Tshs.151,000,000/=
Kif. 3024 *Sub Treasury Manyara*… … … … .Tshs.151,000,000/=
Kif. 4001 *Local Government Finances* ........Tshs.426,000,000/=
Kif.7001 *Pension and Gratuity* … … ..........…Tshs.629,250,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 50 - Wizara ya Fedha**

Kif. 1001 *Administration and HR Management* … Tshs.7,898,819,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ni mshahara wa Waziri. Wizara hii ina mafungu mengi hivyo basi nitawapeleka kwenye Kanuni ya 101(4) ambapo vyama vinavyohusika vimependekeza majina yao ambao ni Mheshimiwa Zungu, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa Masoud Omar, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed. Mheshimiwa Tundu Lissu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri lakini nianze kwa kusema kwamba Mheshimiwa Waziri amejibu maswali yake vizuri sana, ingekuwa ni vizuri na Mawaziri wengine wakajifunza kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Mgimwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Akili ni nywele kila mtu ana zake, hee! *(Kicheko)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita tu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri na jambo ambalo nataka ufafanuzi kutoka kwake ni suala la deni la Taifa. Katika aya ya 17 ya hotuba yake, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba malipo ya deni la Taifa hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu yalikuwa shilingi trilioni 1.666 ambapo kati ya hizo shilingi bilioni 214 zilikuwa ni kwa ajili ya deni la nje na shilingi trilioni 1.453 zilikuwa ni deni la ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hiyohiyo kwenye *paragraph* ya 127, Mheshimiwa Waziri anazungumzia tena deni la Taifa na hapa anatuambia kwamba matumizi katika deni la Taifa hadi kufikia Aprili 2013 yalikuwa shilingi trilioni 2.227 kati ya makadirio ya shilingi trilioni 2.736. Kwa hiyo, tuna maneno mawili, tuna ndimi mbili nilizozizungumza jana, tuna shilingi trilioni 1.666 matumizi ya deni la Taifa na tuna shilingi trilioni 2.227 matumizi ya deni la Taifa. Sasa tumetumia shilingi ngapi kulipa deni la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni muhimu sana kwa sababu katika hotuba nzima ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha hajatwambia hivi tunadaiwa shilingi ngapi kama nchi? Haya malipo ya matrilioni haya, hizi ni fedha nyingi sana, tunahitaji Mheshimiwa Waziri atwambie kwanza, kati hizi ndimbi mbili, tufuate ulimi upi? Tufuate ulimi wa kushoto shilingi trilioni 1.66 au tufuate ulimi wa kulia shilingi trilioni 2.227?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Waziri ni muhimu alieleze Bunge hili Tukufu hivi haya madeni makubwa

yametokana na mikopo ipi? Bunge hili lipate *a complete breakdown* ya wanaotudai ili tuweze kujua hivi tumewakopa vitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nitaondoa shilingi kama Waziri atageuka na kuleta majibu ya ajabuajabu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI**: Kwa hiyo, unayo majibu tayari. Waheshimiwa Mawaziri m-*note* wanayozungumza na inawapeni nafasi kujiandaa vizuri. Mheshimiwa Zungu.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kila Taifa linapokaribisha wawekezaji linakuwa na lengo kunyanyua uchumi katika Taifa lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge sisi hatukusikii vizuri labda uhame.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa linapokaribisha wawekezaji lina lengo la kutaka wawekezaji wawekeze lakini Taifa nalo lifanikiwe. Kuna Sheria za *stock exchange* ya nchi yetu na makampuni haya ya simu yalitakiwa yote yasajiliwe ili sasa uchumi upenyezwe kwa wananchi wetu lakini sheria hii toka ianzishwe bado haijafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano mdogo tu kwa nchi jirani ya Kenya na Kampuni ya Safaricom ambayo sasa hivi imetangaza namna walivyopata faida kwa wananchi kumiliki kampuni ile na namna Serikali ilivyopata faida kuwemo kwenye kampuni ile. Nataka kujua tu, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri ata-*implement* sheria hii na kuhakikisha makampuni yote haya ya simu yanaingizwa kwenye *stock exchange* ili sasa wananchi na wao waweze kununua hisa katika makampuni haya na baadhi ya pesa hizi badala ya kusafirishwa kwenda nje zitumike kwa wananchi kama walivyofanya nchi nyingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Betty Machangu.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilibinafsisha Mashirika ya Umma na mengi yao yalikuwa ni viwanda na mashirika haya yaliwekwa kwenye Shirika Hodhi la *Consolidated Holding Corporation* na tumekuwa tunaambiwa hapa na Serikali kila leo kwamba kwa makampuni yale ambayo hayakuendeleza vile viwanda, Serikali ita-*revoked title* ya vile viwanda lakini mpaka leo hakuna kinachofanyika na badala yake Serikali inatueleza kuhusu *Consolidated Holding Corporation* kumaliza muda wake mwaka kesho na Hazina kuchukua kazi zake. Tunachohitaji sisi ni ajira kwa vijana wetu, kwa nini inakuwa vigumu kwa Serikali ku-*revoked titles* ili watu wengine waanzishe hivyo viwanda vijana wetu waweze kupata ajira. Naomba Serikali ieleze Taifa kwa nini hizo *title* za hawa watu waliochukua viwanda ambavyo hawaviendelezi hawazi-*revoke,* kuna matatizo gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali iliamua kwa dhamira nzuri tu kuondoa suala la ukusanyaji kodi ya majengo kutoka katika Halmashauri na kuzipeleka *TRA* kwa lengo moja la kuweza kupata ufanisi. Kutokana na hali ilivyo sasa hivi, Halmashauri zetu nyingi kwa kweli zimepungukiwa na mapato yake yanayotokana na hii *property tax* na ufanisi unaonekana kulegalega chini ya *TRA*. Naomba kujua kipindi cha mpito cha *TRA* kukusanya hizi *tax* kitamalizika lini? Naomba Waziri anipe ufafanuzi, wamejipangaje kurejesha mfumo huu katika Halmashauri zetu ili ziendelee kupata mapato yake katika njia nzuri?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nassib Omar.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nilimweleza Mheshimiwa Waziri kuhusiana na wizi ambao unafanyika *TRA* kwa Kampuni ya za *Forwarding and Clearing*. Wafanyakazi wa TRA hutumia *password* za makampuni haya

na kuwapa watu binafsi na kuweza kuingiza magari ndani ya nchi bila kulipa ushuru. Mfano halisi ni Kampuni ya Kisiwani *Enterprise* ambayo imefungiwa toka mwaka 2009. Wafanyakazi wa *TRA* waliohusika badala ya kuachishwa kazi walitawanywa na bado waendelea na kazi. Vilevile kesi hii ipo Polisi na Mheshimiwa Waziri kwa kweli hakulitolea ufafanuzi mzuri. Kwa hiyo, namtaka Mheshimiwa Waziri anieleze lini kesi hii itamalizika kwa sababu sasa hivi ni zaidi ya miaka minne na bado wanapigwa danadana huku na huku. Nyaraka na vielelezo vyote wameshapewa Wizara na TRA lakini bado halijapatiwa ufumbuzi. Kwa hiyo, naomba nipate ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa suala hili sikupewa maelezo mazuri itabidi nizuie shilingi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Unazuia, unatoa? Haya twende kwa Mheshimiwa David Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilihoji kwa nini Serikali isichukue hatua za ziada kufuatia wanaodaiwa na benki ya *NBC* kiasi cha takribani shilingi bilioni 60 ambazo kwa mujibu wa taarifa ya *CHC* iliyopewa dhamana ya kukusanya madeni hayo ni kwamba deni hilo halilipiki limewekwa kwenye orodha ya madeni chefuchefu. Sasa kiasi cha shilingi bilioni 60 ni kiasi kikubwa sana. *CHC* wanasema kwamba watu hawa ambao wanadaiwa tatizo ni kwamba dhamana walizoziweka wakati kuchukua mikopo ni kidogo ukilinganisha na mkopo waliouchukua kwamba mtu amechukua mkopo wa shilingi bilioni 10 wakati dhamana iliyotumika ni shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata kauli ya Serikali, moja imechukua hatua gani kuhusu hao ambao walikopa na ni matajiri wangeweza kufilisiwa katika namna nyingine. Pili, kwa watumishi waliokuwa *NBC* kwa sababu ni jinai, wamechukua hatua gani kwa watumishi ambao walitoa mikopo kiholela kiasi hicho na kuliingizia Taifa hasara?

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naomba kuuliza Serikali pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali kwa kupitia *TRA* kukusanya mapato na kukusanya kodi mbalimbali, ni lini sasa Serikali itakaa na wadau, lakini pia kubadilisha sheria na kuiangalia upya Sheria ya Manunuzi ambayo inadidimiza uchumi wa nchi hii? Katika sheria ile kuna masuala mawili. Moja, ni ile *short list* ya wale wazabuni, wale wachache wanaobaki ambao wanaruhusiwa kuhudumia Halmashauri zetu au Serikali huwa wanaungana na wanaweka bei maalum. Pia katika bei za huduma wanazotoa na bidhaa ambazo wanaleta Serikalini unakuta zile bei ni mara mbili au mara tatu au zaidi ya ile bei ambayo ipo sokoni. Sasa tungekuwa na Sheria ambayo italinganisha bei za sokoni na ile bei ya huduma inayotolewa, tutaweza kuwa na akiba kubwa ya fedha na ile kasi ya makusanyo na matumizi tukiibana vizuri uchumi wetu utakua sana. Sehemu kubwa tunayopoteza uchumi wetu ni kwenye hiyo sekta ya manunuzi. Ni lini sasa Serikali itakaa na wadau mbalimbali pamoja na Wabunge na kuiangalia upya Sheria hiyo ya Manunuzi ili tuweze kubana matumizi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naomba nipate uhakika Mheshimiwa Nassib Omar, unaposema kuna kesi iko wapi, *TRA*, Mahakamani au wapi?

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kesi bado wanayo Polisi haijaenda Mahakamani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri maelezo. Naomba mtajibu kwa kutaja majina yao.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA SALUM MKUYA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nami nijikite hapohapo kwa suala la Mheshimiwa Nassib. Tulipotoka hapa tumekwenda kulifuatilia hili suala ambalo amelieleza...

**MWENYEKITI:** Sauti haitoki.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA SALUM MKUYA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotoka hapa, tulikwenda

kulifuatilia suala hili na tumeona kwamba hawa *Kisiwani Enterprises,* kweli walifungiwa na katika maelezo yao kulikuwa na maelezo ya kwa nini walifungiwa na wao wenyewe wameweza kujitetea kwa kiasi kikubwa sana. Huko nyuma walikwenda Polisi, lakini *final decision* ilikuwa ni kwa *TRA* kuwafungia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala nilijibu mimi, kwa sababu Bodi tayari imeshafanya maamuzi yake, hatua inayofuata ni kwa *Kisiwani Enterprises* kwenda kwa *Tax Revenue Appeal Board,* waka-*appeal,* waka-*revoked* hiyo *decision* ya *TRA*, hapo sasa ndipo *TRA* wataweza kukaa na kuanza kuliangalia suala hili. Kwa hiyo, tunaomba wafuate huo utaratibu uliopo kwa ajili ya suala lao kutazamwa upya. Namwomba Mheshimiwa Nassib Omar awasiliane na hao watu kwamba waanze maandalizi ya kwenda *Tax Revenue Appeal Board*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala lingine la Mheshimiwa Rajab kuhusu kodi ya majengo, kweli muda wa *TRA* kwa ajili ya kufanya kazi hii umemalizika na kweli *capacity* ilikuwa ndogo kutoka na *complexity* ya Taasisi hizi. Katika mpango wetu wa *Big Result Now,* tunaandaa *system* ya kuweza ku-*strengthening capacity* ya Halmashauri zenyewe ziwe zinaweza kukusanya kodi ile kwa sababu hata tukiirejesha, itarudi kwa sababu mwezi Juni ndiyo mwisho wa mkataba wa *TRA* kukusanya kodi hii lakini bado hii itakwenda sambamba na kuweza ku-*strengthening capacity* ya Halmashauri kuweza sasa kukusanya zile kodi kama inavyostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Muendelee.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu kwa niaba ya Waziri wa Fedha swali alilouliza Mheshimiwa Zungu kuhusiana lini sasa makampuni ya simu yataingia kwenye *stock exchange* kama vile ambavyo nchi jirani zinazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako kuwa sasa hivi *Capital Market and Securities Authority* wameshakamilisha kanuni zitakazowezesha makampuni ya migodi ya madini pamoja na makampuni ya simu kuingia katika soko la hisa. Wao wamependekeza kuwa ubia huu kwa mfano kama Serikali itaingia katika ubia huu, basi tutakuwa na asilimia 30 ya hisa katika makampuni ya migodi. Vilevile inapendekeza kuwa katika makampuni ya simu Serikali iwe na ubia wa asilimia 25 na kuwe kuna *conditions* ambazo zitawekwa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa aidha iwe ni asilimia 25 au namba ya wanunuaji wa hizo *shares* au utaratibu mwingine ambao unaenda sambamba na usimamizi huo. Kwa sasa hivi Serikali imeamua kuwa hili suala inalifuatilia kwa karibu na litafanyika kwa sababu inaonekana kuwa wao wenyewe wakiachiwa hawana shauku sana kuingia katika soko la hisa lakini sisi kama wadau wakubwa Serikali tunahitaji ifanyike ili tuwe na *control* zaidi katika makampuni haya.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lililoletwa na rafiki yangu Tundu Lissu, ni suala zuri hata mimi ningeuliza. Nitoe tu ufafanuzi kiujumla, ni kwamba matumizi ya shilingi trilioni 1.6 ni deni ambalo limeshalipwa yaani ni fedha zilizolipwa na shilingi trilioni 2.227 ni matumizi ya Fungu 22 ya deni la Taifa. Kama kuna maandishi yalienda vibaya basi tunaomba radhi lakini ndiyo ufafanuzi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ya pili, alikuwa anataka kujua orodha ya madeni haya tunakowekeza. Kwa kuwa imeulizwa orodha, naomba angetupa nafasi tukaitayarishe ili mbele ya safari iweze kuwasilishwa.

**MWENYEKITI:** Nilimhurumia tu akauliza maswali mawili inatakiwa moja lakini kutoa orodha baadaye si vibaya. Endelea bado kuna swali lingine.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zungu ameeleza umuhimu wa makampuni ya simu kujiunga na *stock exchange* ili watakaonunua hisa waweze kunufaika. Ni hoja nzuri, lakini nitoe ufafanuzi tu

kwamba sasa hivi tunavyozungumza *CMSA* wameshapeleka Shirika husika *TCRA* ili badaye zichambuliwe kwa ajili ya kufanikisha ombi alilosema. Kampuni ambazo *CMSA* wameshapeleka mapendekezo kwa ajili ya *listing* ni kampuni za madini pamoja *Telecom companies* kama alivyosema Mheshimimwa Zungu.

**MWENYEKITI:** Suala la Mheshimiwa David Kafulila hamjajibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Betty Machangu ametaka tufafanue kwa nini basi mashirika yale ambayo yalibinafishwa lakini hayatumii nafasi zile kwa mujibu wa Mkataba yasiwe *revoked* na kwamba *CHC* inafanya nini katika kazi yake ya kuangalia mashirika hayo. Napenda kufafanua kwamba dakika hii tunapozungumza, *CHC* wameshatayarisha tathmini ya makampuni yote na ipo tayari kwa ajili ya kuifanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Bado kuna swali la Mheshimiwa Soni na Mheshimiwa David Kafulila hamjajibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kafulila ameuliza swali kwamba *NBC* wapo kwenye ile *credit portfolio list,* kuna mikopo inayofikia shilingi bilioni 60, benki wakati huo ilikopesha watu ambao sasa hivi hawalipi. Aliuliza kwa nini basi wale waliokopesha nao wasichukuliwe hatua kwamba walikopesha watu wasio na uwezo wa kulipa au walikopesha bila kuangalia *effectiviness* ya matokeo ya kukopesha na kupoteza fedha. Katika hali halisi ya ukopeshaji, kuna njia tatu ambazo lazima ziangaliwe. Kwanza, je, wale waliokuwa wanakopesha ni kweli walikopesha nje ya taratibu za ukopeshaji au yule aliyekopeshwa alikuja akajiweka akawa mwovu mwenyewe badala ya kurudisha pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi watu wanakuja kukopa katika mabenki wakionyesha kila dalili iliyo njema, mara wanapopata fedha kwa kupata misukosuko au kwa tabia zao kubadilika basi hilo ndilo linakuwa tokeo. Wakati

mwingine si sababu ya mkopeshaji lakini pale inapobainika kwamba na mkopeshaji alikiuka kanuni za ukopeshaji akawa sehemu ya tatizo la kukopesha mtu asiyeweza kulipa, taratibu za mabenki yenyewe zipo wazi kuwachukulia hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo, Serikali haina taarifa kwamba wale waliokuwa wanakopesha mpaka sasa hivi benki ile inadai shilingi bilioni 60 kutoka kwa waliokopeshwa ambao hawajarudisha na kama walikuwa nao sehemu ya tatizo lakini hiyo ndiyo hali halisi ya kazi za ukopeshaji. Kama kweli ikibainika mkopeshaji alikuwa sehemu ya tatizo ni lazima *system* itamchukulia hatua na *system* wenyewe ni mabenki yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, taratibu za benki zenyewe ikiwa deni lile litaonekana limeshindikana, wana taratibu kwanza ya *restructuring*, wanamhusisha mkopaji ajieleze ana tatizo gani, kama bado kuna *viability propositions* ambazo zinaonyesha kwamba tatizo lililosababisha asilipe linaweza likaangaliwa kwa mapana mengine, benki huwa zinasikiliza na kuangalia namna ya kumsaidia mkopaji. Pili, ikiwa *market conditions* na *viability position* ya Shirika haipo, benki yenyewe lazima ikubali kuchukua hasara kwa niaba ya mkopeshaji. *Proposition* ya tatu ni kwamba kama mkopaji bado yupo, mali zipo na *security* iliyochukuliwa kwa mkopo ule basi inategemea benki ile ilichukua mkopo ule na kuweka rehani ya *security* ya aina gani. Kama ni *legal mortgage* au *other securites kama guarantees,* wana-*reinforce securities* ili ziwe-*realised* na mkopo urejeshwe. Inaweza ikatokea kwamba pale wanapojaribu kuchukua hatua au *security* zile hazipo au hazikuchukuliwa, kwa hiyo, hapo ndipo linapogeuka kuwa tatizo la benki kuwa na mkopo usioweza kuwa-*recovered*. Sasa itategemea hali halisi iliyokuwepo na kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge mwenyewe kwamba ulikuwa mkopo wa shilingi bilioni moja, mimi kama upande wa Serikali sina uhakika kama kweli ulikuwa mkopo wa shilingi bilioni moja sasa kwa sababu ya riba ikafikia shilingi bilioni 60, hili ni suala ambalo linatakiwa lifanyiwe tathmini katika hali halisi ya kilichotokea.

**MWENYEKITI:** Bado swali moja la Mheshimiwa Soni.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Jitu Soni kuhusiana na Sheria ya Manunuzi kuwa itapitiwa lini? Naamini labda alikuwa hayupo wakati tunajibu, sasa hivi tupo katika utaratibu wa kuainisha zile sheria ambazo zinashabiana, Sheria ya *PPP* na Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 ili kuondoa mgongano wote ambao utajitokeza kabla ya kuanza sasa kupitia ile Sheria yenyewe ya Manunuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa vile sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba kutoa hoja ya kuondoa shilingi katika mshahara wa Waziri ili hili suala lijadiliwe na Kamati yako ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kuna kauli mbili hapa za Serikali na Waziri hajazitolea ufafanuzi. Kauli ya hotuba yake kwamba tumetumia shilingi trilioni 1.666 kulipa deni, hiyo ni ya kwanza na kauli ya pili, tumetumia shilingi trilioni 2.227 kwa matumizi ya Fungu 22. Fungu 22 ni la deni la Taifa, matumizi ya Fungu 22 hayawezi yakawa mengine zaidi ya kulipa deni la Taifa. Kwa hiyo, atwambie Mheshimiwa Waziri na nimemsikia akisema kwamba kuna makosa mahali fulani hajayaeleza ni makosa gani, kama Wizara ya Fedha ambayo ndiyo imekabidhiwa jukumu la kusimamia hazina ya Taifa hili inaleta kauli mbili zisizoeleweka, fedha zetu zipo salama kiasi gani? Tutashangaa kweli tunaposikia wizi kama wa miaka iliyopita wa mabilioni ya *EPA* ya madeni hayahaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tafadhali, Mheshimiwa Waziri atueleza katika hizi kauli mbili, ipi ipo sahihi. Tumetumia shilingi trilioni 1.666 au tumetumia shilingi trilioni 2.227 kulipa deni la Taifa na kama kuna kosa Waziri afafanue ni kosa lipi lililofanywa na Wizara, wataalam mamia wa Wizara hawakulliona mpaka limeletwa Bungeni hapa anakuja kukiri

kwamba kuna makosa. Majibu haya rahisirahisi haya hayatatosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono, hili suala la deni la Taifa ni msalaba mkubwa kwa Taifa. Mimi nilikuwa naangalia kwenye kitabu hiki. Kwenye kitabu hiki, Fungu 22, fedha tunazoambiwa tuidhinishe mwaka huu kwa ajili ya kulipa riba tu ya deni la Taifa, ni shilingi trilioni 1.29, ni mapesa mengi kweli kwa *interest payments alone,* zipo kwenye kitabu hiki. Sasa kama hatupewi majibu yanayotosheleza ni kipi kinalipwa kwa kweli tunaweza tukawa tunapitisha fedha hapa zinakwenda kwenye mifuko binafsi, nchi yetu inazidi kuagamia kwa sababu ya malipo ya aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono, suala hili lijadiliwe, suala hili ni kubwa, ni zito, niungeni mkono tupate majibu sahihi kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unajua, tatizo hata mimi ni Mhasibu, unajua mahesabu hayana lugha mbili, mimi nakuambia wengine watakaounga mkono hapa, watatupigia kelele tu hapa sisi laiti ungekuwa umeandaa watu na kuwafundisha haya matrilioni, sasa Waziri tujibu tena, hata Naibu unaweza kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA SALUM MKUYA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa rafiki yake, mie kaka yangu naomba...

**MWENYEKITI:** Naomba mzungumze kwa taratibu mpaka sisi wote ituingie vizuri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA SALUM MKUYA):** Sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha kwanza cha 17 na kama utaangalia vizuri *title* yake ni usimamizi wa deni la Taifa ambapo hapo kuna malipo ya madeni ambayo yamefikia shilingi trilioni 1.6. Nachotaka kuelezea ni kwamba kifungu hiki kingine cha 127, ni deni la Taifa. Kweli kwa mtu ambaye hayupo katika mahesabu inaleta *confusion*. Ndipo pale ambapo Mheshimiwa Waziri alipoona kwamba pengine kama kutakuwa kuna makosa kwa sababu yeye alisoma *summary*, lakini kitabu hiki kipo. Deni la Taifa ni *vote* nzima yaani ile *vote* 22 inajulikana ni deni la Taifa lakini ndani yake mna hilo deni, mikopo tuliyokuwa tumekopa ndani, lakini vilevile kuna vitu vingine vingi. Kwa mfano, *vote* ya deni la Taifa, *vote* 22 ndani yake mna hilo deni la Taifa ambayo ni shilingi trilioni 1.6, lakini ndani yake kuna fedha ambazo zimewekwa kwa ajili ya michango ya kulipia katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yaani michango ya wafanyakazi wote imo katika hiyo *vote* 22. Vilevile kuna michango ya kulipia Bima ya Afya inayotokana na mishahara, kwa hiyo, inalipiwa kule. Pia ndani ya *vote* hiyohiyo 22 ambayo inajulikana kama deni la Taifa ndani yake kuna stahili za Maafisa wa Serikali ambao wanalipwa malipo yao kupitia deni la Taifa, kwa mfano, Makamishna hawa wa Tume ya Kurekebisha Sheria, mishahara yao na mafao yao yote yamo humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachotaka kuelezea hapa ni kwamba deni la Taifa ni *title* kubwa, ni *vote*, lakini ndani yake kuna vipengele vingi. Kuna hilo deni la Taifa, kuna matumizi kama hayo ya kulipia wafanyakazi ambao wanastahili kulipwa kutokana Fungu hili, kuna matumizi ya kulipia Bima za Afya, kuna matumizi ya kulipia Mifuko ya Pensheni na ndiyo hii yote sasa kwa umoja wake ndiyo imewekwa katika hicho kipengele cha 127 ile ya kule 17 ni kile ki-*component* kidogo tu cha kulipia yale madeni yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya majibu kwa kweli hayatoshelezi kabisa. Haiwezekani, kama haya anayoyasema Mheshimiwa Naibu Waziri ni ya kweli yangesemwa katika hotuba yao kwamba tunapozungumzia Fungu 22 – Deni la Taifa tunazungumzia na mishahara, posho, zote hizo ambazo anazisema sasa hivi. Ukiliacha hivi, ukasema kwamba matumizi ya Deni la Taifa matrilioni yote haya, nani atakayeelewa kwamba kwenye posho mmelipa kiasi gani, kwenye michango ya Mifuko ya Jamii mmelipa kiasi gani, haiwezi kuwa hivi, hii ni ya jumla, haiwawezeshi Waheshimiwa Wabunge kupata ufahamu wa namna hizo fedha zimefikia idadi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona watu wanagunaguna, hili suala sio dogo kama Serikali inaleta mahesabu ya jumlajumla na kama alivyosema Waziri kuna makosa yamefanyika, ni ukosefu wa umakini. Huwezi ukaleta *figure* ambazo hazielezeki. Tukiuliza ndio unaanza oooh unajua, haiwezekani tunataka tuletewe taarifa ambazo zinaelezeka. Mtu ukimweleza kwamba hii *figure* ya shilingi trilioni 2.227 inatokana na vitu hivihivi inajieleza yenyewe katika hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa siku nyingine, kwa kesho na kesho kutwa Mheshimiwa Waziri na watu wako mlete Bungeni vitu vilivyopikika vikaiva. Hivi vitu *half cooked*, havitakubalika siku zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waziri kuna maelezo mengine labda uki-*clear* ile ya kusema ulisema kuna makosa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusema kuna makosa. Nimesema kama maelezo hayakueleweka, hakuna makosa. *Vote* 22 iko wazi na mimi nikaruhusu Naibu Waziri ili tutumie mdomo mwingine lakini hakuna makosa yoyote, *I have all the details here*, kwa hiyo hakuna kubabaisha hapa, kila kitu kiko-*clear.* *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unajua kila mtu na fani yake, mimi nimeelewa kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*..........Tshs. 1,287,129,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*................Tshs. 29,311,935,000/=
Kif. 1004 - *Legal Services*..........................Tshs. 842,046,000/=
Kif. 1005 - *Government Comm. Unit*.........Tshs. 1,092,517,000/=
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit* ....................Tshs. 377,886,000/=
Kif. 1007 - *MCC Tanzania*..........................Tshs. 500,000,000/=
Kif. 1008 - *Procurement Mgt. Unit*...................Tshs.617,381,000/=
Kif. 3001 - *Internal Auditor General*.........Tshs.3,610,951,000/=
Kif.5001-*Government Asset Management Div*...........................Tshs.4,520,908,000/=
Kif. 6001 - *Financial Mgt. Inform. Systems Division*.......................Tshs. 2,951,519,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu la 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

Kif.1001 - *Administration and HR Management*.........................Tshs.1,610,389,000/=
Kif. 1002 - *Internal Audit Unit* ........................Tshs.71,090,000/=
Kif. 2001 - *Technical Department*.................Tshs.269,360,000/=
Kif. 2002 - *Zanzibar Office*...........................Tshs.113,585,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu la 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*......................Tshs. 1,132,777,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*..........Tshs. 62,290,000/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*...........................Tshs.32,753,000/=
Kif. 1004 - *Monitoring Unit*...........................Tshs.344,810,000/=

Kif. 1005 - *Inspection Unit*……….................…Tshs.123,150,000/=
Kif. 1006 - *Procurement Mgt. Unit*...................Tshs. 14,570,000/=
Kif. 1007 - *Legal Service Unit*…......................….Tshs. 19,420,000/=
Kif. 1008 - *Management Information Systems Unit*…................................Tshs.215,020,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu la 21 – Hazina**

Kif. 1009 - *Public Procurement Policy Unit (PPU)* ……….....................Tshs.1,142,312,000/=
Kif. 2001 - *Government Budget Division*…...............Tshs.1,170,668,174,000/=
Kif. 2002 - *Policy Analysis Division*……...Tshs.196,226,540,000/=
Kif. 4001 - *External Finance Division*….........Tshs.6,535,158,000/=
Kif. 4002 - *Public Private Partnership Unit*............................................Tshs.1,032,400,000/=
Kif. 7001- *Poverty Eradication an Empowerment*…......................Tshs.2,537,982,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 22 – Deni la Taifa**

Kif. 1001 – *Administration ande HR Management*…................Tshs. 3,319,017,772,000/=

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi wa kasma 250500 -*Interest Payments on Long-term Debt to Other General Government Units* ambayo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 311 za mwaka jana mpaka shilingi bilioni 424.7 za mwaka huu. Naomba nipate ufafanuzi haya malipo ya riba yameongezeka kwa kiasi kikubwa hiki kwa sababu gani kwa zaidi ya shilingi bilioni 114, ni sababu zipo ambazo zinafanya malipo ya riba tu yaongezeke kwa kiasi kikubwa hivi katika kasma hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, si umeiona kasma anayoizungumzia?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inazungumzwa *interest payments,* hii ni *cost of borrowing*. Hii ni gharama ya ku-*service* mikopo ambayo ilikopwa muda mrefu. Tuko katika kipindi cha *convergence*, tuna mikopo mingi tuliyokopa miaka ya 20, 30, 40 sasa ina-*mature*. Huko nyuma tumekuwa na *moratorium period* ya muda mrefu sasa *maturities* zimeingia. Sasa kadri *maturities* zina-*converge, volume* ya ulipaji nayo inakuwa kubwa. Kwa hivyo, riba ni mkusanyiko wa madeni ambayo tulikopa kwa muda mrefu huko nyuma lakini si kwamba riba ya mikopo tuliyochukua leo au juzi.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu la 45 – Ofisi Taifa ya Ukaguzi**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*...........Tshs.25,095,005,300/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*...Tshs. 2,259,605,600/=
Kif. 1003 - *Internal Audit Unit*..........................Tshs.574,033,400/=
Kif. 1004 - *Ministerial Audit Division*............Tshs. 7,702,036,600/=
Kif. 1005 - *Regional and Local Govt Audit Division*....................... Tshs.11,781,903,800/=
Kif. 1006 - *Value For Money Audit Div.......*Tshs.2,260,942,000/=
Kif. 1007 - Tr*easury Audit Division*..............Tshs. 3,076,793,000/=
Kif. 1008 - *Techn. Support, Research and Consultancy* ..................Tshs. 4,656,094,300/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*…............Tshs.1,665,300,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu la 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*…................Tshs.399,685,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 21 – Hazina**

Kif. 1009 - *Public Procurement Policy Unit (PPU)*….......................Tshs. 876,000,000/=
Kif. 2001 - *Government Budget Div*....….Tshs. 3,748,000,000/=
Kif. 2002 - *Policy Analysis Division*…..........Tshs.22,458,234,000/=
Kif. 4001 - *External Finance Division*….......Tshs. 9,217,928,000/=
Kif. 7001 - *Poverty Eradication and Empowerment*...........…Tshs. 1,890,000,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kif. 3003 - *Financial Management*….........Tshs. 2,590,147,000/=
Kif. 3004 - *Financial Systems* ......…......Tshs. 1,646,400,000/=
Kif. 4001 - *Local Government Finances*…..Tshs.519,000,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*........................Tshs. 7,500,000,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*................................................Tshs. 6,199,100,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 50 – Wizara ya Fedha**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*....................... Tshs. 407,000,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*…. ............ Tshs.11,183,488,000/=
Kif. 1005 - *Government Communication Unit*....................Tshs. 623,500,000/=
Kif. 1007 - *MCC Tanzania*...................... Tshs. 213,612,181,000/=
Kif. 3001 - *Internal Auditor General*............Tshs.2,639,000,000/=
Kif. 5001 - *Government Asset Mgt. Div…. Tshs*. 2,510,000,000/=
Kif. 6001 - *Financial Mgt. Inform System Division*...............Tshs.2,694,000,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na mabadiliko yake. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi kwa Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, napenda nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, Mawaziri akina mama, kwa kazi nzuri kabisa waliyoifanya mpaka tumeshindwa kuwa na maswali mazito. *(Makofi)*

Pia ni kwa sababu ya kazi nzuri ambayo Hazina na wasaidizi wao wamefanya lakini kama walivyosema wachangiaji, leo michango ya Wizara yenu ilikuwa *one of the best*, wachangiaji waliochangia leo walichangia vizuri mpaka tunasahau kugonga kengele. *Message* ambayo waliileta katika michango yao, tuimarishe ukusanyaji wa mapato. Nadhani ndio *message* iliyokuwepo na kuweza kuziba mianya mbalimbali ambayo inaweza kuwa ni sababu ya kuondoka matumizi kwa sababu kuomba tu fedha bila ya kutumia zile tulizonazo vizuri na kutafuta nyingine kwa kweli tutashindana humu ndani. Kwa hiyo, tunawapongezeni muendelee kufanya kazi iliyo njema na tunawasubiri tena tarehe 13, nadhani mtaelewana na *budget committee* yangu.

Waheshimiwa Wabunge, kesho tutakuwa na maswali asubuhi halafu tutakuwa na Uchaguzi wa nafasi zilizotangazwa juzi, naomba wote mhudhurie.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawatakieni jioni njema, naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.6 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 7 Juni, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*